

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 8 Julai, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali na tunaanza na ofisi ya Waziri, Mheshimiwa Kayombo, kwa niaba yake Mheshimiwa Rage.

Na. 321

**Ofisi kwa ajili ya Tarafa-Mbinga**

**MHE. ISMAIL A. RAGE (K.n.y. MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO)** aliuliza:-

Wilaya ya Mbinga ina tarafa sita lakini tarafa zote hazina ofisi rasmi zilizojengwa:-

Je, ni lini Serikali itajenga ofisi kwa Makatibu Tarafa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma una jumla ya tarafa 24 yaani Tunduru wako saba, Mbinga wana tarafa sita, Nyasa wana tarafa tatu, Namtumbo wana tarafa tatu na Songea wana tarafa tano. Ni kweli tarafa za Wilaya ya Mbinga hazina ofisi rasmi zilizojengwa na Serikali. Ujenzi wa hizo ofisi unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sasa Mkoa wa Ruvuma umeweka kipaumbele katika ujenzi wa ofisi nne za tarafa katika Wilaya ya Nyasa na Tunduru. Tarafa hizo ni Luhuhu (Lituhi-Nyasa), Ruhekei (Mbamba bay-Nyasa), Mpepo (Tinga-Nyasa) na Nampungu (Nandembo-Tunduru).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Mkoa ulitenga shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Tarafa ya Luhuhu (Lituhi), Ruhekei (Mbamba bay), Mpepo (Tingi) na Nampungu (Nandembo). Mpaka sasa mkoa umeshapokea kiasi cha shilingi milioni mia moja na hamsini ili kuendelea na ujenzi wa miradi hiyo. Ofisi za Tarafa ya Ruhekei, Luhuhu na Nandembo zimekamilika. Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Mkoa umetenga kiasi cha shilingi 140, 337,239 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ofisi za tarafa. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 75 zitatumika kukamilisha ofisi ya tarafa ya Mpepo na shilingi 65,337,000 zitatumika kukamilisha kulipa deni la mkandarasi aliyejenga ofisi ya tarafa ya Nandembo katika Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kuhakikisha tarafa zote zinakuwa na ofisi. Mkoa umejipanga kutekeleza ujenzi wa ofisi hizo kwa awamu kutokana na ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na mahitaji makubwa yaliyopo ya ujenzi wa ofisi hizo na majengo mengine ya Serikali. Serikali inaendelea kuwasisitiza wananchi na wadau mbalimbali kushiriki katika ujenzi wa mjengo mbalimbali ili kuharakisha ukamilishaji wa majengo hayo ikiwemo ujenzi wa ofisi za tarafa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rage.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namheshimu sana rafiki yangu Naibu Waziri lakini leo majibu yake hayakuniridhisha hata kidogo. Mimi nauliza swali linalohusu Wilaya ya Mbinga, yeye ananieleza Wilaya za Nyasa na Tunduru. *Interest* yangu mimi ni kutaka kujua tarafa sita ambazo ziko Mbinga lini ofisi zake zitaanza kujengwa basi ni hilo tu. Naomba maelezo hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niliweke hili jambo vizuri kwa sababu najua kwa nini anasema ananishangaa. Ofisi za halmashauri zinajengwa na halmashauri. Ofisi hizi nazozitaja hapa si za Halmashauri ni za Serikali Kuu. Afisa Tarafa anawajibika kwa Mkuu wa Wilaya. Kwa hiyo, napozungumza habari ya mkoa, hela zote tunazozungumza hapa zinapita kwa Katibu Tawala wa mkoa ndipo zinakwenda pale Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kweli tu, anachosema Mheshimiwa Gaudence Kayombo hapa kwamba hakuna ofisi ambayo imejengwa pale ni kweli. Mimi ninayo orodha hapa ngoja niwaeleze vizuri ili nieleweke nachozungumza na nisome. Mbinga mjini wako katika ofisi ya jengo la ushirika, Kigonsera wako katika ofisi ya VEO (*Village Executive Officer*), Luanda wako katika ofisi ya kijiji, Mkumbi wako katika ofisi za kijiji, Mbuji wako katika ofisi za kijiji, ofisi hiyo ni ya zamani sana na mikakati iko hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nikizungumza habari za halmashauri kwamba wamejenga hapa si atatoka Rage tena ataniambia umesema uongo hapa. Ofisi zote nazokuambia hapa haziingii katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga zinapita kwa Katibu Tawala wa Mkoa na jitihada nilizozionyesha hapa ni hizo tunazozungumza hapa. Kwa hiyo, napoeleza hela zilizokwenda nikataja mimi Nandembo, Tunduru, ni kwa sababu hela zote zinafikia Mkoani pale kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sisi tunatambua kwamba kuna tatizo kubwa hapa na ndiyo maana tumejibu kuhusu jitihada tunazozifanya hapa, ni pamoja na kuhamasisha wananchi kupitia ofisi za Wakuu wetu wa Wilaya watusaidie kuchangia ofisi hizi kama ambavyo tumekuwa tunafanya katika maeneo mengine. Kusema Wilaya zile nyingine nilisema kwa sababu ofisi inayohusika ni ya Katibu Tawala wa Mkoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza, niseme tu kwamba tatizo la nyumba za Maafisa Tarafa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu kwa sababu Afisa Tarafa wa Tarafa ya Ibindo, Wilaya ya Kwimba ana kata nane na Maafisa Tarafa wengine lakini hawana usafiri ili waweze kuwafikia wananchi. Mtu mmoja anazungukia tarafa saba, nane au tisa lakini hana usafiri. Serikali ina utaratibu gani kama ilivyokuwa zamani kwa hawa Maafisa Tarafa kuwapelekea pikipiki ili waweze kufika kwenye maeneo yao ya kazi bila kuchelewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ametaja Tarafa ya Ibindo na anazungumza habari ya kata. Kwa upande wa kata, ni kweli kata hizi ziko chini yetu katika maana ya halmashauri. Kwa maana ya tarafa inabidi niende nikaiangalie hiyo lakini ni kweli pia kama anavyosema Mheshimiwa Richard Ndassa tumekuwa na utaratibu wa kusaidia ofisi zetu za Maafisa Tarafa kupata pikipiki. Kwa hiyo, nitakwenda kufuatilia kwanza kujua hii Ibindo iko katika utaratibu gani lakini ni jambo ambalo linazungumzika. Kwa upande wa pikipiki ni kweli kabisa kwamba tumekuwa na utaratibu wa kusaidia Maafisa wetu wa Tarafa wafanye kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hilda.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na maelezo mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, napenda kumuuliza swali moja dogo tu la nyongeza kwamba yapo majengo mengine ambayo yalijengwa wakati wa mkoloni, majengo ya Makatibu Tarafa ambayo yako katika Makao Makuu ya Tarafa. Kwa mfano, kuna jengo kubwa sana la Tarafa ya Ukukwe, Wilayani Rungwe, Tarafa ya Pakati na Busokelo, majengo haya yamechakaa na hayafanyiwi matengenezo yoyote lakini yangeweza kufaa kabisa kwa kazi za Maafisa Tarafa. Je, Serikali ina mpango gani basi wa kuweza kuyakarabati majengo haya ili yaweze kurudi tena katika upya uleule wa zamani? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa anachozungumza hapa ni kwamba kuna majengo haya ambayo yanaonekana yamechakaa na kama tulivyofanya katika Halmashauri ile ya Wilaya ya Mbinga ambayo nimeulizwa mara ya kwanza ni jambo ambalo tunaweza tukafanya lakini watako-*coordinate* hii habari itakuwa ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kupitia Katibu Tawala na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kupitia Katibu Tawala wa Wilaya, tutakwenda kuangalia hali yake. Tatizo letu ni bajeti kwa sababu katika *Regional Secretariat* hakuna mahali popote ambapo tunazalisha mali wanategemea zaidi ruzuku ya Serikali na kama nilivyoeleza hapa hela zilizokuwa zimekwenda pale zilikuwa ni shilingi milioni mia tatu. Sasa nitakwenda kuangalia pia kama hizi hela zinaweza zika-*spread over* zikaangalia pia katika maeneo haya anavyosema ya Ukukwe katika Wilaya ile ya Busokelo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Bungara kwa niaba yake Mheshimiwa Shah.

Na. 322

**Tatizo la Maji Hospitali ya Wilaya ya Kilwa**

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA)** aliuliza:-

Kila mwezi Juni hadi Desemba kila mwaka Hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga) hukabiliwa na tatizo kubwa la maji kutokana na visima kushindwa kutoa maji kunakosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi na wakati mwingine hukauka kabisa na kusababisha adha kubwa hospitalini hapo kwa magonjwa ya mlipuko:-

Je, Serikali haioni haja ya kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga mfumo rasmi wa kuvuna maji ya mvua kama njia sahihi ya kutatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga) kwa sasa inapata maji kiasi cha mita za ujazo kumi na tano sawa na asilimia 32 ya mahitaji yake halisi kutoka katika chemchem ya Kitumba pamoja na kisima kirefu kilichochimbwa kupitia mradi wa TASAF ambacho kinatumiwa pia na wananchi wa Kivinje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na tatizo la maji katika Hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga) mwezi Aprili, 2015 Halmashauri imenunua pampu ya kuendeshwa kwa umeme na kuifunga kwenye kisima kilichochimbwa na Kampuni ya Utafiti wa Mafuta ya RAK-Gas kwa ajili ya kupeleka maji katika Hospitali ya Wilaya. Kisima hiki kinatumika kwa sasa na kina uwezo wa kutoa kiasi cha lita elfu moja kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri imetumia kiasi cha shilingi milioni ishirini na nane kwa ajili ya uchimbaji wa kisima kirefu chenye uwezo wa kutoa lita ishirini na sita elfu kwa saa ili kukabiliana na tatizo la maji katika Hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga). Hatua itakayofuata ni ujenzi wa miundombinu ya kisima hicho kama vile mabomba yatakayotandazwa katika umbali wa zaidi ya kilomita kumi kutoka kilipo kisima. Ununuzi wa pampu yenye uwezo wa kutoa lita za maji ishirini na sita elfu kwa saa, kuweka umeme kwenye chanzo na ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita laki mbili.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri pia ina mpango wa kuvuna maji ya mvua ambapo iliomba wataalamu kutoka *Ndanda Mission* ambao walifanya tathmini ya kutoa ushauri ingawa mpango huu hauwezi kutoa suluhisho la kudumu la tatizo la maji hivyo utatumika kama chanzo cha maji ya ziada kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na ambayo inapata mvua kwa miezi minne tu kwa mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shah.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba kumuuliza pamoja na jitihada za Serikali ya kuhakikisha inaondoa kero ya maji katika Hospitali ya Kinyonga pamoja na mji wa Kivinje, huo mpango ambao wamesema wa kuhakikisha hiyo miundombinu ya mabomba ambayo ni muhimu katika kuhakikisha maji yanapatikana mpaka kwenye wodi bila ya watu kutoka nje ya Hospitali ya Wilaya na kwenda kuchafua mazingira, ni lini yatakamilika? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali imeweza kufanikisha miradi mingi kupitia Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia lakini miradi ile mingi pia imekwama kwa sababu ya Serikali hiyohiyo kushindwa kupeleka pesa na kuwamalizia kuwalipa wale wakandarasi ambao wanaifanya kazi hiyo. Je, ni lini Serikali itakamilisha pesa hizi na kuwapatia hawa wakandarasi ili miradi hii iweze kukamilika? Kisiwa cha Jibondo ambacho tayari kimeshatengewa pesa lakini mpaka dakika hii mradi haujaanza, watu wanaadhibika na sisi viongozi tunaonekana si wa kweli. Leo Waziri atamke kwamba, je, huo mradi upo au haupo wakati pesa na mpango upo wa kununua *pipe* za maji kwa ajili ya kuvusha maji kutoka kisiwa kikuu cha Mafia kwenda kisiwa cha Jibondo. Ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na majibu ya msingi aliyotoa Mheshimiwa Waziri kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha inaondoa tatizo la maji katika hospitali hii ya Kilwa Kinyonga. Mimi nilikuwa huko Kilwa na maeneo haya nimefika, kwa hiyo, mara tu ambapo tutapata fedha sisi tutahakikisha azma hiyo ya Serikali inatekelezwa. Nyongeza ya hapo ni kwamba mwaka huu wa fedha kwa bajeti iliyopita tumetenga shilingi milioni mia tano lakini zuri zaidi kwa ajili ya kuondoa tatizo kabisa la Kilwa Kivinje, Masoko, Nangurukuru ni kwamba tayari kuna mpango Wabelgiji wanatoa fedha *Euro* milioni hamsini na tayari suala hili sasa tumelipeleka Tume ya Mipango ili kumaliza kabisa tatizo la maji katika Mji wa Kilwa.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nikubaliane na Mheshimiwa Shah na amekuwa akifuatilia mara kwa mara miradi ya vijiji kumi lakini pia katika kisiwa cha Jibondo. Nimhakikishie tu kwamba mara Wizara ya Fedha itakapotupa fedha na hili nilijibu kwa Wabunge wote, sisi Wizara ya Maji hatutakuwa sehemu ya tatizo, tutakapopata fedha tutazipeleka katika halmashauri ili miradi hii itekelezwe ikiwemo katika kisiwa cha Jibondo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zainab Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kina mama walioko katika Wilaya ya Liwale wamenituma niwasilishe kilio chao hususan kutoka kwenye maeneo ya Ngongowele, Mirui, Lilombe, Kibutuka na Kiangara kwa uchache, wana shida kubwa sana ya maji, wanaomba Serikali itoe kipaumbele katika maeneo hayo. Mimi naomba kutumia nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuomba Serikali itakapopata pesa na kwa kuwa bado Serikali yangu sikivu itaendelea kuwepo madarakani mpaka mwezi wa kumi, naomba itoe kipaumbele kwenye maeneo haya ili wanawake wa Wilaya hiyo ya Liwale wasipate tena shida ya maji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshajibu swali hili hapa ndani ya Bunge lakini kwa rai aliyotoa kwa maeneo yote aliyoyataja ikiwepo Mirui, kama nilivyosema katika jibu la msingi tutatoa kipaumbele kuona kwamba miradi hiyo inatekelezwa kadiri tutakavyopata pesa lakini kilio hicho tumekipokea na tutakifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika maeneo kame taasisi za Serikali zina matatizo makubwa ya maji. Je, kwa nini Serikali isitumie utaratibu wa kuvuna maji ya mvua katika majengo yote yaliyoko katika maeneo kame ili kusaidia maeneo hayo kupata maji wakati wa kiangazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana naye hasa kwa wilaya yake na kwa maeneo ambayo nilifika ni kweli ni maeneo magumu na ni makame na hakukupatikana vyanzo vya maji. Tunapokea ushauri huo lakini juzi nilijibu swali hapa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, tumeagiza halmashauri zote zitunge Sheria Ndogo Ndogo kuona kwamba majengo ya Serikali ambayo yanaweza kuwa na miundombinu

mizuri waweze kuvuna maji ya mvua. Tayari halmashauri 29 zimeshatekeleza na agizo letu ni kuona kwamba halmashauri zingine zote zinatekeleza hayo ambayo tumeyasema.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa na swali la Mheshimiwa Masele, kwa niaba yake Mheshimiwa Deogratias.

Na. 323

**Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Kujenga kwa Lami Barabara yenye Urefu wa Kilomita Moja (KM.1)**

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA (K.n.y. MHE. AUGUSTINO M. MASELE)** aliuliza:-

Tarehe 8/11/2014, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya ziara ya kikazi Wilayani Mbogwe, akiwa huko aliwaahidi wananchi wa Masumbwe kuwajengea barabara ya lami yenye urefu wa kilomita moja (Km.1):-

Je, ni lini ahadi itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyada Masele, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais mwaka 2013 aliahidi kuwa Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara yenye urefu wa kilomita moja katika Wilaya ya Mbogwe. Halmashauri imefanya tathmini na kubaini kuwa zinahitajika shilingi milioni 600 ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo. Maombi hayo yaliwasilishwa ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tarehe 22 Januari, 2015. Hata hivyo, maombi hayo hayakufanikiwa kwa sababu mchakato wa bajeti ya mwaka 2015/2016 ulikuwa uko hatua za mwisho kwa upande wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri inashauriwa kuangalia upya vipaumbele vyake na kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo kwa kiwango cha lami katika bajeti yake 2016/2017.



Hata hivyo, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa miradi ya barabara katika mwaka wa fedha 2015/2016 imeitengea halmashauri hii shilingi 1,078,470,000 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya madaraja na makalavati. Hivyo, ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deogratias.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Rais anatoa ahadi ya kujenga lami kilomita moja, Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Magufuli alikuwepo. Wananchi wa Mbogwe wangependa kujua Serikali imejipangaje kutekeleza ahadi hii na hasa wangependa kupata ile *timeframe*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ilishatoa ahadi ya kuweka lami nyepesi katika barabara za Mji Mdogo wa Ngara, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magufuli majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete akiwa katika Wilaya mpya ya Mbogwe alitoa ahadi kwa wananchi kwamba itengenezwe lami kilomita moja. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe na Mheshimiwa muuliza swali na Bunge hili kwa sababu katika bajeti ya mwaka huu fedha za Mfuko wa Barabara zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 751 hadi shilingi bilioni 866.6 na kwa sababu ahadi ya Rais ni lazima itimizwe na nina uhakika *Engineer* wa Wilaya hiyo ya Mbogwe pamoja na *Engineer* wa TANROAD wa Geita wananisikiliza, barabara hii ya kilomita moja itangazwe tenda mwezi huu na fedha zitatolewa kutoka katika Mfuko wa Barabara ili kilomita moja ianze kutengenezwa kama ambavyo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alivyoahidi katika Wilaya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara za lami nyepesi katika eneo la Mheshimiwa Ntukamazina, napo tutatumia fedha za Mfuko wa Barabara katika kuhakikisha ahadi hizo zinatimizwa. Kwa bahati nzuri Mfuko wa Barabara wakati akiingia madarakani Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ilikuwa ni shilingi bilioni 73 lakini mwaka huu ni shilingi bilioni 866.23. Kwa hiyo, ahadi hizo zitaweza kutekelezwa kadiri alivyoahidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa ahadi za Serikali ni pamoja na ahadi ya barabara inayotoka Iguguno kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama lakini kwenda hadi kwenye daraja la Sibiti. Mpaka sasa hivi pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikisema mkandarasi yuko *site* kitu ambacho si kweli, naomba kupata maelezo kutoka Serikalini tatizo hili la kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki, je, zitaishia lini ni leo au kitu gani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la daraja la Sibiti linahusu Wizara ya Ujenzi na tulikwishatoa maelezo hapa lakini napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mlata daraja lile tenda zilitangazwa kutengeneza lile daraja la Sibiti pamoja na kilomita 25 za eneo la daraja lile. Wakati mkandarasi akiwa kule baada ya kuanza kutengeneza zile *beams* katika mvua ambazo zilijitokeza mwaka huu eneo lote la daraja lile likawa limejaa maji, kandarasi akawa ameshauriwa asubiri mpaka maji yale yakauke na kwa sasa hivi tumeshatoa *instruction* mkandarasi yule ambaye ni kampuni ya Kichina arudi kwenye *site* ile kwa ajili ya kuendeleza kutengeneza lile daraja la Sibiti. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mlata kwamba daraja lile litatengenezwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ameshakubali kwenda kuweka jiwe la msingi katika daraja hilo ili kazi zikamilike. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa, Ofisi ya Utawala Bora, Mheshimiwa Hamad kwa niaba ya Mheshimiwa Mwidau.

Na. 324

### **Tatizo la Rushwa Nchini**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED (K.n.y. MHE. AMINA M. MWIDAU)** aliuliza:-

Rushwa ni adui wa haki na rushwa inasumbua sana nchi yetu kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiteknolojia na kufanya kuongezeka kwa umaskini:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kulinusuru Taifa letu na janga hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kujibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa tatizo la rushwa nchini na athari zake kwa uchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kutokana na hali hii, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza uelewa wa wananchi juu ya mienendo ya rushwa na umuhimu wa kushiriki kwao katika kuzuia na kupambana na rushwa na kuongeza wigo wa wadau wa mapambano dhidi ya rushwa kwa kushirikisha Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Mashirika ya Dini, Vyama vya Siasa, Vyombo vya Habari na Sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine ni kuwepo mfumo mzuri wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kunakuwepo na thamani halisi ya fedha na kuwaelimisha wananchi kutambua wajibu wao katika kusimamia miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao; kuimarisha maadili, uwajibikaji na kubadili tabia za wanasiasa, watendaji na wataalam katika vyombo vinavyolalamikiwa kwa kudai rushwa. Aidha, zinafanyika tafiti za udhibiti kwa kupitia mfumo ya taratibu mbalimbali zinazoongoza utendaji wa Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi ili kupima uzingatiaji na utekelezaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kuzishauri tasisi hizo namna bora ya kuzuia na kusimamia utekelezaji wa mfumo na taratibu zilizorekebishwa baada ya kubainika kwa mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa rushwa imeenea takribani kwenye taasisi zote kwa ujumla, napenda kuchukua nafasi hii kutoa rai kwa viongozi wa ngazi zote pamoja na wananchi mkiwemo na Waheshimiwa Wabunge kuwaomba kuwa sehemu ya juhudi za mapambano dhidi ya rushwa katika nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nina maswali mawili ya nyongeza. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba angependa kuona juhudi za viongozi mbalimbali katika kushughulikia rushwa. Katika Bunge la Tisa mimi nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati za Serikali na pia nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati za Serikali za SADC, tuliandaa utaratibu wa kuona ni namna gani tunaweza tukapambana na rushwa.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Moja tuliloligundua ni kwamba asilimia kubwa ya rushwa inatokana na manunuzi kwenye *procurement*, tukasema ni vizuri tuanzishe utaratibu wa kutumia *TEHAMA* katika ununuzi yaani *electronic procurement*. Tukaleta wataalam wakatumia, tukafanya *studies* mbalimbali na hatimaye hata sheria yetu ikabadilishwa ili tutumie *electronic procurement* kupunguza na kubana mianya ya rushwa. Ni kwa nini Serikali imekuwa na kigugumizi toka Serikali ya Awamu ya Tatu na hii ya Nne katika kutekeleza utaratibu huu ambao unatumika duniani kote ambako watu wamedhamiria kupambana na rushwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Mabunge yanayopambana na rushwa *GOPAC*, tulikubaliana kwamba hii *grand corruption* itafsiriwe kama ni kosa la kibinadamu yaani *crime against humanity*. Ni kwa nini Serikali inashindwa ku-adopt hii *system* ili tuone kabisa kwamba tuna dhamira ya kupambana na rushwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba asilimia kubwa ya pesa tunayopitisha hapa, asilimia 70 inaishia kwenye manunuzi na wanasema walipendekeza kuwe na utaratibu wa *electronic procurement* ili kupunguza mianya ya rushwa katika manunuzi. Napenda kumjibu kwamba Serikali imefanya maamuzi na imeagiza Wizara ya Fedha ilete mapendekezo katika Baraza la Mawaziri ili kubadilisha Sheria ya Manunuzi iweze kuendana na wakati. Tutakapofanya hilo, naamini kwamba pendekezo la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed tutalizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, anasema kwamba tuchukulie *grandcorruption* yaani rushwa kubwa tuichukulie kama ni makosa dhidi ya jamii, mimi napenda tu nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kuliona hilo. Mimi na yeye tulikuwa Bunge Maalum la Katiba, yeye alikuwa mstari wa mbele sana kwamba chombo cha kupambana na rushwa kiingie katika Katiba ya nchi na tumekubaliana kwamba tutakapopitisha Katiba Inayopendekezwa basi mimi na yeye *inshallah* Mungu atujalie turudi humu tushiriki kuitengeneza hiyo sheria na kuzingatia mapendekezo aliyoyatoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami niulize swali la nyongeza. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba Serikali imefanya juu chini kuondoa rushwa, imetumia mbinu zote zile mpaka zimekwisha na rushwa bado ipo. Sasa kwa kuwa tumeona kwamba mbinu zote ambazo Serikali imetumia zimeshindikana, hazikuweza kusaidia lolote, kwa nini sasa Serikali isiamue kuomba msaada kutoka nchi zingine ambazo zimefaulu kuondoa rushwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nihitilafiane naye, rushwa iko katika nchi zote duniani si Tanzania peke yake lakini si kweli kwamba jitihada hizi zote tunazozifanya hazijazaa matunda. Ni kwa sababu ya muda tu katika majibu yangu ya nyongeza niliyokuwa nimeandaa sikusema yote, nitamuomba baadaye Mheshimiwa Leticia Nyerere tuonane, nimueleze mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupambana na rushwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kupungua kwa kiwango cha rushwa nchini mwaka hadi mwaka, hii ni kazi imefanywa na *Transparency International*; kukua kwa uchumi wa nchi, hakuna mahali uchumi unaweza kukua kama rushwa imekithiri, hauwezi ukapata *direct foreign investment* kama nchi imeshamiri kwa rushwa; kuboreka kwa utoaji wa huduma kwa wananchi lakini lingine ambalo tumepata mafanikio makubwa ni kwamba Watanzania wengi leo wanaelewa haki zao na ndiyo maana wanashirikiana sana na TAKUKURU katika kuwafichua watu wanaodai na kutoa rushwa.

Mwisho kabisa nataka kusema moja ya mafanikio chombo chetu TAKUKURU imepata wanafuatilia wakiona mahali pana wizi wanaingilia kati kuzuia wizi ule. Nafurahi kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha miaka mitano 2010/2011 mpaka 2014/2015, TAKUKURU imeokoa kiasi cha shilingi bilioni 12.6 katika kufuatilia fedha ambazo zilikuwa zinakusudiwa kuibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni baadhi ya mafanikio ambayo tumeyapata na mimi nataka niseme kwamba sisi Tanzania ni Taifa huru, Taifa linalojitegemea, Taifa lenye watu makini hatuhitaji mtu kuja kutufundisha namna ya kupambana na rushwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Kabati.

Na. 325

### **Kuimarisha Idara ya Ukaguzi wa Elimu Nchini**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Ukaguzi wa Shule katika Halmashauri zetu umeshindwa kufanyika kwa tija kutokana na Wakaguzi hao kukabiliana na uhaba mkubwa wa rasilimali watu na fedha za kufanyia kazi hiyo ya ukaguzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha Idara ya Ukaguzi wa Elimu ili kuboresha elimu nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo na Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MEM) na Sekondari (MES) yameleta changamoto za ufanisi wa ukaguzi wa shule ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya rasilimali watu na vitendea kazi. Mfano katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Ukaguzi wa Shule ilikuwa na idadi ya wakaguzi 1,109 na upungufu wa wakaguzi wa shule 804. Ili kubaliana na changamoto hizo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya rasilimali watu ambapo mwaka 2014/2015 ilifanikiwa kupata walimu wakaguzi 192 na kufanya jumla ya wakaguzi kuwa 1,263 ukiondoa waliofariki, waliostaafu na waliopangiwa kazi nyingine. Aidha, walimu 309 walioteuliwa kujiunga na ukaguzi wa shule wanasubiri taratibu za uhamisho. Walimu wakaguzi hawa watafanya idadi ya wakaguzi kuwa 1,572 ambapo upungufu utakuwa ni 341 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kushirikiana na mradi wa *Global Partnership for Education* itapatiwa magari 45 ambayo yatakabidhiwa Idara ya Ukaguzi wa shule na kusambazwa katika wilaya zisizokuwa na magari. Aidha, Wizara imeongeza tengeo la bajeti ya matumizi mengineyo kwa ajili ya mafuta na vilainishi kutoka Sh.384,731,000 mwaka 2014 hadi kufikia Sh.784,300,000.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu mchakato wa kuanzisha wakala wa Serikali kwa ajili ya kudhibiti elimu nchini. Napenda Serikali iweke wazi, ni lini hasa chombo hiki kitaanzishwa? Sababu naamini ndiyo suluhisho la ufanisi wa Idara ya Ukaguzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kutokana na miundombinu migumu sana iliyopo katika mkoa wetu wa Iringa, Waratibu Kata wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu sana na Serikali ilikuwa imeahidi kuwapatia pikipiki. Je, ni lini sasa Serikali itawapatia pikipiki hizo ili waweze kuboresha elimu yetu katika nchi yote? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kuhusu Wakala wa Ukaguzi, naomba nikiri kwamba, hili suala Wizara yangu imeanza kulitua kwa kumwandikia Waziri Mkuu barua ambapo naye Waziri Mkuu alitambia kwamba tuangalie hali halisi ya Idara ya Ukaguzi kwa sasa ili tuweze kumpa picha kamili ili aweze kutoa maamuzi kamili kuhusu suala hili. Kwa hiyo, ni suala ambalo tunalishughulikia na naomba nimuarifu Mheshimiwa Kabati kwamba suala hili ni muda tu lakini ni suala ambalo ndiyo litakuwa na utatuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu pikipiki za Waratibu wa Elimu Kata, ambapo ni kweli hili suala ni la msingi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua ugawaji wa pikipiki kwa Waratibu wa Elimu Kata wa Taifa zima. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba suala hili tunalishughulikia kwa karibu sana na tuko kwenye hatua za mwisho za kuhakikisha kwamba Waratibu wa Elimu Kata wanapata pikipiki mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kujali suala ambalo litaleta manufaa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa sababu kubwa ambazo zinafanya Wakaguzi wa Shule za Msingi na Sekondari kushindwa kutekeleza wajibu wao ni usafiri. Kwa kuwa hata wilaya zile ambazo Idara ya Ukaguzi ina gari, hawana hata fedha za kufanya service na wilaya nyingine hazina gari kabisa. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuhakikisha kila Idara ya Ukaguzi kwa wilaya zote zinakuwa na magari na kutengewa fedha kwa ajili ya kufanya service na kuweka mafuta magari hayo ili kutekeleza wajibu wao ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, nakiri kwamba tatizo la usafiri limekuwa ni kikwazo kikubwa kwenye ukaguzi. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba Serikali imepata magari 45 ambayo tutayapeleka kwenye zile wilaya ambazo hazina magari kabisa. Pia bajeti yetu kwa kipindi hiki cha mwaka 2015/2016, upande wa fedha za mafuta ambazo zitapelekwa kwa halmashauri zote, imepanda zaidi ya mara dufu na upande wa service, fedha hizohizo zitatumika kwenye halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyohiyo, Mheshimiwa Anastazia Wambura.

Na. 326

### **Idadi Wasichana Wanaojunga na Elimu ya Juu Nchini**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini idadi ya wasichana wanaojunga na vyuo/elimu ya juu katika nchi yetu inashuka kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na wanaojunga na shule za sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Anastazia Wambura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa idadi ya wanafunzi wa kike wanaodahiliwa katika taasisi za elimu ya juu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka 2008/2009 walidahiliwa wanafunzi wa kike 31,012, kwa 2009/2010 wanafunzi 42,239, mwaka 2010/2011 wanafunzi 51,860, mwaka 2011/2012 wanafunzi 60,592 na mwaka 2012/2013 wanafunzi 74,498. Vilevile katika mwaka 2013/2014 walidahiliwa wanafunzi wa kike 77,524 na mwaka 2014/2015 wanafunzi 78,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya ongezeko katika udahili wa wanafunzi wa kike katika taasisi za elimu ya juu, kwa kiasi kikubwa yalitokana na Serikali kuweka juhudi za makusudi ili kupandisha uwiano wa wanafunzi wa kike vyuoni, hadi ifikie asilimia 50 kwa 50. Juhudi hizi ni pamoja na kuhamasisha jamii kuwekeza katika elimu ya mtoto wa kike, kuimarisha huduma za unasihi shuleni, kuendesha programu za stadi za maisha shuleni na kujenga mabweni na hosteli za wasichana katika shule za sekondari.



Aidha, Serikali kupitia taasisi za elimu ya juu, imekuwa ikitoa mafunzo kabilishi (*pre-entry programmes*) kwa wanafunzi wa kike ili kuwawezesha kupata sifa kwa ajili ya kujiunga na programu husika katika vyuo hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na pia naipongeza sana Serikali kwa jitihada ambazo inafanya kuongeza idadi ya wasichana katika vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala hili linajidhihirisha vizuri kabisa katika kuongezeka kwa uwiano wa kijinsia kupanda ambapo mwaka 2006 ilikuwa asilimia 22 na mwaka 2012 ikawa imeongezeka hadi asilimia 30. Hata hivyo, ukilinganisha na shule za sekondari, uwiano huu bado ni mdogo kwa sababu shule za sekondari utaona ni asilimia 105. Kwa hiyo, bado asilimia 30 ni ndogo sana. Ukiangalia upande wa Zanzibar, uwiano huu tayari umeshavuka asilimia 50 kwa 50. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu tofauti hizi za uwiano wa Zanzibar na Tanzania Bara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kuhusiana na mikopo, wasichana wengi wanalalamika kutopata hii mikopo ya kujiunga na elimu ya juu. Serikali inasema nini kuhusu kutoa mikopo kwa kuzingatia uwiano wa jinsia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ambalo amezungumzia uwiano wa wasichana na wavulana kwenda elimu ya juu iwe ni 50 kwa 50 haswa akifananisha na upande wa Tanzania Zanzibar, naomba nikiri kwamba upande wa Zanzibar wamefika karibu 50 kwa 50 ukilinganisha kati ya watoto wa kike na watoto wa kiume. Sisi upande wa Bara, ni kweli nikiri kwamba hatuendi hivyo lakini sababu za msingi ziko hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni uchache wa watu wa Zanzibar. Upande wa Bara tatizo letu kubwa na Wizara tunakiri ni kwamba watoto wa kike wanaojiunga na kidato cha tano wanakuwa si asilimia kubwa sawa na wavulana. Tumegundua *high school* za watoto wa kike ni chache ukilinganisha na zile za watoto wa kiume. Pia zile *high school* za watoto wa kike ni *boarding school* na wakati huohuo shule nyingi za *day* hazina *high school*. Ukiangalia upande wa Zanzibar, wenzetu shule zao nyingi ni za *day* na ni *high school* na zinachukua watoto wote wa kike na wa kiume sababu inayofanya na wale wasichana waliofaulu waweze kuendelea na masomo na kuleta tofauti na huku Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ambalo linahusu mikopo, ukweli tunatoa asilimia 100 kwa wale watoto tu ambao wamechagua kuingia kwenye masomo ya sayansi. Naomba nichukue nafasi hii kupongeza taasisi kama ya WAMA ambayo imechukua nafasi kubwa sana ya kusomesha kwa upendeleo watoto wa kike.

Katika hili, nichukue nafasi hii kumpongeza mama Salma Kikwete, kwa jinsi ambavyo ametusaidia Serikali kujali watoto wa kike na kuwapa nafasi ya kipendeleo katika masomo, pamoja na TEA ambayo ni taasisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambayo inafanya hivyo hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ana dharura, tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mtangi.

Na. 327

### **Wafanyakazi Wanaolipa Kodi kwa Mfumo wa "PAYE"**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Katika Sheria ya Mapato (*Income Tax Act (Cap. 332)*), viwango vya kodi ya pato la jumla ya shilingi 3,500,000/= kwa mwaka ni shilingi 175,200/= ambapo 'lipa kadri unavyopata' (*PAYE*) kwa shilingi 3,500,000 kwa mwezi ni shilingi 957,700/= sawa na shilingi 11,492,400 kwa mwaka:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba wafanyakazi wanaolipa kodi kwa mfumo wa "PAYE" wanalipa kodi kubwa sana na hivyo kudhoofisha uwezo kimaisha?

(b) Je, Serikali haioni ipo haja ya kurekebisha kodi hiyo kwa punguzo kubwa zaidi ya pendekezo la asilimia moja (1%)?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA(MHE. ADAM K. MALIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kwa ujumla wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kupunguza kodi ya ajira hadi kufikia tarakimu moja. Hata hivyo, kutokana na ukweli kuwa kupunguza kodi hii kwa mara moja, kutapelekea kupungua kwa kiasi kikubwa cha mapato kuliko bajeti ya Serikali inavyoweza kuhimili kwa wakati mmoja, Serikali imeandaa mpango wa kupunguza kodi hii kwa awamu.

Uchambuzi wetu unaonyesha kuwa punguzo la *PAYE (Pay As You Earn)*, kwa asilimia moja tu hupunguza mapato kwa shilingi bilioni 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi kwenye mapato ya ajira ni dhahiri, tumekuwa tunafanya hivyo, kipindi hadi kipindi. Kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali imepunguza kiwango cha chini cha kodi hii kutoka asilimia 18.5 hadi asilimia 12 katika mwaka wa fedha 2014/2015. Mwaka huu wa fedha pia Serikali imepunguza kodi hiyo hadi kufikia asilimia moja yaani punguzo la asilimia moja kutoka asilimia 12 iliyotozwa mwaka jana 2014/2015.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mntangi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tafsiri ya swali haikuwa imeeleweka vizuri lakini tusonge mbele, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna *Finance Act* ya 2015 ambayo inakuja na katika *Finance Act* hiyo kuna pia marekebisho ya sheria hii inayoitwa Sheria ya *Income Tax*. Je, kutakuwa na uwiano wowote wa mabadiliko kati ya sheria hizi mbili, *Pay As You Earn* na sheria hii ya pili ambayo nimeizungumzia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilimwandikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba mwanzoni mwa mwaka huu, pale Muheza kumetokea migongano kati ya *TRA* na wafanyabiashara ambapo *TRA* wamekuwa wakiwadai wafanyabiashara ongezeko la kodi mara 100 zaidi ya kiwango kilichokuwepo, jibu hadi leo sijapata.

Je, si wakati mzuri sasa Mheshimiwa Waziri akatoa jibu ili watu wa Muheza na *TRA* waweze kufahamu ukweli halisi wa mabadiliko kama yapo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA(MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzo hili la asilimia moja, kwa sababu tumelipitisha humu ndani, ameuliza kama *Finance Act* na sheria zingine za masuala ya kodi kutakuwa na uwiano, lazima kutakuwa na uwiano. Punguzo hili lazima liwe *reflected* kwenye sheria zingine zote husika kama ni utaratibu wa sheria zote za *Income Tax*. Kwa hiyo, hili majibu yake ni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la *TRA* na wafanyabiashara wa Muheza, haya malalamiko yamekuwa yakipatikana maeneo mbalimbali lakini naomba niseme, utaratibu ni uleule kwamba, mara nyingi malalamiko haya yanatokana pale ambapo wafanyabiashara na maafisa wa *TRA*

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

wanapokutana na kufanya makisio kwa sababu *record keeping* hakuna. Sasa pale kwenye kukosekana *record keeping* pale ama kwenye mashine za EFD ama kwa utaratibu wa *receipts* za kawaida, ndiyo pale tunapoingia kwenye mgogoro kama huu. Hakuna namna nyingine ya kufanya, kweli ni mgogoro mara nyingine wanazidishiwa *estimates* wakati mwingine wanapunguziwa kulingana na ninyi wenyewe mtakavyoelewana pale. Ili kuondoa tatizo hili, ndiyo maana Serikali inahimiza sana wafanyabiashara katika ngazi zote, wa chini, wa juu, wa kati, wawe na *record keeping* inayoeleweka ili ikifika kukutana na Afisa wa Kodi kusiwe tena na longolongo ya kubishana isipokuwa unamkabidhi takwimu zako, unamkabidhi kumbukumbu zako za biashara ili afanye makisio ya kodi kulingana na *record keeping*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mdogo na tuna Muswada mwingine unafuata. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Macheqli, kwa niaba yake Mheshimiwa Ngonyani.

Na. 328

**Umeme wa REA - Ukerewe**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI (K.n.y. MHE. SALVATORY N. MACHEMLI**  
aliuliza:-

Serikali iliahidi kupeleka umeme kwenye vijiji kumi na nne (14) katika Wilaya ya Ukerewe kupitia REA. Je, mchakato wa mradi huo umefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI(MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Macheqli, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imeanza kutekeleza ahadi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Busungumungu, Kakululu, Murutirima, Muriti Sekondari, Ihebo, Ihebo Musoma, Bukanda, Igara Sekondari, *Rubya Forest Office*, Busanda, Buye, Hamkoko, Lugongo, Mubongo Sekondoari, Munbuga Sekondari, Mgoma Muluseni, Busiri na Bilungo kwenye Wilaya ya Ukerewe kupitia Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili na mkandarasi anayetokeleza mradi huo ni *CHICO-CCC (BJ) JV LIMITED* ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivi inahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33, urefu wa kilomita 19; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4, urefu wa kilomita 31; ufungaji wa mashine umba au transfoma 18 na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 687. Gharama ya kazi hizi ni shilingi bilioni 1.93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi umekamilika kwa asilimia 29 ambapo mkandarasi amemaliza kazi ya kusafisha eneo la kupitisha njia ya umeme na anatarajia kuanza kazi ya kuchimba mashimo na kusimika nguzo. Sababu za kuchelewa kukamilika kwa mradi huu ni kuchelewa kupatikana vifaa vya kusambaza umeme hasa vile vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi ikiwemo nguzo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya ngongeza. Kwanza nimpungeze kwa juhudi zake na jinsi alivyozunguka katika vijiji na wilaya mbalimbali. Nataka kuuliza, je, haya mambo ambayo ameyafanya katika mikoa mingine ni lini atakuja Tanga kuona madhara ya REA na wamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri alimpigia simu Meneja wa TANESCO Korogwe, akamuomba amtotee takwimu ya vijiji vya Kurasi, Pemba pamoja na Mwanahauya ili wapelekewe umeme mwezi huu wa saba. Je, ni lini umeme huo utafika katika vijiji hivyo vilivyo katika kata ya Magoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI(MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamjibu Mheshimiwa Profesa, nitoe taarifa ndogo kwa watu wa Ukerewe na watu wa Ukerewe ndiyo tatizo la kuchagua watu wanaokimbia *game*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, napenda kutoa taarifa kwamba, kisiwa cha Ukara, kitafungiwa *solar min grid* zenye uwezo wa juu kabisa wa *megawatt* moja. Kisiwa cha Ilugwa, kisiwa cha Kamasi, kisiwa cha Bwiro, kisiwa cha Kakukulu na kisiwa cha Ghana, zitafungwa *solar min grid* ndogondogo kuvisaidia visiwa vinavyozunguka Ukerewe. Imebidi niliseme kwa sababu Mbunge wao amekimbia *game*.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini nitakwenda Tanga, Tanga nitakwenda na sitakwenda Tanga na kurudi, nitakwenda Tanga na nimeshamweleza Mheshimiwa Nassir, Mheshimiwa Kitandula na shemeji yangu pale. Niwaombe Wabunge wa Tanga, wakandarasi wangu wameshamaliza kazi, *connectivity* inachelewa. Mpige ngoma, mpige matarumbeta watu wafunge umeme, watu wetu wako *slow* kwenye kufunga umeme. Nimewaambia, kama *wiring* ni tatizo, watumie kifaa kinaitwa Simbachawene. Kuna kifaa kinaitwa Simbachawene kinauzwa Sh. 30,000/=, ukilipa TANESCO Sh.27,000/=, ukafunga Simbachawene, unafunga kwa Sh.63,000/= umemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Meneja wa TANESCO wa Korogwe; Meneja wa TANESCO wa Korogwe, saa tano nitakuwa ofisini, unipigie simu unieleze tatizo la huyo Mbunge, kama tatizo ni guzo zipelekwe.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Moshi Vijijini, Kata ya Kahe Mashariki kuna Kijiji cha Uria ambacho kina vitongoji vinaitwa Kwajima, Mwisho wa Shamba na Reli B.

Naomba kuulizia ni lini Serikali itapeleka umeme wa REA katika vitongoji hivi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu mama mkwe, Mheshimiwa Betty, kama ifuatavyo:-

Kwa wabunge wote, kijiji chochote unachokifikiria kwamba kinahitaji umeme, ukaripoti TANESCO. Utaratibu wa boshi wangu wa kazi, mahitaji yote ya umeme yanapelekwa TANESCO Wilaya na wale vijana wako *mobile* wapigie watakuja, tumewapa magari 132. TANESCO Wilaya wanakwenda Mkoa, Mkoa wanakwenda Taifa, TANESCO Taifa ndiyo wanapeleka kwenda REA, ndiyo utaratibu. Usilete maombi kwangu, peleka kwa Mameneja wako.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Jimbo la Tunduru Kusini ambalo lina takribani vijiji vinavyofikia 70, vilishapimwa vijiji vyote kwa ajili ya umeme wa REA, lakini kwaAwamu hii ya Pili tumepata vijiji vinne tu.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waziri unawaambia nini Wananchi wa Tunduru Kusini juu ya Awamu ya Tatu ya REA; wajenge matumaini gani kwa Serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kama ifuatavyo:-

Mimi nina masilahi makubwa sana na Tunduru, Meneja wenu wa *District* nimempeleka Marekani akapate uzoefu wa kuunga umeme wa kwenye vijiji. Kwa hiyo, Awamu ya Tatu ni miongoni mwa Mameneja ambao tumewapatia kipaumbele cha kwenda kuongeza ujuzi waende kwa kasi. Tunduru, Songea yote, *access rate* iko chini, ni pamoja na Katavi, Rukwa na Kagera. Makusudi mazima tunataka kupeleka *access rate* iende juu, ndiyo maana Meneja wenu amepelekwa Marekani. (*Makofi*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mradi wa REA katika Mkoa wa Rukwa ulikuwa ukamilike mwezi Juni 2015. Cha ajabu hakuna kandarasi yoyote *site* katika Mkoa wa Rukwa hasa *line* ya kutoka Kirando kwenda Namanyere, Kipili na kutoka Kasu kwenda Swaila, kuna nguzo tu zimesimama, leo ni miezi mitatu hakuna mkandarasi.

Lini wakandarasi watarudi kwenye *site*?

**MWENYEKITI:** Waziri majibu, lini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu rafiki yangu Mheshimiwa Keissy, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Suala la Nkasi nalo ni maeneo yenye matatizo. Ninapenda nizungumze atakayenilaumu shauri yake; maeneo yote ambayo hayana wakandarasi Watanzania yamekuwa na utendaji mbovu. Niwapongeze makandarasi wa Kitanzania, wanafanya vizuri kwenye Mradi wa REA II. Ukiwa-*rank* wanaofanya vizuri *Urban* anafanya vizuri, Sengerema anafanya vizuri, DEMO anafanya vizuri, NAMS anafanya vizuri, OKAY anafanya vizuri; ni Waswahili. Hawa wageni wamepata matatizo katika kuweza *kui-manage* sehemu ya Tanzania.

Mheshimiwa Keissy, hilo suala lisipotekelezwa ni mimi nitakuwa nimekuangusha, ninalisimamia, nitahakikisha nasimamia Nkasi, nina masilahi na Nkasi Mzee Keissy na wewe unajua.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Nami nataka kumwuliza Naibu Waziri kwamba, mwezi uliopita Mheshimiwa Waziri alikuja Mtwara na kufanya mkutano wa hadhara pale mjini na kuahidi kwamba maeneo yote ambayo hakuna umeme mpaka ifikapo Julai 2015 umeme utakuwa umewaka; na kwa kuwa mpaka sasa hivi ninapoongea hakuna dalili ya aina yoyote na ukizingatia umeme huu utakaowaka maeneo yote gesi hiyo inatoka Mtwara. Tunataka kumsikia Mheshimiwa Waziri anatusaidiaje ili tuweze kupata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Murji, kama ifuatavyo:-

Unajua mimi ni Naibu Waziri, sasa anaposemwa Waziri wangu ninakuwa mwangalifu kwenye kujibu. Siyo kwamba hakijafanyika kitu Mzee Murji, kaulizie siyo kwamba hakijafanyika kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muwajenge moyo Watendaji wetu. Vijana wapo wanafanya kazi, inawezekana hawajatosheleza lakini wanafanya kazi. TANESCO wanafanya kazi, REA wanafanya kazi, Wakandarasi nimetoka kuwasifia sasa hivi wanafanya kazi. Mzee Murji, niko tayari niache jimbo langu nikatetee Watendaji wangu. Watendaji wangu mimi ni muhimu, sifa ninazopata na anazopata Waziri wangu ni kwa sababu ya Watendaji. *(Makofi)*

Mzee Murji, Mwenyezi Mungu atusaidie na Ramadhani hii, Vijana wanafanya kazi. Watu wa REA wapo wanatafuta pesa za ziada kwa ajili ya Mtwara Vijijini, Mtwara Mjini na Mikoa yote ya Lindi na Mtwara. Ninachowaomba, hawa Vijana mkiwakatisha tamaa, sisi Mawaziri siyo chochote. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba uniruhusu niipongeze sana Serikali hasa, TANESCO pamoja na REA, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kututoa kwenye asilimia kumi mpaka asilimia thelathini na sita ya umeme vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nimpongeze sana Mheshimiwa Kinana, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, kwa kwenda eneo moja ambalo tangu Uhuru, Kisiwa cha Ilugwa kilichoko Ukerewe.

Kama ulivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, umeme umeombwa, swali langu; kwa sababu huyu CHICO, umewasifia sana wakandarasi wa ndani wazalendo; huyu kandarasi CHICO amechukua maeneo mengi kweli kweli



lakini utendaji wake ni wa kusuasua. Mheshimiwa Waziri, nataka kupata maelezo, tatizo hasa la huyu CHICO hasa kwenye Jimbo langu la Sumve na mimi ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, lakini kazi haiendi kule Jimbo la Sumve; tatizo hasa ni nini Mheshimiwa Waziri? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Ndassa, Mbunge wa Sumve, ambaye yeye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo muumini wa kwamba, mfinyanzi hulia gaeni, wala siyo muumini wa kwamba seremala akalie gogo badala ya kukalia *furniture*. Hili suala la CHICO nitalisimamia mwenyewe. Nimeshamwambia Mchina yule, lazima kwa Mwenyekiti umeme uwake, mambo ya mfinyanzi hulia gaeni ni ya zamani. Atakayenilaumu anisamehe bure. Hata ukiamka asubuhi unanawa uso, uso wa Wizara ya Nishati na Madini ni Mwenyekiti wake, amefanya kazi nzuri, amefuatilia pesa, amejenga hoja ya kuongeza tozo, kwa hiyo itafanyiwa.

Kijiji cha Kilugwa alichokwenda Katibu Mkuu wa Chama, napeleka *solar mini-grid* kisiwani, visiwa vyote vitawaka. Hizi siyo porojo, tumshafunga *units* 500 katika Mkoa wa Kigoma, *solar mini-grid* 500 zimefungwa na zingine zinakuja. Visiwa vyote vya Ziwa Victoria mambo mazuri yanakuja. Maisha bora wanasema ni mchakato siyo tukio na maisha bora yameanza kuonekana. (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Kandege!

Na. 329

### **Usambazaji wa Umeme – Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Wilaya Mpya ya Kalambo hususan Makao Makuu ya Wilaya Matai Kata ya Kasunga, Kasimba, Mwazye na Mwimbi?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kutumia chanzo kipya cha Maporomoko ya Kalambo katika kuzalisha umeme utakaotumika WILAYA nzima ya Kalambo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imenza kupeleka umeme katika Wilaya Mpya ya Kalambo hususan Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo, Matai Mjini na Vitongoji vyake. Utekelezaji wa Mradi katika Wilaya ya Kalambo unahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolt 33, urefu wa kilometa 180. Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolt 0.4 urefu wa kilometa 95, usungaji wa mashineumba (*transformer*) 39 na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 10,820, gharama za Mradi ni bilioni 2.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme Matai Mjini imekamilika kwa asilimia 100 na wateja wa awali 234 wameunganishwa. Mradi wa kupeleka umeme katika Kata za Kasumba, Kasunga na Mwimbi unatekelezwa na Mkandarasi aitwaye Nakuloi Investment. Kazi imekamilika kwa asilimia 84 ambapo ujenzi wa laini kubwa na ndogo za umeme umekamilika kwa asilimia 100 na hivi sasa mkandarasi anaendelea na taratibu za kufunga *transformer* ili aweze kuwaunganishia umeme wateja zaidi.

Mradi wa kupeleka umeme katika Kata ya Mwanzye unatekelezwa na mkandarasi aitwaye Sinotec ambapo Mradi umekamilika kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ipo haja ya kuwa na vyanzo vingine vya kuzalisha umeme wa bei nafuu. Wizara ya Nishati na Madini ina mpango wa kuangalia uwezekano wa kuzalisha umeme katika chanzo cha Maporomoko ya Kalambo. Maporomoko ya Kalambo yapo mpakani mwa nchi ya Tanzania na Zambia. Zambia imetenga eneo la maporomoko haya kwa shughuli za kitalii zaidi, ambapo watu wengi hufika kutembelea. Kabla ya kufanya upembuzi yakinifu kujua kama eneo hili linafaa kutumika katika kuzalisha umeme, Serikali yetu inazungumza na Serikali ya Zambia ili kufanikisha uzalishaji wa umeme.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, kwanza na mimi naomba niungane na wenzangu kuwapongeza hasa wakandarasi wa kizalendo, wamefanya kazi nzuri sana. Kwangu mimi Kalambo kuna mzalendo mmoja anaitwa Nakuloi Investment, amefanya kazi nzuri sana, anahitaji kusaidiwa na Serikali, angekuwa ameshamaliza kazi sasa hivi kama kontena moja lingekuwa limeshakwamuliwa.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Pamoja na kuipongeza Serikali nina maswali mawili kwa Wizara. Ni ukweli usiofichika kwamba, Wilaya ya Kalambo na Jimbo la Kalambo ilikuwa na zero *electrified*. Katika vijiji 112 kwa REA Awamu ya Pili ni vijiji 17 tu ndivyo vinavyokwenda kunufaika na umeme huu. Ili tufikie azma ya kupata umeme kwa asilimia 53 ni wazi kwamba, Wilaya ya Kalambo inahitaji kutazamwa kwa jicho la pekee.

(i) Kwa kuwa kwenye ziara ya Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM alivisoma vijiji ambavyo vinatakiwa kupata umeme kwa awamu hii ya pili na katika wanufaika katika vijiji 17 vilivyotajwa vijiji hivyo havipo. Je, Serikali iko tayari kuhakikisha vile vijiji ambavyo vimetajwa na tukaenda kuwafanyia mikutano Wananchi wanapata umeme katika Awamu hii ya Pili?

(ii) Kwa kuwa Wizara inajua kabisa tumeongeza tozo ili kuhakikisha umeme unaenda kwenye vijiji vingi nchini Tanzania. Je, Serikali iko tayari kutoa orodha mpya kwa vijiji vipya vitakavyopata umeme Kalambo ili na sisi tufanane na Wilaya zingine?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Josephat Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephat katika swali nililojibu, nilieleza mikoa ambayo nimeelekezwa na mkuu wangu wa kazi niisimamie. Rukwa, Katavi, Kigoma, Ruvuma ni miongoni mwa mikoa ambayo ninapaswa kuiangalia kwa karibu. Sababu gani tunaiangalia kwa karibu, tunatumia kipimo cha *access rate*, wangapi wanaweza kuamka usiku wakauona umeme, wangapi wanaweza kutembea kilometa moja wakauona umeme, ndicho kipimo. Kwenu hali ni mbaya, nayo iko chini yangu.

Naogopa Mzee Arfi asiingie hapa, nina majukumu nimepewa ya kuongeza *megawatt* moja kule Mpanda, yote ni majukumu yangu.

Mheshimiwa Josephat, mimi nawasiliana na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi moja kwa moja, Katibu Msaidizi wake Edward ananipigia simu kunipa maelekezo na mimi ninajipenda.

Kwa hiyo, suala hili litatekelezwa kwa *formula* ile ile kuanzia *District Manager*, unakwenda *Regional Manager*, unakwenda Makao Makuu. Tumekubaliana kwamba, huu ndiyo utaratibu mwafaka, kwa hiyom ninyi ni kipaumbele.

REA Namba Tatu Rukwa nyie, Katavi nyie, Songea, Ruvuma na Kigoma ndiyo kipaumbele.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Nianze tu kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wa REA, TANESCO na Wizara ya Nishati, kwa jinsi ambavyo wanafanya juhudi kubwa za kuleta umeme katika nchi yetu.

Swali langu ni kwamba; Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali ameeleza juu ya hatua za dharura za kupeleka umeme katika Mkoa wa Mtwara na Lindi, *underlying project*.

Nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri ni lini hiyo *project* itaanza kwa kuwa Wananchi wangu wa vijiji mbalimbali wa kata zangu ikiwemo Milunda, Namombwe pamoja na Mchauru, wote hao wanahitaji kupata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili ni swali langu la nyongeza la mwisho katika Bunge la Kumi, ambalo limefanya kazi vizuri sana ya kupeleka umeme. Wakati ninajiandaa kurudi tena kwenye Bunge la Kumi na Moja, naomba nimjibu kwa niaba ya Waziri wangu, Mheshimiwa Bwanausi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Bwanausi, nalazimika kukwambia yale ambayo sikutaka kuyasema. Swali hilo linaulizwa na kila Mbunge wa Lindi na kila Mbunge wa Mtwara, sasa naamua kusema msije mkaniona mimi ni mbaya wenu. Serikali ilishaamua bilioni arobaini na nane zitengwe kwa ajili ya ku-*electrify* Mtwara na Lindi. Kwamba, tunapoanza kusukuma gesi mwezi wa tisa, watu hawa wajue manufaa ya gesi. Wakiambiwa gesi huwasha umeme, basi wauone umeme unawaka kwao. Ilishaamuliwa na tajiri yangu, unajua Simbachawene ni bosi wangu, sasa kuna tajiri yangu, anayejua anajua. Ilishaamuliwa siku nyingi, kilichokuwa kinakwamisha ni michakato. Ili mtu apewe kuna *tender*, baada ya *tender* kuna vikao vinakaa, baada ya hapo pesa ni ndefu bilioni arobaini na nane, lazima barua hizo *award* ziende kwa AG. Makaratasi yote yanafanyika, AG akishasaini makandarasi wapo watapewa kazi, hapo Waziri kwa AG hahusiki.

Niwaambie Watu wa Mtwara na Lindi, haiwekezekani gesi ikatoka kabla hamjaona nguzo na waya na kila kitu kinamwagwa kule. Nami nitahakikisha kauli ya mkuu wangu wa kazi Mheshimiwa Simbachawene ya kuwasha vijiji 100, nasimama *site* kule kuhakikisha kazi inafanyika. Watu wa Tanzania mtulie, nawaambia maisha bora yameshafika siyo kesho ni leo. (*Makofi*)

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais mwaka wa jana akiambatana na aliyekuwa Waziri wa Nishati wakati huo Profesa Muhongo, vilisomwa vijiji 80 vya Mbinga vitawekewa umeme na mpaka sasa bado na vilisomwa vijiji vya Mikaranga, Kambarage, Matiri na Luanda, lakini hakuna nguzo wala chochote. Nini kinatokea Wilaya ya Mbinga kuhusu Miradi ya REA?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, jibu kwa kifupi muda umeisha.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Kayombo tusipoteze muda, mimi niko kwenye Viwanja vya Bunge, tukitoka nje tukae hapo tumpigie *District Manager* aniambie tatizo ni nini tunasuluhisha.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwa kuwa watu wa Itilima na zaidi sehemu ya Bumela mpaka Nanga na pia kutoka Mwamapalala mpaka Gambasingu wanaona nguzo tu. Waziri unasema nini katika kumsukuma huyu mkandarasi aliyepo Itilima amalize kazi yake kabla kama ulivyosema hatujamaliza awamu yetu ya Bunge la Kumi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cheyo, ambaye aliunga mkono bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mimi Charles John Paul Mwijage, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, nakuagiza Engineer Msofe, uende Itilima, Mela na Mapalala, uhakikishe umeme unafungwa na ninataka taarifa kesho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Chilolo!

Na. 330

### **Serikali Huwawezesha Wakunga wa Jadi**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Wakunga wa Jadi wana uwezo sawa wa kutibu au kuwasaidia akina mama wenye matatizo ya uzazi au wagumba lakini hutoa huduma hizo katika mazingira magumu na vifaa duni:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fungu la kuwawezesha wakunga hawa wa jadi ili waendeleo kuwasaidia wanawake wenye matatizo kwenye mazingira mazuri na vifaa vya kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya akina mama na watoto wachanga katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma kwa utoshelezi bado kuna changamoto zake.

Kulingana na takwimu za mwaka 2013, inaonyesha kwamba, akina mama wapatao 432 hufariki kwa kila vizazihai 100,000. Lengo ni kupunguza vifo hivi hadi kufikia vifo 193 kwa kila vizazihai 100,000.

Katika juhudi za kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya wanawake wajawazito, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mwaka 2008 iliandaa Mpango Mkakati ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkakati katika mpango huo ni pamoja na:-

Kuimarisha mifumo ya huduma za afya; kuwa na watoa huduma waliopata mafunzo, yaani *skilled attendants*; uwepo wa vifaa na vifaa tiba muda wote na hasa vifaa vinavyotumika wakati wa dharura; dawa muhimu na vitendea kazi; pia kuwajengea uwezo watoa huduma ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za dharura kwa wanawake wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusisha jamii katika kupanga na kutekeleza mipango inayohusu masuala ya afya. Aidha, mkakati huo unahusu kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma kwa kusaidiwa na wahudumu waliosomea, ambao tafiti zimedhihirisha kwamba, wakitumika ipasavyo hupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakunga wa jadi ni kiungo kikubwa katika utoaji wa huduma za ukunga wa jadi tangu miaka mingi iliyopita. Wakunga wa jadi wamekuwa wanatoa huduma kwa jamii, ikiwa ni pamoja na wanawake wenye matatizo ya uzazi. Pamoja na kwamba huduma hizi zimekuwa zikitolewa, lakini siyo kwa kiwango kinachostahili. Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inashirikiana na wakunga wa jadi kama watu muhimu katika jamii.

Katika kutambua wanawake wajawazito wenye vidokezo vya hatari na kuwashauri kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara imekamilisha mwongozo wa huduma ya mama na mtoto katika jamii. Matumaini yangu ni kwamba, wakunga wa jadi kama watu muhimu katika jamii, watashiriki kikamilifu kuhakikisha afya ya mama na mtoto inaimarika na hatimaye kufikia lengo la Maendeleo ya Milenia Namba Tano ifikapo Desemba 2015.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chilolo!

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali imetambua juhudi ambazo zinatolewa na wakunga wa jadi kwa ajili ya akina mama wajawazito na wenye matatizo ya uzazi; na kwa kuwa Serikali imekiri kwamba katika zahanati zetu na vituo vya afya bado kuna upungufu wa wauguzi. Kwa kuwa Serikali imeanza kutoa elimu kwa wakunga wa jadi itakuwa tayari sasa kuwapatia chumba kwenye zahanati zetu au kwenye vituo vya afya ili waendeleo kutoa huduma hiyo nzuri katika mazingira safi na salama?

(ii) Kwa kuwa Sera yetu ya Afya Vijijini haijaainisha wakunga wa jadi kupewa angalau posho kwa kazi nzuri wanayofanya; na kwa kuwa tuna Mfuko wa Bima ambao unatumika kwa kila zahanati na kila kituo cha afya na hospitali zote. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote nchi nzima kuanza kuchukua pesa kidogo kwenye Mfuko wa Bima ili kuwapa posho hawa wakunga wa jadi ambao wanafanya kazi nzuri za kuwasaidia akina mama wajawazito na wenye matatizo ya uzazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa kwamba kuwe na chumba maalum katika zahanati kwa ajili ya wakunga wa jadi haiendani na utaratibu wa utoaji wa huduma.

Katika utafiti ambao umefanyika kwa Dunia nzima chini ya Shirika la Afya Ulimwengu (*WHO*), umeonyesha kwamba, wakati mwingine wakunga wa jadi wanafanya kazi kubwa na nzuri, lakini wanachangia kuongezeka kwa vifo vya akina mama kutokana na uzazi kwa sababu ya kucheleweshwa katika maeneo husika.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoshauri na ndiyo maelekezo na msimamo wa Serikali katika Sera, wakunga wa jadi washirikishwe na kuelimishwa hasa kupunguza maambukizi pale ambapo uzazi unakuwa ni wa dharura katika eneo husika. Wasiwacheleweshe akina mama ambao ni wajawazito. Mara nyingi imejitokeza uzazi pingamizi, akina mama hawa wanapocheleweshwa kwa wakunga wa jadi, hutokea vifo kwa akina mama au kwa mama na mtoto.

Namshukuru Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa kufuatilia suala hili la kupunguza vifo vya akina mama kutokana na uzazi.

Swali la pili kuhusu kuwepo kwa posho ya wakunga hao wa jadi, hili lipo kwenye utaratibu kama ifuatavyo:-

Pale ambapo wameshiriki katika huduma ya MUCOBA wakiwemo wahudumu wa afya vijijini, wakishirikishwa katika mfumo huo, tunatoa maelekezo na kukumbusha maeneo yote husika wapatiwe posho. Hawapo katika mfumo rasmi wa ajira kwa hiyo hatuwezi kuwapangia kupata posho. Kwa utaratibu huu mzuri ambao nchi tunafahamu, tunao upungufu mkubwa wa watumishi, wanashirikishwa kwa njia hiyo. Wahudumu wa afya wa vijiji pamoja na wakunga wa jadi katika mfumo huo wanatambulika na wanaweza kupewa posho kwa sababu wako katika maeneo. Vilevile huwa wanashirikishwa katika huduma ya MUCOBA, yaani *outrich services*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina!

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza swali moja Mheshimiwa Waziri.

Kwa suala la ugumba lipo *fifty-fifty* wanawake na wanaume lakini akina baba huwa hamkubali kama ninyi mnatokezea kuwa wagumba.

Je, ni kwa nini Serikali isifungue *infertility clinic* ya wagumba wanawake na wanaume iweze kuwahudumia yenye vifaa kamili vya kisasa kabla akina mama hawajajiona wanyonge wakakimbilia kwa wakunga wa jadi kwenda kutafuta tiba zisizokuwa na uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!



**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWII WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Amina Clement, kama ifuatavyo:-

Suala zima la Serikali kuanzisha *clinic* hizi za ugumba, yaani *infertility clinic*, ni suala ambalo limejumuishwa katika huduma ya kuhudumia afya ya uzazi na mtoto wakiwemo akina mama walio katika umri wa kuzaa. Kwa hiyo, suala la *infertility clinic*, yaani kliniki za ugumba zinajumuishwa katika huduma hii kwa ujumla, isipokuwa kwa wazo lake hili zuri kulingana na taaluma inavyozidi kupanuka, kliniki hizi maalum zinaweza kuanzishwa, lakini huduma hizi zinalenga wote akina baba na akina mama.

Ninatoa rai kwa Watanzania wote, akina baba wakati mwingine suala zima la mfumo dume kunyoosha kidole kwa mama mgumba kuwa tangu wafunge ndoa hawajapata mtoto miaka 10, suala hilo kitaalamu linahusu pande zote mbili. Sababu za kutopata mtoto katika familia inaweza kuchangiwa na baba au mama, kwa hiyo, suala hili la kimaumbile lipo pande zote mbili. Kwa hiyo, nawaasa akina baba kuwa ni vizuri kutoa ushirikiano kwa mama ili mtoto apatikane. Taaluma hii imeanza kuongezeka ikiwemo *in vivo training* ambayo wataalamu wetu wanafanya kwa ajili ya kupandikiza mbegu katika yai la mama na akapata mtoto.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo; Mheshimiwa Bukwimba!

Na. 331

### **Serikali Kutoa Ruzuku kwa Wakulima Wote**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Mpango wa KILIMO KWANZA unatoa ruzuku ya pembejeo za kilimo na kuwanufaisha Wakulima wachache na Wananchi watanufaika zaidi pindi mgawanyo wa pembejeo utakapokuwa unatolewa kwa vijiji vyote na kwa Wananchi wote.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwa Wakulima wote wa Jimbo la Busanda?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto ya uzalishaji na tija katika kilimo, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa Wakulima kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa pembejeo na kujenga utamaduni wa matumizi endelevu ya pembejeo za kilimo miongoni mwa Wakulima nchini na hivyo kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa Wakulima umeweka vigezo mbalimbali kwa wanufaika ikiwemo uwezo wa kuchangia gharama za pembejeo husika kwa lengo la kuwajengea Wakulima uwezo na mazoea ya kujinunulia pembejeo wenyewe. Aidha, utaratibu huo umezingatia ukweli kuwa, mpango wa kutoa ruzuku siyo endelevu na Serikali haina uwezo wa kibajeti wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa Wakulima wote nchini wakiwemo wa Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua juhudi za Wakulima wa Jimbo la Busanda na Mkoa wa Geita katika uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo nchini. Kwa kutambua juhudi za Wakulima, Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya pembejeo kwa Wakulima wa Mkoa wa Geita na Jimbo la Busanda, ambapo kati ya mwaka 2010/11 hadi 2013/14, jumla ya Vocha 300,888 zenye thamani ya Sh. 7,658,770,000 zimenufaisha kaya 100,296 kupitia pembejeo za ruzuku ya mbegu bora za mahindi na mpunga pamoja na mbolea ya kupandia na kukuzia. Aidha, mpango huo umesaidia kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo hususan mazao ya chakula nchini na hivyo Taifa kujitosheleza kwa chakula.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bukwimba!

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu ya Serikali, natambua kabisa kwamba zaidi ya 80% ya Watanzania wanategemea kilimo na bila ya kuwa na pembejeo hasa za mbolea, maana yake hatujaweza kumsaidia huyu Mtanzania.

- (i) Napenda kujua kwa nini Serikali isianzishe Mfuko Maalum wa Pembejeo wa kuwasaidia Wakulima kama ambavyo imeanzisha katika Wizara mbalimbali kama Wizara ya Ujenzi kuna Mfuko Maalum wa Barabara na Wizara nyingine?

(ii) Nchi yetu iko katika soko huria ambapo ununuzi wa bidhaa mbalimbali unafanyika na watu mbalimbali. Katika Wilaya ya Geita ununuzi wa pamba unafanyika na kampuni moja tu, yaani kampuni ndiyo inaenda kununua pamba katika eneo moja, jambo ambalo Wananchi hawajakubaliana nalo, kwa sababu bei ya pamba inakuwa chini kwa sababu mnunuzi ni mmoja tu.

Napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kulifuatilia suala hili ili Wananchi wanufaike zaidi kutokana na Kilimo cha Pamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ipo haja kubwa sana ya kuhakikisha tunakuwa na pembejeo za kutosha ili Wananchi wengi zaidi wazitumie kwa ajili ya kuleta tija zaidi katika uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho Serikali inakifanya sasa ni kuhakikisha tunaanzisha viwanda vya kuzalisha kwa kushirikiana na sekta binafsi na ndiyo sababu sasa tuna kiwanda cha kuzalisha mbolea ya Minjingu kule Arusha ambacho kimsingi kimekuwa kikiboresha mbolea zake mwaka hadi mwaka na kwa kweli zimeanza kuleta matumaini mazuri kwa Watanzania.

Tunajua sote kwamba, kuvumbuliwa kwa gesi Mtwara wapo watu au makampuni ambayo yameonyesha nia ya kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya mbolea. Tumaini la Serikali ni kwamba, viwanda vingi vikijengwa, hizi mbolea ambazo kwa sasa zinazwa kwa bei kubwa kidogo, bei zake zitashuka na Watanzania wengi zaidi wataweza kunufaika. Kwa hiyo, Watanzania wachache kama kaya 1,000,000 ambao wanapata mbolea kupitia utaratibu wa ruzuku ya Serikali, wengi zaidi wanaweza kupata mbolea ikiwa tu viwanda hivyo vitajengwa.

Suala la kuanzisha Mfuko wa Pembejeo ni suala la Wabunge, kama Wabunge wataielekeza Serikali na kuitaka Serikali hivyo na ikaonekana iko nia ya dhati kama ambavyo tumefanya kwenye sekta nyingine, sisi Wizara ya Kilimo tutalikaribisha sana wazo hilo.

Swali la pili kwamba, ipo kampuni moja ya kununua pamba. Wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri alitoa kauli hapa kwamba, si nia ya Serikali kuona kampuni moja inanunua pamba katika eneo moja na kwa bei wanayopanga wao

wenyewe. Kwa kauli hii napenda sasa nimwagize Mkurugenzi Mkuu wa Pamba na kwa sababu Mheshimiwa Waziri alishatoa maelekezo, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba aende Geita, akaone kitu kinachoendelea na wachukue hatua mara moja kukomesha hali hiyo ya Wafanyabiashara kuwanyonya Wakulima wetu na hususan katika Zao hilo la Pamba kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani, kisha ajiandae Mheshimiwa Likokola!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Chai ni Zao la Biashara. Wakulima wa Tarafa ya Bungu wamelima chai kwa muda mrefu na ndiyo kipato chao kikubwa katika maisha yao. Ghafila wawekezaji au wenye viwanda wameamua kupunguza bei kutoka kwenye Sh. 226 mpaka Sh. 176. Wakulima wameacha kuchuma chai na chai imekuwa kama miti.

Je, Serikali itawasaidiaje Wananchi ambao ndiyo zao ambalo lilikuwa linawasaidia kuwasomesha vijana wao na mambo mengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niseme kwamba, Serikali inachukizwa sana na Wafanyabiashara ambao lengo lao kubwa limekuwa ni kuwanyonya Wakulima wetu. Kwa namna ambavyo Mbunge amekuwa anawapigania Wakulima wake wa Jimbo la Korogwe Vijijini, nachukua nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Chai na nina hakika wanafuatilia na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, suala hili lifuatiliwe mara moja na ikiwezekana wenzangu wa Bodi ya Chai waende Korogwe Vijijini mara moja kufuatilia hali hiyo na ninaomba mpaka kesho wawe wamenipa majibu niweze kumpatia Mheshimiwa Mbunge kabla hajaondoka hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Devotha!

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali dogo la nyongeza.

(i) Kwa nini Serikali haioanishi mipango yake ya kutoa pembejeo na kuboresha masoko ya mazao kwa wakulima; hii inasababisha Wakulima wa Mikoa ya Ruvuma, Rukwa na kadhalika kuwa na pembejeo nyingi na kuongeza uzalishaji lakini kukosa masoko ya mazao?

(ii) Je, Serikali iko tayari safari hii kufanya mipango ambayo inakuwa endelevu ili mazao na pembejeo vitolewe kwa pamoja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Devotha M. Likokola, Mbunge wa Viti Maalum Ruvuma, kama ifuatavyo:-

Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na ninataka nimfahamishe kwamba, Serikali ilishaliona hilo na tulishaanza kuchukua hatua hizo na ndiyo sababu tuna mpango wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ambao tumeanza kuufanyia kazi na katika baadhi ya maeneo huo mpango umeanza kufanya kazi. Vilevile ili kupanua soko kwa uhakika zaidi, ule utaratibu wa *Commodity Exchange* nao pia tunauimarisha kwa kasi kubwa sana.

Jambo lingine ni kujenga maghala mengi sana ambayo Wananchi wakulima watakuwa wanatunza mazao yao wakati tunasubiri bei ziwe nzuri zaidi. Tayari tumeshapata msaada wa zaidi ya *Euro* milioni 50 au zaidi ya *Shilingi* za Tanzania bilioni moja kwa ajili ya kujenga maghala ambayo yatatuwezesha kuhakikisha tunatunza mazao ya wakulima wakati tukisubiri bei zikiwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tumekuwa pia tunatafuta masoko katika nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (*SADC*), lakini pia katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika nchi za Ulaya na Mashariki ya Mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika hili la masoko imejipanga vizuri sana kuhakikisha uzalishaji huu unaendana pia na upatikanaji wa soko kwa masoko ya mazao ya wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malocha!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nina swali moja la nyongeza.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Suala la utoaji wa pembejeo ya ruzuku kwa uzoefu karibu kila mwaka linachelewa sana na hivyo kusababisha Wananchi kutowahi msimu kadiri ilivyopangwa.

Je, Serikali imejipangaje kwa mwaka huu kuhakikisha inawahisha pembejeo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimiwa Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kumekuwa na ucheleweshaji wa pembejeo kwa wakulima karibu kila msimu. Naomba nikiri jambo hilo, lakini naomba pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kwa kipindi cha mwaka huu imejipanga vizuri. Ninaomba niwahakikishie kwamba, sasa hivi tayari utaratibu wa Vocha kuchapishwa unaendelea na tuna hakika tumeagiza Wizarani Vocha zitufikie mwishoni mwa mwezi Agosti, inapofika mwezi Septemba hizi Vocha zianze kusambazwa kwa Wakulima. Kwa kuwa Serikali itakuwepo pamoja na kwamba tunaenda kwenye uchaguzi, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba, mwaka huu tutalisimamia vizuri zoezi la vocha ili zifike mapema zaidi kwa Wakulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, sasa ni kipindi cha kuwatambulisha wageni ndani ya Bunge.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Mbunge wa Jimbo la Siha, anaomba kuwatangazia Wachungaji sita kutoka kwenye Jimbo lake, ambao ni Jeremiah Kileo, Elibariki Maimu, Paulo Mmari, William Mollel, Joshua Laizer na Paniel Kweka; karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambaye ni Ndugu Ngeke Nzigula Ole Mganga, mfugaji kutoka Chalinze Pwani; karibu. *(Makofi)*

Wageni kumi wa Mheshimiwa Grace Puja, ambao ni Wanakijiji wa Tarafa ya Ihanja wakiongozwa na Ndugu Eliudi Bakari; karibuni Dodoma. *(Makofi)*

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Wageni wa Mheshimiwa Said Arfi, ambao ni Ndugu Joseph Mona - Katibu wa Mkoa wa ACT, Ndugu Crisphian Salvia - Katibu wa Jimbo ACT Mpanda Vijijini na Ndugu Pius Maswila - Mwenyekiti Ngome Wazee ACT Makasi. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Godbless Blandes kutoka Jimboni kwake. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Paul Lwanji kutoka Jimboni kwake; karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni Viongozi 17 wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Taifa, wakiongozwa na Ndugu Gracian Mukoba - Rais wa CWT Taifa.

Maafisa wanne kutoka Taasisi ya Mikopo iitwayo Yetu Microfinance, ambao ni Ndugu George Ndugu, Alex Miliga, Happy Sembega na Altemius Milinga; karibuni Dodoma.

Ndugu John Bura Chuwa, Mkazi wa Kijiji cha Barazani, Kata ya Mahangwi, Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara, karibu. *(Makofi)*

Ndugu Amina Shaibu na Ndugu Mwanahamis Juma, wapo kwa ajili ya kutembelea Bunge. *(Makofi)*

Kaimu Katibu wa Bunge, Mama Kippa, anaomba niwatangazie Wajumbe wote waliochukua mikopo ya matrekta na vifaa vingine vya kilimo kutoka SUMA JKT, waende Chumba Namba 227 kuna maelekezo muhimu ambayo wanatakiwa kuyapata. Waheshimiwa Wabunge, ukumbi umebadilishwa sasa mnatakiwa mwende Ukumbi wa Pius Msekwa.

Katibu, hatua inayofuata!

### **MWONGOZO WA MWENYEKITI**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ukweli kwamba, shughuli za Bunge huenda zikafungwa kesho na kwa kuzingatia minong'ono inayozunguka katika duru mbalimbali za siasa za hapa Bungeni, ni kwa nini usituongoze kwa kuitisha kikao cha pamoja cha Kamati ya Uongozi mimi nikiwa Mjumbe wake

pamoja na Kamisheni ya Bunge tuweze kujadili minong'ono hii ambayo inazunguka kwenye duru mbalimbali hapa kuliko kuja kupata aibu yoyote ile hapo kesho? Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, nimekuelewa na nikuhakikishie tunalifanyia kazi na kabla ya saa saba nitakupa majibu. *(Makofi)*

Katibu, hatua inayofuata!

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Tume ya Walimu wa Mwaka 2015 (The Teachers Service Commission Bill, 2015)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Muswada huo utawasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kwa heshima ya Kiti chako nitaomba sasa umwite kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kuwasilisha Muswada huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa niaba ya Waziri Mkuu. Tiatia ubani bwana mambo ndiyo yanavyoanza hivyo hivyo. *(Kicheko)*

#### **WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (K.n.y. WAZIRI MKUU):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu wa Mwaka 2015 pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya Uenyekiti mahiri wa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, kwa kuujadili Muswada huu kwa kina na kutoa ushauri. Aidha, katika kipindi chote cha majadiliano Kamati ilitoa michango kadhaa kwa Serikali kuhusu namna bora ya kusimamia Utumishi wa Walimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kipekee, namshukuru Mheshimiwa George Masaju - Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Bwana Casmir Kiuki - Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake, kwa kushirikiana na Wataalam wa Ofisi yake na Wataalam wengine kutoka Ofisi ya Rais,



## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Tume ya Utumishi wa Umma Idara ya Utumishi wa Walimu au TSD.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu ni kutungwa kwa Sheria ambayo itasimamia masuala ya Utumishi wa Walimu pamoja na kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu. Baadhi ya masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na yafuatayo:-

Moja, uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu, kazi za Tume pamoja na Wajumbe wa Tume.

Mbili, uanzishwaji wa Sekretarieti ambayo itakuwa inafanya kazi ambazo itapewa na Tume.

Tatu, uanzishwaji wa Kamati mbalimbali zitakazokuwa katika Mikoa na Wilaya pamoja na kutoa majukumu ambayo Kamati hizo zitatakiwa kufanya.

Nne, kuanzishwa kwa utaratibu wa kuwatambua na kuwasajili Walimu waliopo katika Utumishi wa Umma.

Tano, kutoa adhabu kwa Walimu wote ambao watakuwa wanashindwa kutekeleza maamuzi ambayo Tume itakuwa imeyatoa.

Sita, kutoa mamlaka kwa Waziri kutengeneza kanuni ambazo zitamsaidia katika utekelezaji wa kazi za Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tano.

Sehemu ya Kwanza yenye ibara ya kwanza, pili na tatu, inahusu mambo ya utangulizi ambapo inaelezea Jina la Sheria, sehemu ambayo sheria itatumika katika Jamhuri ya Muungano na tasfiri au ufafanuzi wa maneno mbalimbali yaliyotumiwa katika sheria. Katika kifungu cha tatu cha Muswada, Serikali imefanya marekebisho kwenye tafsiri za maneno kama ifuatavyo:-

Kifungu cha tatu kimerekebishwa kwa kurekebisha maana ya neno "Waziri" ili lisomeke "Waziri maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa" na kufuta tafsiri ya neno "mwajiri" kwa kuwa neno hilo halijatumika mahali popote katika Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada ina ibara ya 4 hadi ya 18. Ibara ya 4 ya Muswada inaanzisha Tume ambayo itajulikana kama Tume ya Utumishi wa Walimu itakayokuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ibara ya 5 ya Muswada inaelezea kazi ya Tume ya Utumishi wa Walimu ambazo ni pamoja na kuajiri, kupandisha madaraja na kushughulikia nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, kumshauri Waziri kuhusu masuala ya kiutawala, usimamizi na utumishi wa Walimu na ufanyaji wa tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya Walimu na uwekaji wa rejista itakayotunza orodha ya majina ya Walimu wote waliopo katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya sita inahusu Muundo wa Tume. Katika ibara hii Serikali imefanya marekebisho katika kifungu cha 6(b) cha Muswada kwa kuongeza uwakilishi wa Chama cha Walimu na Bodi ya Kitaalam ya Walimu pamoja na Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa msingi huo, kifungu cha 6(b) kinafutwa na badala yake kitasomeka kama ifuatavyo:-

(b)“Wajumbe wengine kumi ambao watateuliwa na Waziri kama ifuatavyo: Moja, Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma; mbili, Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; tatu, Mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana ya elimu; nne, Mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana na Serikali za Mitaa; tano, Mwakilishi kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi; sita, Wawakilishi wawili kutoka Bodi ya Kitaalam ya Walimu; Saba, Wawakilishi wawili kutoka Chama cha Walimu na nane Kamishna wa Bajeti au Mwakilishi wake.

Ibara ya 7 inahusu uanzishaji wa Kamati za Tume ya Utumishi ya Walimu, kwa lengo la kutekeleza shughuli mbalimbali za Tume kama zitakavyoelekeza.

Ibara ya 8 inaelezea uteuzi wa Katibu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais.

Ibara ya 9 inahusu kiapo kwa Mwenyekiti na Katibu wa Tume kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

Ibara ya 10 na 11 zinaelezea ajira za Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Taifa na katika ngazi ya Wilaya. Aidha, ibara ya 11 Waziri amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni zitakazotoa utaratibu wa ufanyaji kazi wa Tume.

Ibara ya 12 inahusu kazi na majukumu ya Tume katika ngazi ya Wilaya ikiwemo masuala ya nidhamu, kutunza orodha ya Walimu, orodha ya tange (*seniority list*). Aidha, imetoa mamlaka kwa Mkuu wa Shule kushughulikia makosa madogo madogo ya kinidhamu ambayo hayatasababisha Mwalimu kufukuzwa kazi, kushushwa daraja au kupunguziwa mshahara.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ibara ya 13 inahusu masuala ya rufaa kwa Mwalimu ambaye atakuwa hajaridhika kwa maamuzi yaliyotolewa dhidi yake katika ngazi mbalimbali.

Ibara ya 14 ya Muswada imeweka masharti kuhusu masuala ya usimamizi wa utawala wa Walimu chini ya mamlaka ya Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Katika ibara hii Serikali imefanya marekebisho kwa lengo la kuonyesha uhusiano kati ya Tume na Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 14(1) kwa kuondoa maneno “welfare” na kifungu kidogo cha (2) kwa kuondoa maneno “Wizara yenye dhamana ya elimu” na kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno “Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa” na badala yake kuweka “Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.”

Ibara ya 15 inaweka masharti kuhusu posho na malipo mengine ambayo Wajumbe wa Tume wanaweza kulipwa kutoka katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi hayo na Bunge na kama itakavyoainishwa na Waziri mwenye dhamana ya sheria hii.

Ibara ya 16 inatoa jukumu kwa Tume kuandaa na kuwasilisha taarifa kuhusu shughuli na utendaji wake katika mwaka husika.

Ibara ya 17 inaweka katazo la kutoa taarifa za Tume kwa watu ambao hawakuidhinishwa kupata taarifa hadi ridhaa ya Waziri iwe imetolewa kwa maandishi kuruhusu kutolewa kwa taarifa hizo kwa amri ya kisheria. Aidha, imeweka zuio la watu wasiohusika na utoaji taarifa za Tume.

Ibara ya 18 inaainisha kuwa ni kosa kwa mtu yeyote kushawishi Tume kufanya maamuzi na mtu atakayepatikana na kosa la kushawishi Tume atapewa adhabu kwa mujibu wa Muswada huu.

Sehemu ya Tatu ya Muswada huu ina ibara za 19 hadi ya 22. Sehemu hii inapendekeza masharti yanayohusiana na masuala ya fedha na vyanzo vyake. Katika ibara ya 19 inapendekezwa kuwa, mapato ya fedha ya Tume ya Walimu yatakuwa ni yaleyale yaliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yake na mapato mengine yanaweza kupatikana kwa njia ya misaada au mikopo toka ndani ama nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hii ibara za 20 hadi 22 zinapendekeza namna ambavyo kila mwaka wa fedha, Tume itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana, taarifa ya matumizi, makadirio ya mapato, taarifa za ukaguzi wa mapato na matumizi na taarifa hizo kuwasilishwa Bungeni. Serikali imefanya marekebisho kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) cha ibara ya 21 na kufuta ibara nzima ya 22 ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya Muswada huu inaadinisha namna Waziri mwenye dhamana kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi wa Walimu, atakavyotengeneza kanuni zitakazoweka utaratibu wa jinsi ya kutekeleza sheria hii. Aidha, Serikali imefanya marekebisho kwenye kifungu cha 23 cha Muswada kwa kuingiza aya mpya ambayo itakuwa ni (c) na kurekebisha aya ya (c) na (d) kuwa aya (d) na (e). Kifungu cha 23(c) sasa kitasomeka kama ifuatavyo:-

*“Kuelezea namna na utaratibu ambao ustawi wa Walimu ikiwemo ulipaji mishahara, posho na pensheni yatakavyoshughulikiwa ama kwa Kiingereza; prescribing the manner and procedure by which welfare of teachers including payment of salaries, allowances and pension, shall be administered.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano na ya mwisho ya Muswada huu inapendekeza vifungu vya Sheria ya Utumishi wa Umma (Sura 298), ambavyo vitafutwa ili kuondoa masuala ambayo yameondolewa au yatashughulikiwa na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge, waujadili Muswada huu na hatimaye wakubali kuupitisha ili uwe sehemu ya sheria za nchi yetu kwa manufaa ya Sekta ya Elimu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Walimu wa Mwaka 2015  
(The Teachers Service Commission Bill, 2015)  
Kama Ulivyowasilishwa Mezani**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**BILL SUPPLEMENT**

No. 3

20<sup>th</sup> February, 2015

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.8 Vol. 96 dated 20<sup>th</sup> February, 2015  
Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

THE TEACHERS' SERVICE COMMISSION ACT, 2015

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section Title*

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title and commencement
2. Application
3. Interpretation

PART II

TEACHERS SERVICE COMMISSION

4. Establishment of the Commission
5. Functions of the Commission
6. Composition of the Commission
7. Committees of the Commission
8. Appointment of Secretary
9. Oath
10. Staff of the Commission
11. District offices
12. Functions of the Commission at the district level
13. Appeals
14. Supervision and administration of welfare of teachers
15. Remuneration of members
16. Activity report
17. Prohibition of unauthorized disclosure of information
18. Offence of attempt to influence the Commission

PART III

FINANCIAL PROVISIONS

19. Resources of the Commission
20. Estimates of the revenue and expenditure
21. Audit
22. Annual report

PART IV

MISCELLANEOUS PROVISIONS

23. Regulations
24. Transitional provision

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**PART V  
CONSEQUENTIAL AMENDMENT**

25. Amendment of the Public Service Act.

**NOTICE**

-----

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,  
3<sup>rd</sup> February, 2015

**OMBENI Y. SEFUE**  
*Secretary to the Cabinet*

**A Bill**

*for*

**An Act to establish the Teachers Service Commission, to provide for its functions and obligations and to provide for matters related thereto.**

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania.

**PART I  
PRELIMINARY PROVISIONS**

Short title and commencement

**1.** This Act may be cited as the Teachers Service Commission Act, 2015, and shall come into operation on such date as the Minister may, by notice published in the *Gazette*, appoint.

Application

**2.** This Act shall apply to Mainland Tanzania in respect of primary and secondary schools teachers employed in the public service.

Interpretation

**3.** In this Act, unless the context otherwise requires -  
“appointing authority” in relation to teachers, means the Teachers Service Commission;  
“Commission” means the Teachers’ Service Commission established under this Act;  
“committee” means committee of the Commission established under section 7 this Act;  
“disciplinary authority” means any person or authority vested with powers under this Act to take disciplinary measures against a teacher and includes a person to whom those powers have been delegated;

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

“employer” in relation to teachers, means a person or organization in the public service with whom a teacher entered in to a contract of service and who is responsible for the payment of salaries of such teacher;

Cap. 287  
Cap.288

“local government authority” has a meaning ascribed to it by the Local Government (District Authorities) Act and the Local Government (Urban Authorities ) Act;

“member” in relation to the Commission includes the Chairman and other members of the Commission;

“Minister” means the Minister responsible for education;

Cap.298

“public service” has the meaning ascribed to it under the Public Service Act;

“the service” means the teachers Service;

“teachers service” means the unified service of all teachers in the public service;

“teacher” means a person registered as a teacher and who pursued a teaching training course in a registered teachers’ college or university,

### PART II

#### THE TEACHERS SERVICE COMMISSION

Establishment of  
the Commission

4. There is hereby established a commission under the Ministry responsible for education which shall be known as the Teachers’ Service Commission.

Functions of the  
Commission

5. The functions of the Commission shall be to-

- (a) maintain and administer the teachers’ service;
- (b) advise the Minister on administration and maintenance of the teachers service;
- (c) appoint, promote and discipline teachers;
- (d) to ensure equitable deployment and distribution of teachers among and within local governments and schools
- (e) determine appeals from decisions of disciplinary authorities;
- (f) maintain a register and records of all teachers who are in the service;
- (g) supervise teachers in-service training programmes;
- (h) conduct research and evaluation on matters relating to teachers service and advise the Minister accordingly;
- (i) to assess the teacher situation and advise the Minister responsible for teachers training on the number, type and level of teachers needed in the country;
- (j) prescribe code of ethics and conduct of teachers service;
- (k) maintain communication with district offices and on all or any matter relating to the development of teachers service; and
- (l) do any other thing or act, which in the opinion of the Minister, is conducive or incidental to the better carrying out of its functions.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Composition of the Commission

- 6.**-(1) The Commission shall be composed of-
- (a) a Chairman to be appointed by the President;
  - (b) not more than eight other members to be appointed by the Minister from the following:
    - (i) a member from President Office, Public Service Management;
    - (ii) a member from the Ministry responsible for education;
    - (iii) a member from the Ministry responsible for local government authorities;
    - (iv) a member from the National Council for Technical Education;
    - (v) a member from the Teachers Professional body;
    - (vi) a member from the Teachers Trade union;
    - (vii) Commissioner for Budget or his representative; and
    - (viii) a member from the Planning Commission.
- (2) In appointing members of the Commission, the Minister shall ensure that both men and women are appointed on grounds of merit.
- (3) The provisions of the First Schedule to this Act shall have effect as to procedure at meetings, tenure of members and other matters relating to the Commission.

Committees of the Commission

- 7.**-(1) The Commission may, for the purpose of facilitating performance of its functions, form such number of committees to perform specific functions as the Commission may determine.
- (2) The size, terms and conditions of the committees shall be as be determined by the Commission.

Appointment of the Secretary

- 8.**-(1) There shall be a Secretary to the Commission who shall be appointed by the President.
- (2) In appointing the Secretary, the President shall have regard to appoint a person who has demonstrated ability of, and capacity in dealing with teachers' affairs.
- (3) The Secretary shall be the chief executive officer of the Commission and shall be responsible for the co-ordination of functions of the Commission.

Oath

- 9.** The Chairman and the Secretary of the Commission shall on first appointment each take and subscribe to an oath or affirmation in a form set out in the Second Schedule to this Act.

Staff of the Commission

- 10.**-(1) There shall be recruited and employed in the office of the Commission, such number of public officers in such categories and levels as the Commission may, with approval of the Permanent Secretary (Establishment), determine.
- (2) The office of the Commission shall be public office.



## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

District offices

**11.-**(1) There shall be offices of the Commission at district level with such number of staff as may be determined by the Commission.

(2) Each district office shall, subject to direction of the Commission, perform functions of the Commission and report to the Commission on its performance.

(3) The Minister may, on the advice of the Commission, make regulations prescribing procedures for performance of functions of the Commission by the district office.

Functions of the Commission at the district level

**12.-**(1) In performing functions conferred by this Act, each district office shall-

(a) keep and maintain an updated register of all teachers under its jurisdiction who are employed in the public service;

(b) keep and maintain an updated seniority list for all teachers under their jurisdiction;

(c) ensure that teachers appointed in the service fill and sign agreement forms before reporting to their respective stations;

(d) recommend to the Commission for approval of re-appointment of teachers formerly terminated from the service provided that such a teacher shall have been out of service for a period of not less than twelve months from the date of receipt of the letter of termination;

(e) maintain records in open and confidential files and submit service particulars to other districts in the event of the teacher's transfer;

(f) uphold and maintain the code of ethics and conduct for teachers;

(g) exercise disciplinary powers over teachers under its jurisdiction; and

(h) carry out such other functions as may be prescribed or conferred to it by the Commission.

(2) For the purpose of paragraph (g) of subsection (1), disciplinary powers at the school level in respect of offences which does not warrant punishment of dismissal, reduction in rank or reduction in salary, shall be exercised by the head of the school.

Appeals

**13.-**(1) Where a teacher is aggrieved by the decision of the head of school, he may appeal to the Commission at the district level.

(2) Where a teacher is aggrieved by the decision of the Commission at the district level, he may appeal to the Commission.

(3) Appeals against the decision of the Commission shall be referred to the President for determination.

Offence of attempt to influence the Commission

**18.-**(1) Without prejudice to the provisions of any other written law, every person who otherwise than in the cause of duty, directly or indirectly, personally or by any other person influence or attempts to influence in any manner a decision of the Commission, commits an offence and shall be liable on conviction to a fine not exceeding five hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding twelve months or to both.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Supervision and administration of welfare of teachers

**14.**-(1) The supervision and administration of the welfare of primary and secondary school teachers shall be the responsibility of the local government authorities.

(2) In administering the welfare of teachers, the local government authorities and the Ministry responsible for education shall comply with the terms and conditions pertaining to employment and welfare of the teachers as shall from time to time be prescribed by the Commission.

(3) For the purpose of this section, the Commission at the district level shall, from time to time convene consultative meetings with the Director of Local Government to deliberate on the matters pertaining to teachers in the district and advise accordingly.

Remuneration of members

**15.** Members of the Commission shall be paid such allowances and other benefits as may be determined by the Minister.

Activity report

**16.** The Commission shall for each financial year prepare and submit to the Minister a report containing detailed information of its activities and operations.

Prohibition of unauthorized disclosure of information

**17.**-(1) No member, officer of the Commission or any other person shall without the written permission of the Minister, publish or disclose to any unauthorized person or otherwise than in the cause of duty, the contents of any document, communication or information of any kind which has come to his knowledge in the cause of performance of functions under this Act.

(2) Any person who knows of any information which, to his knowledge has been disclosed in contravention of this section and who publishes or communicates such information to any other person for purposes other than proceedings in the court of law that has been commended pursuant to this Act or in the exercise of official functions, commits an offence and on conviction shall be liable to a fine of not less than five hundred thousand shillings or to imprisonment for a term of twelve months or to both .

(3) Nothing in this section shall be construed as prohibiting any person from giving a certificate or testimonial to any applicant or candidate for any office or from supplying any information or assistance at the request of the Commission

Offence of attempt to influence the Commission

**18.**-(1) Without prejudice to the provisions of any other written law, every person who otherwise than in the cause of duty, directly or indirectly, personally or by any other person influence or attempts to influence in any manner a decision of the Commission, commits an offence and shall be liable on conviction to a fine not exceeding five hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding twelve months or to both.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(2) A prosecution in respect of an offence under this section shall not be instituted without consent of the Director of Public Prosecutions.

### PART III FINANCIAL PROVISIONS

Resources of the  
Commission

**19.**-(1) The funds of the Commission shall consist of such moneys appropriated by Parliament for purposes of the Commission.

(2) All funds allocated in terms of subsection (1) shall be-

(a) disbursed directly by the Treasury to the respective district office bank account which shall be opened in accordance with public financial laws; and

Cap.348

(b) administered in accordance with the Public Finance Act.

Estimates of the  
revenue and  
expenditure

**20.** The Commission shall, in respect of each financial year, prepare and submit to the Minister estimates of its revenue and expenditure and the Minister shall examine the same and table before the National Assembly.

Audit

**21.**-(1) Accounts of the Commission shall be audited once in every financial year by the Controller and Auditor-General in accordance with the Public Audit Act.

Act. No.11 of 2008

(2) Upon completion of examination of accounts, the Controller and Auditor-General shall certify the accounts and submit a report to the Commission.

Annual report

**22.** The Commission shall, within six months after the end of each financial year, prepare and submit to the National Assembly through the Minister an annual report in respect of that financial year containing-

(a) a copy of audited accounts of the Commission together with the auditor's report;

(b) a report of the operations of the Commission during that financial year; and

(c) such other information as the Minister may require.

### PART IV MISCELLANEOUS PROVISIONS

Regulations

**23.**-(1) The Minister may, upon consultation with the Commission, make regulations for the better carrying out of the provisions of this Act.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), the Minister shall make regulations-

(a) prescribing procedures for recruitment, appointment and deployment of teachers;

(b) prescribing matters related to teachers development;

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- (c) prescribing procedures for disciplinary matters related to teachers; and
- (d) providing for any matter necessary or ancillary to the furtherance of objectives and purposes of this Act.

Transitional provision

**24.** The Minister may, by order published in the Gazette at any time before expiry of six months from the commencement of this Act, make such transitional and supplementary provisions necessary to give effect to the provisions of this Act in respect of maintaining continuity of the Commission.

**PART V  
CONSEQUENTIAL AMENDMENTS**

Amendments of Public Service Act. Cap. 298

**25.** The Public Service Act is hereby amended, by repealing-

- (a) section 6(4);
- (b) section 15(1) (b);
- (c) sub heading “(a)” appearing immediately after section 29; and
- (d) section 30.

-----  
**FIRST SCHEDULE**  
-----

*(Made under section 6(3))*  
-----

**PROCEDURE AT MEETINGS, TENURE OF MEMBERS AND  
MATTERS RELATING TO THE COMMISSION**

Vice Chairman

**1.** The Commission shall elect one of its members to be the Vice-Chairman and any member elected as a Vice-Chairman shall, subject to his continuing to be a member, hold office of Vice-Chairman for a term to be fixed by the Commission and shall be eligible for re-election after the end of such period.

Tenures of Member

**2.-(1)** Subject to the provisions of subparagraphs (2) and (3), a member may hold office for a period of three years from the date of appointment and shall be eligible for reappointment.

(2) Where a member of the Commission other than the Chairman is for any reason unable to perform duties as a member of the Commission, the Minister may revoke his appointment and appoint another member for the period during which the member is disabled.

(3) A member of the Commission may resign by notice in writing addressed, in the case of the Chairman to the President and in case of any other member to the Minister and as from the date specified in such notice, such member shall cease to be a member of the Commission or if no date is specified from the date of receipt of the letter.

(4) A member who fails to attend three consecutive meetings of the Commission or Committee without reasonable cause shall be deemed to have ceased to be a member of the Commission or Committee, as the case may be.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- Validity of any proceedings                    **3.** Validity of any proceedings of the Commission shall not be affected by any vacancy amongst members thereof or by a defect in the appointment of any member.
- Secretary of the Commission                    **4.** The Secretary to the Commission shall attend all meetings but shall not vote at such meetings.
- Meetings and quorum                    **5.**-(1) The Commission shall meet at least four times per year or in such time and place as the Chairman may appoint.  
(2) The Chairman may at any time convene a special meeting of the Commission and shall-  
(a) call a meeting within twenty one days of receiving a written request in that behalf specifying the reason for the meeting and addressed to him and signed by not less than six members of the Commission;  
(b) call a meeting when so directed by the Minister.  
(3) At any meeting of the Commission not less than two third of the members in office for the time being shall constitute a quorum.
- Invitation of non members                    **6.** The Chairman may invite any person to attend a meeting of the Commission, and any such person may take part in the proceedings of that meeting but shall not be entitled to vote.
- Power of the Chairman and Vice-Chairman                    **7.**-(1) The Chairman shall preside at all meetings of the Commission.  
(2) Where at any meeting the Chairman is absent, the Vice-Chairman shall preside.  
(3) In the absence of both the Chairman and Vice-Chairman at any meeting, members present may, from amongst their number elect a temporary Chairman who shall preside at the meeting.  
(4) The Chairman, Vice-Chairman or temporary Chairman presiding at any meeting, shall have a vote and, in the event of an equality of votes, shall have a casting vote in addition to his deliberative vote.
- Commission to regulate its own procedure                    **8.** Subject to the provisions of this Act, the Commission may regulate its own procedure.

-----  
**SECOND SCHEDULE**  
-----  
*(Made under section 9)*  
-----

*Oath/Affirmation by members*

**I**,..... having been appointed as Chairman/member of the Teachers' Service Commission Secretary, do swear/affirm that I will freely and without fear or favour, affection or ill-will, discharge the functions of Chairman/member of the Commission, and that I will not directly or indirectly reveal any matters relating to such functions to any unauthorized person or otherwise than in the course of duty.

**SO HELP ME GOD**

Sworn/Affirm before me this .....day of.....20....  
Before me .....  
President/Minister

-----  
**OBJECTS AND REASONS**  
-----

This Bill proposes to make provisions for the establishment of the Teachers Service Commission of Mainland Tanzania for the purposes of regulating the teaching service for Public Primary and Secondary Schools in Mainland Tanzania.

The Bill is divided in Five Parts, whereas, Part I provides for Preliminary Provisions, to include the Short Title of the proposed Bill, Application clause and Interpretation.

Part II of the Bill has provisions in relation to the establishment of the proposed Teachers Commission.

This Part begins with Clause 4 which provides for provisions for establishment of the Teachers Service Commission which will be an independent Commission under the Ministry of Education.

Clause 5 of the Bill provides for the functions of the Commission whereas it is provided that the Commission shall maintain and administer the teacher's service. It will also advise the Minister on maintenance, administration of the service and will strive to secure good conditions of service for all teachers as would from time be provided by the service regulations.

Clauses 6 and 7 of the Bill provides for the composition of the Commission. The Clauses provide further that the chairman of the Commission to be appointed by the President and other members and to be appointed by the Minister while the Secretary is to be appointed by the President.

Clauses 8, 9 and 10 provide for appointment of the Secretary of the Commission and oath of members and Clause 10 deals with matters relating to appointment of other staff of the Commission.

Clauses 11, 12 and 13 covers establishment of the Commission's offices at district level and their functions and matters related to appeals from decisions of disciplinary authorities.

Clause 14 provides for matters relating to supervision and administration of welfare of teachers.

Clauses 16 provide for matters about preparation of the activity report dealing generally with its activities and operations during the previous year. Clause 16 provides for communications of the Commission are privileged, that is, it is not to be disclosed to unauthorized persons unless the Minister consents in writing in that behalf, its production or disclosure in any legal proceeding may not be compelled.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Clause 18 provides for an offence of attempt to influence the Commission. It is stated in the proposed provision that any person who attempts to influence any decision of the Commission guilty of an offence and shall be liable on conviction to a fine not exceeding five hundred thousand shillings or to, imprisonment for a term not exceeding two years.

Part III of the Bill contains financial provisions. The provisions provide for resources of the Commission, whereas it is provided in Clauses 19, 20, 21 and 22 that the fund of the Commission will come from funds appropriated by Parliament for the purpose of the Commission. Also in this Part there are provisions with regard to estimates of the revenue and expenditure to be prepared and submitted to the Minister, Audit of the Commission's accounts and Annual Report to be prepared and submitted to the Minister. The Minister will cause the Report submitted to him to be laid before the National Assembly.

The Bill in Part IV makes provision for miscellaneous provisions. In clause 23 and 24 this Part provides for power to make regulations and transitional provisions.

Finally Part V of the Bill has Clauses that deal with consequential amendments of the Public Service Act. Amendments are proposed for repealing of subsection (4) of section 6, subsection (1)(b) of section 15 and the whole of section 30 respectively.

Dar es Salaam,  
2<sup>nd</sup> February, 2015

**SHUKURU J. KAWAMBWA**  
*Minister of Education and  
Vocational Training*

### SHERIA YA TUME YA WALIMU YA MWAKA 2015

#### MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu*                      *Kichwa*

#### SEHEMU YA KWANZA MASHARTI YA AWALI

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika
2. Matumizi
3. Tafsiri

#### SEHEMU YA PILI TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

4. Kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

5. Kazi za Tume
6. Muundo wa Tume
7. Kamati za Tume
8. Uteuzi wa Katibu
9. Watumishi wa Tume
10. Kiapo
11. Uanzishwaji wa Tume katika ngazi za Wilaya
12. Kazi za Tume katika ngazi ya Wilaya
13. Rufaa
14. Usimamizi wa Walimu
15. Malipo ya Wajumbe
16. Taarifa za kazi
17. Katazo kuhusu utoaji wa taarifa za siri
18. Makosa ya kushawishi maamuzi ya Tume

**SEHEMU YA TATU  
MASHARTI YA FEDHA**

19. Vyanzo vya Mapato ya Tume
20. Makadirio ya mapato na matumizi
21. Ukaguzi wa hesabu
22. Taarifa ya Mwaka

**SEHEMU YA NNE  
MASHARTI MBALIMBALI**

23. Kanuni
24. Masharti mpito

**SEHEMU YA TANO  
MAREKEBISHO YATOKANAYO**

25. Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma



## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

### TAARIFA

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni umechapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya taarifa ya jumla kwa umma.

Dar es Salaam,  
3 Februari, 2015

**OMBENI Y. SEFUE**  
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

**Sheria ya kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu, kuainisha kazi na majukumu yake na kuainisha masuala mengine yanayohusiana nayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### SEHEMU YA KWANZA MASHARTI YA AWALI

Jina na tarehe ya  
kuanza  
kutumika

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Tume ya Walimu ya mwaka, 2015 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo, Waziri kwa Tangazo litakalochapishwa kwenye *Gazeti* la Serikali, atateua.

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara kwa walimu wote wa shule za msingi na sekondari walioajiriwa katika utumishi wa umma.

Tafsiri ya  
maneno

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-  
“Tume” maana yake ni Tume ya Utumishi wa Walimu iliyoanzishwa chini ya Sheria hii;  
“kamati” maana yake ni kamati za Tume zilizoanzishwa chini ya kifungu cha 7;

“Mjumbe” kuhusiana na Tume, inajumuisha Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume;

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya elimu;

“mamlaka ya ajira” maana yake ni Tume ya Utumishi wa Walimu;

“mamlaka ya nidhamu” ni mtu au mamlaka iliyopewa mamlaka ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mwalimu na inajumuisha mtu aliyekasimiwa mamlaka hayo;

“mwajiri” maana yake ni mtu au taasisi katika utumishi wa umma ambaye ameingia mkataba wa ajira na mwalimu na ambaye anawajibika kumlipa mwalimu mshahara;

Sura ya 287

“mamlaka ya serikali za mitaa” ina maana kama ilivyofafanuliwa katika sheria ya Serikali ya Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

Sura ya 288

Sura ya 298

“utumishi wa umma” ina maana sawa na ile iliyoelezewa katika Sheria ya Utumishi wa Umma;

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- Sura ya 298 “ofisi ya utumishi wa umma” ina maana sawa na ile iliyoelezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma;
- Sura ya 298 “Utumishi” ina maana ya utumishi wa walimu;  
“utumishi wa walimu” maana yake ni utumishi wa walimu wote katika Utumishi wa Umma;  
“mwalimu” maana yake ni mtu aliyesajiliwa kama mwalimu na ambaye amehitimu mafunzo ya ualimu katika chuo cha ualimu au chuo kikuu kinachotambuliwa.

### SEHEMU YA PILI TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

Kuanzishwa kwa Tume **4.** Inaanzishwa Tume chini ya Wizara yenye dhamana na masuala ya elimu ambayo itajulikana kama Tume ya Utumishi wa Walimu.

- Kazi za Tume **5.** Kazi za Tume zitakuwa ni-
- (a) kuendeleza na kusimamia utumishi wa walimu;
  - (b) kumshauri Waziri juu ya kusimamia na kuendeleza utumishi wa walimu;
  - (c) kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu;
  - (d) kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa walimu ndani ya Serikali za Mitaa na shule;
  - (e) kushughulikia masuala ya rufaa zinazotokana na maamuzi ya mamlaka ya kinidhamu;
  - (f) kutunza daftari na kumbukumbu za walimu wote ambao wako katika utumishi wa walimu;
  - (g) kusimamia programu za mafunzo ya walimu kazini;
  - (h) kufanya utafiti na tathmini kuhusu masuala yanayohusu utumishi wa walimu na kumshauri Waziri inavyostahiki;
  - (i) kutathmini hali ya Walimu na kushauri Wizara yenye dhamana ya masuala ya walimu juu ya mafunzo, idadi na uhitaji wa walimu nchini;
  - (j) kuandaa kanuni za maadili ya utendaji kazi ya mwalimu;
  - (k) kuendeleza mfumo wa mawasiliano na Ofisi za Tume katika ngazi ya Wilaya juu ya mambo yote au jambo lolote kuhusiana na maendeleo ya utumishi wa walimu na kuhakikisha kwamba mwajiri na Ofisi ya Tume ngazi ya Wilaya wanatekeleza kazi zao kwa mujibu wa Sheria hii;
  - (l) kufanya jambo au kitendo chochote ambacho kwa maoni ya Waziri kinafaa au kinategemewa katika utekelezaji bora wa kazi zake;

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Muundo wa  
Tume

**6.-**(1) Tume itaundwa na-

- (a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais; na
- (b) wajumbe wengine wasiopungua nane watakaoteuliwa na Waziri kutoka;
  - (i) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
  - (ii) Wizara yenye dhamana na elimu;
  - (iii) Wizara yenye dhamana na serikali za mitaa;
  - (iv) Baraza la Elimu ya Ufundi;
  - (v) chombo kinachosimamia taaluma ya Walimu;
  - (vi) Chama cha Walimu Tanzania.
  - (vii) Kamishna wa Bajeti au mwakilishi wake; na
  - (viii) Mjumbe kutoka Tume ya Mipango.

(2) Katika kuteua wajumbe wa Tume, Waziri atahakikisha ya kwamba inajumuisha wanaume na wanawake watakaoteuliwa kwa misingi ya sifa.

(3) Masharti yaliyomo katika Jedwali la Kwanza katika Sheria hii yatakuwa na nguvu katika mwenendo na utekelezaji wa Tume.

Kamati za Tume

**7.-**(1) Tume inaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake, kuteua Kamati mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza majukumu mahsusi kama itakavyoona inafaa.

(2) Masharti kuhusu muundo na masharti ya utendaji wa Kamati za Tume yatakuwa kama itakavyoamriwa na Tume.

Uteuzi wa Katibu

**8.-**(1) Kutakuwa na Katibu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Katika uteuzi wa Katibu, pamoja na sifa nyingine Rais ataangalia mtu ambaye ameonyesha uwezo wa kushughulikia masuala ya walimu.

(3) Katibu atakuwa mtendaji mkuu wa Tume na atakuwa na jukumu la kuratibu kazi zote za Tume.

Kiapo

**9.** Mwenyekiti, Katibu na wajumbe wa Tume watatakiwa kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao kila mmoja kula kiapo au kuthibitisha kwa dhati katika Fomu iliyopo katika Jedwali la Pili la Sheria hii.

Watumishi wa  
Tume

**10.-**(1) Tume itaajiri idadi ya watumishi katika ngazi na nyadhifa mbalimbali baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu, Utumishi.

(2) Ofisi za Tume zitakuwa ofisi katika utumishi wa umma.

Ofisi za Tume  
ngazi ya wilaya

**11.-**(1) Kutakuwa na ofisi za Tume katika wilaya zenye idadi ya watumishi kama itakavyoamuliwa na Tume watakaotosheleza majukumu ya Tume katika wilaya husika.

(2) Ofisi za wilaya zitaishauri Tume juu ya mambo yanayoweza kuelekezwa na Tume na kutekeleza kazi nyingine kama zitakavyoainishwa au kuelekezwa na Tume na zitatoa taarifa zake za utekelezaji kwa Tume.

(3) Waziri kwa kushauriana na Tume ataandaa kanuni kwa ajili ya kutoa mwongozo wa utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ngazi ya wilaya.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kazi za Tume  
katika ngazi ya  
Wilaya

**12.-**(1) Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, Ofisi za Tume ngazi ya wilaya-

- (a) zitaweka na kuendeleza daftari la kumbukumbu sahihi za walimu wote katika maeneo yao ambao wameajiriwa katika utumishi wa umma;
- (b) zitaweka na kutunza tange ya walimu wote kwenye maeneo yao;
- (c) itahakikisha kwamba walimu walioajiriwa chini ya Sheria hii na kujaza na kutia saina fomu za makubaliano kabla ya kuripoti katika maeneo yao ya kazi baada ya kuthibitishwa kuwa wanafaa;
- (d) kupendekeza kwa Tume utaratibu wa kupata ridhaa ya kuwarudisha tena katika utumishi wa umma walimu ambao walioachishwa kazi, kwa kuzingatia kwamba walimu hao wamekuwa nje ya utumishi wa umma kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kupokea barua ya kuacha kazi;
- (e) kutunza kumbukumbu katika majalada ya wazi na ya siri na kutuma kumbukumbu za utumishi kwenye wilaya nyingine iwapo mwalimu huyo atakuwa amehamishwa;
- (f) kusimamia na kuendeleza kanuni za maadili ya utumishi wa walimu;
- (g) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya walimu katika maeneo yao; na
- (h) kutekeleza kazi nyingine yoyote kama itavyoelekezwa na Tume.

(2) Kwa madhumuni ya aya ya (g) ya kifungu kidogo cha (1), mamlaka ya nidhamu katika shule kuhusu makosa madogo itakuwa mwalimu mkuu wa shule husika.

Rufaa

**13.-**(1) Pale ambapo mwalimu hakuridhika na uamuzi wa mkuu wa shule anaweza kukata rufaa kwa Tume katika ngazi ya wilaya.

(2) Endapo mwalimu hajaridhika na uamuzi wa Tume katika ngazi ya wilaya atakata rufaa kwa Tume makao makuu.

(3) Rufaa kutokana na uamuzi wa Tume zitawasilishwa kwa Rais kwa uamuzi.

Usimamizi na  
masuala ya  
utawala wa  
waalimu

**14.-**(1) Usimamizi na utawala wa waalimu wa shule za msingi na sekondari litakuwa ni jukumu la mamlaka husika ya serikali za mitaa.

(2) Katika kutekeleza masuala yanayohusu maslahi ya walimu, mamlaka ya serikali za mitaa na wizara yenye dhamana na elimu atazingatia masharti ya ajira na maslahi ya walimu kama itakavyokuwa ikitolewa katika nyakati mbalimbali na Tume.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti kifungu hiki, Tume katika ngazi ya wilaya itakuwa na vikao vya mara kwa mara vya mashauriano na mkurugenzi wa Halmshauri kwa lengo la kujadili masuala yanayohusu walimu katika wilaya husika na kutoa ushauri ipasavyo.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Malipo ya wajumbe

**15.** Wajumbe wa Tume watalipwa posho na stahili nyingine kama itakavyoamuriwa na Waziri.

Utoaji wa Taarifa za kazi za mwaka

**16.**-(1) Tume itaandaa, kila mwaka wa fedha taarifa za utekelezaji wa kazi zake na kuiwasililisha kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu, ikitoa maelezo ya kutosha kwenye taarifa ya mwaka kuhusu utekelezaji ulivyokuwa kwa mwaka fedha uliopita na mwaka wa fedha husika pamoja na gharama za utekelezaji.

(2) Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu baada ya kupokea taarifa hiyo, ataiwasilisha Bungeni.

Katazo la kutoa taarifa za siri

**17.**-(1) Mjumbe yeyote, ofisa yeyote wa Tume au mtu mwingine yeyote hataruhusiwa kuchapisha au kutoa taarifa za Tume au yaliyomo kwenye hati yoyote, mawasiliano au taarifa ambazo zimefikia wakati wa kutekeleza kazi zake na kuzitoa kwa mtu yeyote asiyeruhusiwa iwe ni kwa ajili ya kazi yake au vinginevyo, bila kupata kibali cha maandishi toka kwa Waziri kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Mtu yeyote ambaye amepata taarifa, kwa uelewa wake umepatikana kinyume cha kifungu hiki na kuzitangaza au kuzisambaza au kuzitoa kwa mtu mwingine yeyote kwa madhumuni tofauti na ya uendeshaji wa mashtaka chini ya Sheria hii au katika utekelezaji majukumu yake kikazi, atakuwa ametenda kosa.

Sura 47

(3) Masharti ya kifungu hayatafafiriwa kumzuia mtu kutoa cheti kwa mwombaji kwa ajili ya Ofisi au kutoa taarifa zozote zitakazoombwa na Tume.

Makosa ya kushawishi maamuzi ya Tume

**18.**-(1) Bila kuathiri masharti ya sheria nyingine yoyote, kila mtu ambaye, isipokuwa katika utendaji wake wa kazi, atashawishi au kujaribu kushawishi Tume kwa kuhusika moja kwa moja au kumtumia mtu mwingine kuishawishi Tume kwa makusudi ya kuathiri maamuzi ya Tume, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Mashtaka hayatafunguliwa kwa makosa yatakayofanywa na mtu yeyote kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika kifungu hiki bila ya kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

### **SEHEMU YA TATU MASHARTI YA FEDHA**

Vyanzo vya mapato ya Tume

**19.**-(1) Vyanzo vya mapato ya Tume vitajumuisha fedha zitakazotengwa na Bunge kwa ajili ya Tume.

(2) Fedha zote zitakazotengwa kwa ajili ya Tume katika ngazi ya wilaya-

- (a) zitatumwa kwenye akaunti ya Tume ngazi ya wilaya ambayo itafunguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma; na
- (b) zitasimamiwa na kutumiwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Fedha za Umma.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Malipo ya wajumbe

**15.** Wajumbe wa Tume watalipwa posho na stahili nyingine kama itakavyoamuriwa na Waziri.

Utoaji wa Taarifa za kazi za mwaka

**16.**-(1) Tume itaandaa, kila mwaka wa fedha taarifa za utekelezaji wa kazi zake na kuiwasililisha kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu, ikitoa maelezo ya kutosha kwenye taarifa ya mwaka kuhusu utekelezaji ulivyokuwa kwa mwaka fedha uliopita na mwaka wa fedha husika pamoja na gharama za utekelezaji.

(2) Waziri mwenye dhamana na masuala ya elimu baada ya kupokea taarifa hiyo, ataiwasilisha Bungeni.

Katazo la kutoa taarifa za siri

**17.**-(1) Mjumbe yeyote, ofisa yeyote wa Tume au mtu mwingine yeyote hataruhusiwa kuchapisha au kutoa taarifa za Tume au yaliyomo kwenye hati yoyote, mawasiliano au taarifa ambazo zimefikia wakati wa kutekeleza kazi zake na kuzitoa kwa mtu yeyote asiyeruhusiwa iwe ni kwa ajili ya kazi yake au vinginevyo, bila kupata kibali cha maandishi toka kwa Waziri kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Mtu yeyote ambaye amepata taarifa, kwa uelewa wake umepatikana kinyume cha kifungu hiki na kuzitangaza au kuzisambaza au kuzitoa kwa mtu mwingine yeyote kwa madhumuni tofauti na ya uendeshaji wa mashtaka chini ya Sheria hii au katika utekelezaji majukumu yake kikazi, atakuwa ametenda kosa.

Sura 47

(3) Masharti ya kifungu hayatafafiriwa kumzuia mtu kutoa cheti kwa mwombaji kwa ajili ya Ofisi au kutoa taarifa zozote zitakazoombwa na Tume.

Makosa ya kushawishi maamuzi ya Tume

**18.**-(1) Bila kuathiri masharti ya sheria nyingine yoyote, kila mtu ambaye, isipokuwa katika utendaji wake wa kazi, atashawishi au kujaribu kushawishi Tume kwa kuhusika moja kwa moja au kumtumia mtu mwingine kuishawishi Tume kwa makusudi ya kuathiri maamuzi ya Tume, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Mashtaka hayatafunguliwa kwa makosa yatakayofanywa na mtu yeyote kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika kifungu hiki bila ya kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

### SEHEMU YA TATU MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya mapato ya Tume

**19.**-(1) Vyanzo vya mapato ya Tume vitajumuisha fedha zitakazotengwa na Bunge kwa ajili ya Tume.

(2) Fedha zote zitakazotengwa kwa ajili ya Tume katika ngazi ya wilaya-

- (a) zitatumwa kwenye akaunti ya Tume ngazi ya wilaya ambayo itafunguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma; na
- (b) zitasimamiwa na kutumiwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Fedha za Umma.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Makadirio ya mapato na matumizi

**20.**-(1) Tume katika kila mwaka wa fedha husika, itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri makadirio ya mapato na matumizi yake na Waziri atazipitia na kuziwasilisha mbele ya Bunge.

(2) Katika kuandaa makadirio yake, Tume itazingatia ushauri uliotolewa na Waziri na Waziri mwenye dhamana na fedha.

Ukaguzi wa hesabu Sheria Na.11 ya mwaka 2008

**21.**-(1) Hesabu za fedha za Tume zitakaguliwa mara moja katika kila mwaka wa fedha na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma.

(2) Baada ya kukamilika kwa ukaguzi wa hesabu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataidhinisha hesabu hizo na kuwasilisha taarifa yake kwenye Tume.

Taarifa ya mwaka

**22.** Tume ndani ya miezi sita baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, itatayarisha na kuwasilisha Bungeni kupitia Waziri mwenye dhamana ya elimu, taarifa ya akaunti ya mwaka kwa mwaka husika ambayo itajumuisha-

- (a) nakala iliyokaguliwa ya Tume pamoja na taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo;
- (b) taarifa ya shughuli za Tume katika kipindi cha mwaka husika wa fedha; na
- (c) taarifa nyingine zozote kama zitakavyoweza kutakiwa na Waziri mwenye dhamana na elimu, na Waziri atawasilisha taarifa hiyo kusomwa Bungeni.

### SEHEMU YA NNE MASHARTI MBALIMBALI

Kanuni

**23.**-(1) Waziri baada ya kushauriana na Tume, anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kutengeneza kanuni-

- (a) kuainisha utaratibu wa kuajiri, uteuzi na upangaji wa walimu katika vituo;
- (b) kuainisha masuala yanayohusu maendeleo na madaraja ya walimu;
- (c) kuweka masharti kuhusu masuala ya nidhamu kwa walimu; na
- (d) zinazoainisha jambo lolote katika kuendeleza malengo na madhumuni ya sheria hii.

Masharti yatokanayo

**24.** Kwa amri itakayochapishwa katika *Gazeti* la Serikali, Waziri atatengeneza muda wowote kabla ya muda wa miezi sita kumalizika baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, masharti ya mpito ambayo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SEHEMU YA TANO  
MAREKEBISHO YATOKANAYO**

Marekebisho ya  
Sheria ya  
Utumishi wa  
Umma  
Sura 298

- 25.** Sheria ya Utumishi wa Umma inafanyiwa marekebisho kwa kufuta-
- (a) kifungu cha 6(4);
  - (b) kifungu cha 15(1)(b);
  - (c) kichwa kidogo cha habari “(a)” kinachoonekana mara baada ya kifungu cha 29;
  - (d) kifungu cha 30.

-----  
**JEDWALI LA KWANZA**  
-----

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 6(3))*  
-----

**TARATIBU KATIKA MIKUTANO YA TUME**

Makamu  
Mwenyekiti

**1.** Tume itachagua mmoja kati ya wajumbe wake kama Makamu Mwenyekiti na mjumbe yeyote atakaechaguliwa kama Makamu Mwenyekiti wakati akiendelea kuwa mjumbe, atashikilia kwa muda utakaopangwa na Tume na atastahili nafasi ya Makamu Mwenyekiti kuchaguliwa tena baada ya kumazilizika kwa kipindi hicho.

Muda wa kukaa  
madarakani

**2.-(1)** Kwa kuzingatia masharti yaliyopo katika aya ya (2) na ya (3), mjumbe atashika na nafasi hiyo kwa muda wa miaka mitatu kuanzia muda alioteuliwa na atastahili kuchaguliwa tena.

(2) Endapo Mwanachama wa Tume mbali na Mwenyekiti kwa sababu zozote zile ameshindwa kutimiza majukumu yake kama mjumbe wa Tume, Waziri atabatilisha uteuzi wake na atamchagua mwingine kwa muda ule ambao mjumbe atakuwa ameshindwa.

(3) Mjumbe yeyote wa Tume anaweza kujiuzulu kwa taarifa ya kimaandishi atakayowasilisha, kama ni Mwenyekiti, kwa Rais na kama ni mjumbe mwingine kwa Waziri na tokea tarehe iliyoainishwa katika notisi, mjumbe huyo atakoma kuwa mjumbe wa Tume au kama tarehe haijaainishwa basi ni tokea tarehe ya barua iliyvyopokelewa.

(4) Mjumbe yeyote atakayeshindwa kuhudhuria mikutano mitatu yoyote ya Tume au Kamati mfululizo bila sababu za msingi atachukuliwa kuwa amekoma kuwa mjumbe wa Tume.

Uhalali na  
mwenendo  
wowote

**3.** Uhalali na mwenendo wowote wa Tume hautaathiriwa na nafasi yoyote iliyo wazi kati ya wajumbe au dosari yoyote katika uteuzi wa mjumbe yeyote.

Katibu wa Tume

**4.** Katibu wa Tume atahudhuria mikutano yote lakini hatapiga kura katika mikutano hiyo.

Mikutano na akidi

**5.-(1)** Tume itakutana si chini ya mara nne kwa mwaka katika muda na mahali ambapo Mwenyekiti atakachagua.

(2) Mwenyekiti anaweza, katika muda wowote, kuitisha mkutano maalum wa Tume na-



## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (a) itaitisha mkutano ndani ya wiki sita baada ya kupokea maombi kwa maandishi kwa niaba hiyo ikiainisha sababu ya mkutano huo na kuwasilishwa kwake na kusainiwa na si chini ya wajumbe watatu wa Tume;
- (b) itaitisha mkutano pale atakapoelekezwa na Waziri.
- (3) Katika mkutano wowote wa Tume, si chini ya moja ya tatu ya wajumbe katika ofisi kwa wakati huo watafanya akidi.

Mwaliko kwa wasio wanachama

6. Mwenyekiti anaweza kumwalika mtu yeyote kuhudhuria mkutano wa Tume, na mtu mwingine huyo anaweza kushiriki katika mwenendo wa mkutano huo lakini hatakuwa na haki ya kupiga kura katika mkutano huo.

Mamlaka ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti

7.-(1) Mwenyekiti ataongoza mikutano yote ya Tume.  
(2) Endapo hatakuwepo katika mkutano wowote Makamu Mwenyekiti ataongoza.  
(3) Endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wote hawapo katika mkutano wowote, wajumbe waliopo wanaweza, kutoka miongoni m wao, kumchagua Makamu wa muda ambaye ataongoza mkutano.  
(4) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au mwenyekiti wa muda watakaongoza katika mkutano wowote, watakuwa na kura na ikitokea kura zikalingana atakuwa na kura ya turufu juu ya nyongeza katika majadiliano ya kura.

Tume kusimamia taratibu zake

8. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Tume inaweza kusimamia utaratibu wake.

### JEDWALI LA PILI

*(Limetenenezwa chini ya Kifungu cha 9(1))*

### KIAPPO CHA WAJUMBE

Mimi ..... baada ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti/Mjumbe/Sekretari wa Tume ya Walimu naapa ya kwamba, kwa uhuru na bila woga au fadhila, upendeleo au nia ovyu, nitatimiza majukumu ya Mwenyekiti/Mjumbe wa Tume, na kwamba sitatoa moja kwa moja au vinginevyo, jambo lolote linalohusu majukumu hayo kwa mtu yeyote asisye kuwa na mamlaka au vyoyote vile nikiwa katika utekelezaji.

### MUNGU NISAIDIE

Ameapa/amethibitisha mbele yangu leo tarehe ..... mwezi wa ..... mwaka 20.....

Mbele yangu

Rais/Waziri

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

### MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kuweka masharti kwa ajili ya kutunga Sheria ya kuanzi Tume ya Utumishi wa Walimu kwa ajili ya kuratibu Utumishi wa Walimu wa Shule za umma msi na sekondari za Tanzania Bara.

Muswada huu umegawanyika katika sehemu Kuu Tano. Sehemu ya Kwanza inaweka man ya utangulizi kama Jina la Sheria, sehemu itakayotumika katika Jamhuri ya Muungano na tafsiri ufafanuzi wa maneno au dhana mbalimbali kama zilivyotumiwa katika Sheria hii.

Sehemu ya Pili ya Muswada yenye Ibara mbalimbali inahusu uanzishwaji wa Tume Walimu. Sehemu hii inaanzia Ibara ya 4 ambayo inaelezea namna Tume ya Wali itakavyoanzishwa na kwamba Tume hiyo itakuwa ni Idara ya Serikali inayojitegemea chini W izara yenye dhamana na elimu.

Ibara ya 5 ya Muswada inaelezea kazi za Tume ya Utumishi wa Walimu, kwamba itakuwa wajibu wa kusimamia na kuratibu utumishi wa walimu wa shule za umma za Tanzania Bara itamshauri Waziri kuhusu utaratibu wote unaohusu kuimarisha usimamizi wa utumishi wa walimu kuzingatia masuala ya utumishi, ajira, upandishaji vyeo na nidhamu kwa walimu wa msingi na sh za sekondari za umma yanawekewa utaratibu.

Ibara ya 6 na 7 zinaainisha masharti yanayohusu muundo wa Tume. Katika Ibara h inaelekezwa kuwa Mwenyekiti wa Tume atateuliwa na Rais, wakati wajumbe wengine wa Tu watateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya elimu na Katibu wa Tume atateuliwa na Rais.

Ibara ya 8, 9 na 10 zinaainisha masharti kuhusu uteuzi wa Katibu wa Tume ya Utumishi W alimu na viapo kwa ajili ya wajumbe na ajira za watumishi wa Tume.

Ibara ya 11, 12 na 13 zinaweka utaratibu wa kuanzishwa kwa ofisi za Tume katika ngazi wilaya, na kazi zake, pamoja na masuala ya rufaa kutokana na maamuzi ya mamlaka za nidham Ibara ya 14 inahusu usimamizi wa masuala ya utawala wa waalimu na maslahi yao.

Ibara ya 15 inaweka masharti ya malipo ya wajumbe, ambapo inaelekeza kwamba wajun watalipwa posho na stahili kama Waziri atakavyoamua.

Ibara ya 16 zinaelezea utayarishaji wa Taarifa za mwaka za Tume ya Utumishi wa Wali ambapo taarifa hiyo itakuwa inaeleza utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi cha mw uliopita.

Ibara ya 17 inakataza kutoa taarifa za Tume kwa watu ambao hawajaidhinishwa kup taarifa, hadi ridhaa ya Waziri iwe imetolewa kwa maandishi kuruhusu kutolewa kwa taarifa hizo k amri ya kisheria.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ibara ya 18 inaeleza kuwa ni kosa mtu kutaka au kushawishi Tume kufanya maamuzi. I atakayepatikana na kosa la kushawishi Tume atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa fi ya shilingi laki tano au kutumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na miwili au vyote.

Sehemu ya Tatu ya Muswada huu ina masharti kuhusu mambo ya fedha. Katika Ibara ya 20, 21 na 22 inaelezewa kuwa vyanzo vya mapato ya fedha ya Tume ya Utumishi wa Wali yatakuwa ni yale yaliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yake. Hali kadhalika, Sehe hii kuna masharti yanayohusu namna ambavyo kila mwaka wa fedha, Tume itatayarisha kuwakilisha kwa Waziri mwenye dhamana, taarifa za hesabu za Tume na Taarifa za mwaka. Wa atawasilisha taarifa zilizowasilishwa kwake Bungeni.

Sehemu ya Nne ya Muswada huu yenye Ibara ya 23 na 24 inaweka masharti mbalim kuhusu, jinsi Waziri mwenye dhamana, kwa kushirikiana na Tume ya Walimu atakavyotunga kan chini ya sheria hii na pia kuweka masharti ya mpito kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

Sehemu ya Tano na ya mwisho ya Muswada huu inaainisha ibara zinazohusu marekebi yatokanayo katika Sheria ya Utumishi wa Umma. Marekebicho yanapendekezwa kwa ajili ya kuf kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 6, kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu cha 15 na kif chote cha 30.

Dar es Salaam,  
2 Februari, 2015

**SHUKURU J. KAWAMBWA**  
*Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. MARGARET S. SITTA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kusoma Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*The Teachers Service Commission Act, 2015*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii lakini pia niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Tabora ambao bila wao nisingesimama ndani ya Bunge hili Tukufu; pia niwashukuru wananchi wa Urambo ambao wamenipa ushirikiano muda wote huu; na hali kadhalika kipekee nimshukuru Mzee Sitta ambaye ni kiongozi wa familia yetu ambaye amekuwa akinisaidia kunipa ushauri mbalimbali ambao umenisaidia katika kufanikisha shughuli zangu.

Pia nichukue nafasi hii kabla sijaendelea, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nawapenda, nawaheshimu na ninawashukuru kwa ushirikiano na umakini wenu ambao umewezesha kuja na taarifa hii. Ahsanteni sana Wajumbe wa Kamati hii ya Kudumu ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*The Teachers' Service Commission Act, 2015*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Hansard* ichukue taarifa kama tulivyowasilisha, kwani kutokana na muda kuwa mfupi huenda nisiweze kumaliza yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kwa niaba ya Kamati yangu, kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wenzetu; Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga na Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mbunge wa Geita, ambao walifariki dunia katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kujadili Muswada huu katika vikao vilivyofanyika katika Ukumbi wa Hazina Ndogo uliopo Mjini Dodoma na pia katika Ofisi za Bunge hapa Dodoma. Katika kikao cha kwanza kilichofanyika tarehe 22 Juni, 2015 Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliwasilisha maelezo ya jumla kuhusu madhumuni ya Muswada huo.

Aidha, tarehe 23 Juni, 2015 Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wadau mbalimbali ambao walialikwa kwa lengo la kutoa maoni kuhusiana na Muswada huu. Wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni kwa njia ya kuzungumza ni hawa wafuatao:-

- (i) Chama cha Walimu Tanzania (CWT);
- (ii) Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD);
- (iii) Chama cha Wanasheria Tanzania Bara (TLS); na
- (iv) Shirika lisilo la Kiserikali la HakiElimu.

Aidha, Kamati iliwaalika Wadau wengine ambao hata hivyo hawakuweza kufika mbele ya Kamati kwa lengo la kutoa maoni. Wadau hao weameonyeshwa ndani ya taarifa yetu ya Kamati.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya vikao tarehe 24 hadi 26 Juni, 2015 kwa lengo la kuchambua kwa kina maoni ya Wadau yaliyowasilishwa mbele ya Kamati kuhusiana na Muswada huu. Katika vikao hivyo, Kamati ilihitaji ufafanuzi wa baadhi ya mambo kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya Elimu kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 07 Julai, 2015 Kamati ilikutana na Wizara pamoja na Wawakilishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupata ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo yaliyojitokeza wakati wa ilipokutana na Wadau na pia wakati wa kujadili Muswada huu. Katika kikao hicho, Kamati ilihitaji ufafanuzi wa mambo kadhaa yakiwemo:-

Kwanza, Mwajiri wa Walimu awekwe bayana kuwa ni Tume ya Utumishi wa Walimu (*TSC*); pili, Uhusiano kati ya *TSC* na Serikali za Mitaa; tatu, masuala ya ulipaji wa mishahara ya Walimu; na masuala ya usimamizi wa Shule za Msingi na Sekondari na pia masuala ya taaluma kwamba yatakuwaje katika utendaji wa kazi wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaka kupata maelezo kuhusu uhusiano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na *TSC* ambayo sasa itakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maelezo na kwamba hoja zote zilizotolewa na Kamati zitawekwa katika Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Wizara yanaacha utata kuhusu wajibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi endapo *TSC* itakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakusudia kutunga Sheria ambayo itaanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*TSC*) ambayo itasimamia Utumishi wa Walimu kwa Tanzania Bara ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo katika kusimamia utumishi wa Walimu. Kwa mfumo uliopo sasa, masuala ya Walimu yanasimamiwa na mamlaka tatu tofauti ambazo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Tume ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Utaratibu huu umesababisha hali ya Uwajibikaji na Utawala Bora kuwa ngumu, na hivyo kusababisha usumbufu kwa Walimu wanapofuatilia stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tano ambazo Kamati imezifanyia kazi na kutoa mapendekezo ya kuziboresha na hatimaye kuwa na Sheria ambayo itasimamia Utumishi wa Walimu kwa kuanzisha chombo ambacho kitawezesha kuondoa kero zinazowakabili Walimu katika kutimiza wajibu wao kikamilifu.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza inaelezea jina la Muswada na tarehe ya kuanza kutumika. Kamati inashauri, Kifungu cha (2) kisomeke, Sheria hii itatumika Tanzania Bara kwa Walimu wote walioajiriwa katika Utumishi wa Umma ili kuondoa dhana ya kuyabagua makundi mengine ya Walimu.

Katika Kifungu cha (3) Kamati inashauri, ili kuondoa mkanganyiko katika tafsiri za maneno, tafsiri ya neno “Mwajiri” iwe ni Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) hasa kwa kuzingatia kuwa tafsiri ya maneno “Mamlaka ya Ajira” yamepewa maana ya kuitwa “Tume ya Utumishi wa Walimu” (TSC).

Kamati inashauri, katika tafsiri ya maneno “Mamlaka ya Nidhamu” yaongezwe maneno “na sheria hii” kabla ya maneno “ya kuchukua” na hivyo kufanya tafsiri ya “Mamlaka ya Nidhamu” isomeke kuwa ni “mtu au mamlaka iliyopewa mamlaka na sheria hii ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mwalimu na inajumuisha mtu aliyekasimiwa mamlaka hayo.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inashauri kwamba katika tafsiri ya “Mwalimu” yaongezwe maneno “na Serikali” ili kukifanya kifungu hicho kisomeke, “Mwalimu maana yake ni mtu aliyesajiliwa kama Mwalimu na ambaye amehitimu mafunzo ya Ualimu katika Chuo cha Ualimu au Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Serikali.”

Kamati inashauri kuongezwa kwa tafsiri ya maneno “Mkuu wa Shule” na isomeke; “Mkuu wa Shule maana yake ni Kiongozi Mkuu katika Shule ya Msingi au Sekondari.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya pili inaelezea kuhusu kuanzishwa kwa Tume ambayo itajulikana kama Tume ya Utumishi wa Walimu ambayo itakuwa na dhamana na masuala ya Utumishi wa Walimu kwa kutekeleza majukumu yaliyoanishwa katika Kifungu cha (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchambua kwa kina sehemu hii, Kamati imebaini kasoro kadhaa na inashauri yafanyike marekebisho yafuatayo ili kuleta tija katika utekelezaji wa Sheria hii.

Kwa mfano, Kifungu cha 5(c) kinaelekeza kuwa Tume itakuwa na jukumu la “kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Walimu. Kamati inapendekeza kwamba, pia Tume ipewe jukumu la kutawanya Walimu.

Kwa mantiki hiyo, Kamati inapendekeza kifungu hiki kisomeke; “kuajiri, kutawanya, kupandisha vyeo pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Walimu.”

## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Aidha, Kamati imebaini upungufu mkubwa katika kifungu hiki kwani Tume imepewa kazi ya kusimamia mambo yote yanayohusu Utumishi wa Walimu ikiwa ni pamoja na kuajiri, kupandisha vyeo, kutawanya Walimu na masuala ya nidhamu, lakini imenyimwa kutekeleza jukumu la msingi la kulipa mishahara. Kamati inaona kuwa, iwapo Tume haitatekeleza jukumu la kulipa mishahara basi kuanzishwa kwake hakutakuwa na maana kwani inapoteza sifa ya kuwa Mwajiri na haitaleta tofauti yoyote na mfumo uliopo sasa.

Ikumbukwe kwamba kilio cha Walimu ni kuwa na chombo kimoja kitakachosimamia mambo muhimu ya utumishi wao ikiwa ni pamoja na kuondoa usumbufu ambao wamekuwa wakiupata katika kufuatilia mishahara na stahiki nyingine.

Kamati inashauri Tume ya Utumishi wa Walimu ipewe pia jukumu la kulipa mishahara ya Walimu hata kama itapangwa na Serikali kupitia Menejementi ya Utumishi wa Umma kama ilivyo kwa Watumishi wengine. Kutokana na mantiki hiyo, Kamati inapendekeza katika kazi za Tume, kiongezwe kifungu kidogo ambacho kitatamka wazi kuwa, "miongoni mwa kazi za Tume itakuwa ni kulipa mishahara kwa niaba ya Serikali."

Kifungu cha 5(j) kinaipa Tume jukumu la kuandaa kanuni za maadili ya utendaji kazi ya Ualimu. Kamati inashauri kwamba Tume pia iwe na jukumu la kuzisimamia kanuni ambazo itaziandaa. Kwa mantiki hiyo, Kifungu cha 5 (j) kisomeke; "kuandaa na kusimamia kanuni za maadili ya utendaji kazi wa Mwalimu."

Kamati inapendekeza kiongezwe kifungu kipya ambacho kitaipa Tume jukumu la kuteua Wakuu wa Shule na Vyuo vya Ualimu pamoja na Wakaguzi wa Elimu. Inapendekezwa kifungu hicho kiwe cha 5(m) na kisomeke; "kuteua Wakuu wa Shule, Wakuu wa Vyuo vya Ualimu pamoja na Wakaguzi."

Kifungu cha (6) ambacho kinazungumzia muundo wa Tume kimetaja kwamba, Mwenyekiti wa Tume atateuliwa na Rais na Wajumbe wa Tume watateuliwa na Waziri. Hata hivyo, kifungu hiki hakibainishi sifa za Mwenyekiti na Wajumbe watakaoteuliwa. Ni kwa mantiki hii Kamati inashauri viongezwe vifungu vipya vya 6(2)(a) na 6(2)(b) vitakavyoeleza sifa anazopaswa kuwa nazo Mwenyekiti na Wajumbe kwa mfuatano huo.

Kifungu cha 6(2)(a) kisomeke; "Mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti iwapo ana sifa zifuatazo ambazo tumezifafanua vizuri sana katika taarifa yetu.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kifungu cha 6(2)(b) kisomeke kama kilivyoelezwa, yaani mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Tume hii ya TSC au Tume ya Huduma kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo ya kuundwa kwa vifungu hivyo, kilichokuwa Kifungu cha 6(2) sasa inapendekezwa kiwe Kifungu cha 6(3) na kilichokuwa Kifungu cha 6(3) sasa kiwe Kifungu cha 6(4) ili kuleta mtiririko sawia.

Pia Kamati inapendekeza kwamba, neno “wasiopungua” katika kifungu cha 6(1)(b) liondolewe na badala yake liwekwe neno “wasiozidi.”

Aidha, Kamati inashauri idadi ya Wajumbe wengine iongezwe kutoka nane hadi kumi ili kuyapa makundi ya Walimu uwakilishi zaidi katika Tume. Kutokana na mapendekezo hayo, Kifungu hicho sasa kitasomeka; “Wajumbe wengine wasiozidi kumi watakaoteuliwa na Waziri husika.”

Aidha, mabadiliko haya yatawezesha maana ya kifungu hiki kwenye tafsiri ya Kiswahili kuoana na ile iliyoko kwenye tafsiri ya Kiingereza ambapo maneno “*not more than*” yametumika.

Aidha, kwa lengo la kuongeza uwakilishi wa Walimu katika chombo hiki, ambacho kinaundwa kwa ajili yao, Kamati inapendekeza kuongezwa kwa vifungu vidogo viwili katika Kifungu cha 6(1)(b) ambavyo vitakuwa ni cha (ix) na cha (x). Pia Kifungu cha 6(1)(b) kitakukwa na (ix) yaani uwakilishi kutoka Vyuo vya Ualimu vinavyotambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati inapendekeza kuongezwa kwa Kifungu kipyua cha 6(5) ambacho kitaeleza mambo ambayo yatamfanya mtu akose sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume kama ilivyofafanuliwa kwenye taarifa akiwa na sifa hizi, basi hatakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 7(1) kinaelezwa kwamba, “Tume inaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake, kuteua Kamati mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza majukumu mahsusuni kama itakavyoona inafaa.” Kamati inaona kuwa, kifungu hiki hakioneshi ulazima wa Tume kuwa na Kamati, licha ya umuhimu wa Kamati hizo.

Hivyo basi, Kamati inashauri neno “inaweza” liondoke na kifungu kitamke wazi kuwa, “Tume itateua Kamati mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza majukumu mahusuni.”



## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kifungu cha (8) kinazungumzia juu ya uwepo wa Katibu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais. Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa Katibu atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Tume, aajiriwe na Tume kwa nafasi yake kutangazwa kwa kuzingatia vigezo vya elimu na uzoefu wa masuala ya elimu. Kamati inapendekeza Kifungu cha 8 (1) kiandikwe upya na kusomeka “kutakuwa na Katibu wa Tume ambaye ataajiriwa na Tume.”

Aidha, Kamati inapendekeza Kifungu cha 8(2) kiandikwe upya na kueleza sifa ambazo atatakiwa kuwa nazo Katibu wa Tume kama ilivyofafanuliwa viziuri ndani ya taarifa yetu.

Kifungu cha 11 cha Muswada kinaelezea kuhusu Ofisi za Tume katika ngazi ya Wilaya. Kifungu cha 11(1) kinaeleza kwamba, “kutakuwa na Ofisi ya Tume katika Wilaya zenye idadi ya watumishi kama itakavyoamuliwa na Tume ili kutosheleza majukumu katika Wilaya.” Kamati inaona kuwa kifungu hiki hakiipi Tume mamlaka ya kuanzisha Ofisi zake katika Wilaya, hivyo inapendekeza kifungu hiki kiandikwe upya na kisomeke; “Tume itaanzisha Ofisi katika Wilaya, ambazo zitakuwa na idadi ya Watumishi watakaotosheleza utekelezaji wa majukumu katika Wilaya husika.”

Kifungu cha 12 kinaeleza kazi za Tume katika ngazi ya Wilaya. Hata hivyo, hakioneshi kuwa Tume katika ngazi ya Wilaya itahusika na ulipaji wa mishahara. Kamati inapendekeza kuwa, kwa kuwa imeshauri miongoni mwa kazi za Tume iwe ni ulipaji wa mishahara, basi inapendekeza kuwa miongoni mwa kazi za Tume katika ngazi ya Wilaya iwe ni kulipa mishahara. Hivyo, kuongezwe kifungu kipyamba ambacho kitasomeka kwamba; “kulipa mishahara ya Walimu katika Wilaya husika.”

Kamati inashauri kwamba, Kifungu 12(1)(c) kiandikwe upya ili kizungumzie mkataba wa ajira badala ya fomu ya makubaliano. Maneno “fomu za makubaliano” yaondolewe na badala yake yatumike maneno “mkataba wa ajira” na kifungu hicho kiandikwe upya na kusomeka ifuatavyo;

“itahakikisha kwamba Walimu walioajiriwa chini ya sheria hii, wanajaza na kusaini mkataba wa ajira kabla ya kuripoti katika maeneo yao ya kazi baada ya kuthibitishwa kuwa wanafaa pamoja na kumchukulia Mwalimu hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kupendekeza kufukuzwa kazi” na hivyo kukifanya kifungu cha 12 (g) kiwe na mabadiliko kiwe na mabadiliko kisiende kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya Mwalimu katika maeneo ikiwa ni pamoja na kupendekeza kuwafukuza kazi.”

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Aidha, Kamati inapendekeza wigo wa Mamlaka ya Nidhamu katika shule kuhusu makosa madogo umeminywa sana, hivyo inashauriwa uongezwe kwa kumhusisha Mwalimu Mkuu, Mwalimu Mkuu Msaidizi na Mwalimu mmoja ambaye atachaguliwa na Walimu wengine.

Kutokana na mapendekezo hayo, Kifungu cha 12(2) sasa kisomeke kwamba, “kwa madhumuni ya aya ya (g) ya Kifungu kidogo cha (1), Mamlaka ya Nidhamu katika shule kuhusu makosa madogo itakuwa ni Mwalimu Mkuu wa Shule husika, Mwalimu Mkuu Msaidizi na Mwalimu mmoja ambaye atachaguliwa na Walimu wenzake.”

Kifungu cha 13 kinazungumzia rufaa. Kamati inashauri mabadiliko katika Kifungu cha 13(1) ili kiendane na mapendekezo ya marekebisho ya Kamati katika Kifungu cha 12(1)(g) ambayo yameongeza wigo wa mamlaka ya nidhamu katika ngazi ya shule. Kutokana na mapendekezo hayo, kifungu hiki kiandikwe upya na kisomeke ifuatavyo; “pale ambapo mwalimu hakuridhika na uamuzi wa Mamlaka ya Nidhamu katika ngazi ya shule, anaweza kukata rufaa kwa Tume katika ngazi ya Wilaya.”

Pia Kamati inapendekeza kwamba Kifungu cha 13(3) ambacho kinaelekeza kwamba, rufaa kutoka Tume zielekezwe kwa Rais, kibadilishwe na kumwondolea Rais jukumu hilo. Inapendekezwa kwamba Tume Makao Makuu ndiyo kiwe chombo cha mwisho cha nidhamu.

Kwa mantiki hiyo, Kamati inapendekeza kifungu hicho sasa kisomeke; “uamuzi wa Tume Makao Makuu juu ya rufaa zitakazotokana na maamuzi yaliyopendekezwa na Tume katika ngazi ya Wilaya utakuwa wa mwisho.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 14 kinazungumzia usimamizi wa masuala ya Utawala wa Walimu. Kamati inaona kwamba Kifungu vidogo cha (1) na (2) vinapokonya Tume jukumu lake la msingi la kusimamia Walimu na kulielekeza kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa, jambo ambalo litaifanya Tume kutokuwa na mamlaka juu ya Utumishi wa Walimu. Pia kama vifungu hivi vitaachwa kama vilivyo, vitakuwa vinakinzana na Kifungu cha 5 na 12 vya sheria hii ambavyo vimeeleza kazi za Tume. Kamati inashauri vifungu hivyo vifutwe na Kifungu kidogo cha (3) sasa kiwe Kifungu cha 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yanalenga kuifanya Tume ya Utumishi wa Walimu kuwa na mamlaka kamili ya shughuli zote zinazohusu Utumishi wa Walimu na hivyo kukidhi kiu ya Walimu ambayo siku zote imekuwa ni kuondokana na utitiri wa mamlaka za ajira na kupata chombo kimoja kitakachosimamia masuala ya Walimu tu.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Tatu, sehemu hii inaelezea kuhusu masharti ya fedha. Katika kuchambua na kupitia sehemu hii, Kamati inatoa ushauri ufuatao: kwamba, Kifungu cha 19 kinazungumzia vyanzo vya mapato ya Tume ambapo kifungu kidogo cha (1) kinaeleza kwamba, vyanzo hivyo vitajumuisha fedha zitakazotengwa na Bunge. Hata hivyo, Kamati inaona kwamba, kifungu hiki kimeminya wigo wa mapato ya Tume kwa kutoanisha vyanzo vingine.

Kamati inashauri sheria iruhusu Tume kuwa na vyanzo vingine vya mapato kama vile kutekeleza shughuli za kuingiza mapato, zawadi, michango na misaada kutoka wadau wa elimu. Kamati inashauri Kifungu cha 19 (1) kiandikwe upya na kuwa na sehemu (a), (b) na (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya Muswada inaeleza juu ya masharti mbalimbali. Kifungu cha 23 kinazungumzia juu ya kanuni na Kifungu kidogo cha (1), kinaeleza kwamba, "Waziri atandaa kanuni baada ya kushauriana na Tume, kwa lengo la kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii."

Kamati inashauri kwamba, mara baada ya sheria hii kupitishwa, Waziri atekeleze jukumu hilo mapema ili ianze kutumika hasa kwa kuzingatia kwamba kiu ya Walimu kuwa na chombo kinachosimamia masuala yao ni ya muda mrefu, lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba Walimu hawapatii huduma kwa wakati kutokana na urasimu unaotokana na kusimamiwa na mamlaka mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati inaamini kuwa Muswada huu muhimu umebeba maoni mengi ya wadau wa Sekta ya Elimu na bila shaka utakapokuwa sheria kamili inayoanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu, maoni ya Wadau yatakuwa yamezingatiwa kikamilifu. Aidha, Kamati inachukua fursa hii kuishauri Serikali kutosita pale itakapobaini kuwa kuna umuhimu tena kuangalia upya sheria hii ili kuleta mabadiliko mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuweza kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, nakushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa wasaa huu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu.

Pia nawashukuru Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati hii pale ilipohitajika.

Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Naibu Waziri, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela; na aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu ya Mafunzo ya Ufundi

Mheshimiwa Jenista Mhagama; na pia Mheshimiwa Celina Kombani kwa ushirikiano wao mkubwa katika kufanikisha Muswada huu. Pia Katibu Mkuu Mheshimiwa Sifuani Mchomi pamoja na wataalamu wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioonyesha kwa Kamati hii.

Pia nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa usikivu kwa sababu jambo hili limekuwa la muda mrefu, hatimaye Serikali imesikiliza. Vile vile tunaomba kwamba iwe tayari kufanya marekebisho pale ambapo itaonekana kuna umuhimu wa kuleta mabadiliko hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru kipekee Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ambao wamekuwa na ushirikiano mkubwa, wamenichagua, nimekuwa Mwenyekiti kwa miaka mitano. Nawashukuru sana Wajumbe na pia na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Charles Mloka na Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Happiness Ndalu, Ndugu Gerald Magili na Ndugu Nesta Kawamala kwa ushauri na uratibu wa kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Hoja ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuanzisha  
Tume ya Utumishi wa Walimu  
(The Teachers' Commission Bill, 2015)**

**Kama ilivyowasilishwa Mezani**

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU  
MUSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (THE  
TEACHERS' SERVICE COMMISSIONBILL, 2015)**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*The Teachers' Service Commission Act, 2015*).

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nachukua fursa hii kwa niaba ya Kamati yangu, kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge

Iako Tukufu kwa kuondokewa na wenzetu; Mheshimiwa Eugen Elishilinga Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga na Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mbunge wa Geita, ambao walifariki dunia katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kujadili Muswada huu katika vikao vilivyofanyika katika Ukumbi wa Hazina Ndogo, uliopo Mjini Dodoma na pia katika Ofisi za Bunge hapa Dodoma. Katika kikao cha kwanza kilichofanyika tarehe 22 Juni, 2015 Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliwasilisha maelezo ya jumla kuhusu madhumuni ya Muswada huo.

Aidha, tarehe 23 Juni, 2015 Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wadau mbalimbali ambao walialikwa kwa lengo la kutoa maoni kuhusiana na Muswada huu. Wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni kwa njia ya kuzungumza ni hawa wafuatao:-

- (i) Chama cha Walimu Tanzania (CWT);
- (ii) Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD);
- (iii) Chama cha Wanasheria Tanzania Bara (TLS); na
- (iv) Shirika lisilo la Kiserikali la HakiElimu.

Aidha, Kamati iliwaalika Wadau wengine ambao hata hivyo hawakuweza kufika mbele ya Kamati kwa lengo la kutoa maoni. Wadau hao ni pamoja na:-

- (i) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- (ii) Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuho Binafsi Nchini (TAMONGSCO); na
- (iii) Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya vikao tarehe 24 hadi 26 Juni, 2015 kwa lengo la kuchambua kwa kina maoni ya Wadau yaliyowasilishwa mbele ya Kamati kuhusiana na Muswada huu. Katika vikao hivyo Kamati ilihitaji ufafanuzi wa baadhi ya mambo kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya Elimu kuhusiana na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika, Tarehe 07 Julai, 2015 Kamati ilikutana na Wizara pamoja na Wawakilishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupata ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo yaliyojitokeza wakati wa ilipokutana na Wadau na pia wakati wa mjadala wa Muswada huu.**

**Katika kikao hicho Kamati ilihitaji ufafanuzi wa mambo kadhaa yakiwemo mwajiri wa walimu awekwe bayana kuwa ni Tume ya utumishi wa walimu (TSC), uhusiano kati ya TSC na Serikali za Mitaa, masuala ya ulipaji wa mishahara ya walimu na masuala ya usimamizi wa shule za msingi na Sekondari, kwa masuala ya taaluma utakuwaje, Kamati ilitaka kupata maelezo kuhusu uhusiano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na TSC ambayo sasa itakuwa chini ya ofisi ya Waziri Mkuu kwa maelezo na kwamba hoja zote zilizotolewa na Kamati zitawekwa katika Kanuni.**

**Mheshimiwa Spika, maelezo ya Wizara yanaacha utata kuhusu wajibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi endapo TSC itakuwa chini ya ofisi ya Waziri Mkuu.**

**Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kutunga Sheria ambayo itaanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambayo itasimamia Utumishi wa Walimu kwa Tanzania Bara ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo katika kusimamia utumishi wa Walimu.**

Kwa mfumo uliopo sasa masuala ya Walimu yanasimamiwa na mamlaka tatu tofauti ambazo ni; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Tume ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Utaratibu huu umesababisha hali ya uwajibikaji na utawala bora kuwa ngumu, na hivyo kusababisha usumbufu kwa Walimu wanapofuatilia stahiki zao.

**Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu Tano ambazo Kamati imezifanyia kazi na kutoa mapendekezo ya kuziboresha na hatimaye kuwa na Sheria ambayo itasimamia Utumishi wa Walimu kwa kuanzisha chombo ambacho kitawezesha kuondoa kero zinazowakabili Walimu katika kutimiza wajibu wao kikamilifu.**

### **1.1 Sehemu ya kwanza**

**Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inaelezea jina la Muswada na tarehe ya kuanza kutumika. Kamati inashauri kifungu cha pili kosomeke, **Sheria hii itatumika Tanzania Bara kwa Walimu wote walioajiriwa katika Utumishi wa Umma**, ili kuondoa dhana ya kuyabagua makundi mengine ya Walimu.**

Katika kifungu cha Tatu Kamati inashauri ili kuondoa mkanganyiko katika tafsiri za maneno, tafsiri ya neno **“Mwajiri”** iwe ni Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) hasa kwa kuzingatia kuwa tafsiri ya maneno **“Mamlaka ya Ajira”** yamepewa maana kuwa ni **“Tume ya Utumishi wa Walimu” (TSC).**

Kamati inashauri katika tafsiri ya maneno **“Mamlaka ya nidhamu”** yaongezwe maneno **“na sheria hii”** kabla ya maneno **“ya kuchukua”** na hivyo kufanya tafsiri ya **“Mamlaka ya nidhamu”** isomeke kuwa ni **“mtu au mamlaka iliyopewa mamlaka na sheria hii ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mwalimu na inajumuisha mtu aliyekasimiwa mamlaka hayo.”**

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inashauri kwamba, katika tafsiri ya **“Mwalimu”** yaongezwe maneno **“na Serikali”** ili kukifanya kifungu hicho kisomeke, Mwalimu maana yake ni **“mtu aliyesajiliwa kama Mwalimu na ambaye amehitimu mafunzo ya ualimu katika Chuo cha Ualimu au Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Serikali.”**

Kamati inashauri kuongezwa kwa tafsiri ya maneno **“mkuu wa shule”** na **isomeke ifuatavyo; “mkuu wa shule”** maana yake ni kiongozi mkuu katika shule ya msingi au sekondari.

## 1.2 Sehemu ya pili

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inaelezea kuhusu kuanzishwa kwa Tume ambayo itajulikana kama Tume ya Utumishi wa Walimu ambayo itakuwa na dhamana na masuala ya utumishi wa Walimu kwa kutekeleza majukumu yaliyoanishwa katika kifungu cha 5.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua kwa kina sehemu hii Kamati imebaini kasoro kadhaa na inashauri yafanyike marekebisho yafuatayo ili kuleta tija katika utekelezaji wa Sheria hii.

(i) Kifungu cha 5(c) kinaelekeza kuwa Tume itakuwa na jukumu la **“kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Walimu.** Kamati inapendekeza kwamba, Tume ipewe pia jukumu la kutawanya Walimu. Kwa mantiki hiyo Kamati inapendekeza kifungu hiki kisomeke **“kuajiri, kutawanya, kupandisha vyeo pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Walimu.**

Aidha, Kamati imebaini mapungufu makubwa katika kifungu hiki kwani, Tume imepewa kazi ya kusimamia mambo yote yanayohusu Utumishi wa Walimu ikiwa ni pamoja na kuajiri, kupandisha vyeo, kutawanya Walimu na masuala ya nidhamu, lakini imenyimwa kutekeleza jukumu la msingi la kulipa mishahara.

Kamati inaona kuwa, iwapo Tume haitatekeleza jukumu la kulipa mishahara basi kuanzishwa kwake hakutakuwa na maana kwani inapoteza sifa ya kuwa **Mwajiri** na haitaleta tofauti yoyote na mfumo uliopo sasa.

Ikumbukwe kwamba, kilio cha Walimu ni kuwa na chombo kimoja kitakachosimamia mambo muhimu ya utumishi wao ikiwa ni pamoja na kuondoa usumbufu ambao wamekuwa wakiupata katika kufuatilia mishahara na stahiki nyingine. Kamati inashauri Tume ya Utumishi wa Walimu ipewe pia jukumu la kulipa mishahara ya Walimu hata kama itapangwa na Serikali kupitia Menejementi ya Utumishi wa Umma kama ilivyo kwa Watumishi wengine.

Kutokana na mantiki hiyo Kamati inapendekeza katika kazi za Tume, kiongezwe kifungu kidogo ambacho kitatamka wazi kuwa, miongoni mwa kazi za Tume itakuwa ni “**kulipa mishahara**”.

(ii) Kifungu cha 5(j) kinaipa Tume jukumu la kuandaa kanuni za maadili ya utendaji kazi ya ualimu. Kamati inashauri kwamba, Tume pia iwe na jukumu la kuzisimamia kanuni ambazo itaziandaa. Kwa mantiki hiyo kifungu cha 5 (j) kisomeke “**kuandaa na kusimamia kanuni za maadili ya utendaji kazi wa Mwalimu.**”

(iii) Kamati inapendekeza kiongezwe kifungu kipya ambacho kitaipa Tume jukumu la kuteua wakuu wa shule na vyuo vya ualimu pamoja na wakaguzi wa elimu. Inapendekezwa kifungu hicho kiwe cha 5(m) na kisomeke “**kuteua wakuu wa shule, wakuu wa vyuo vya ualimu pamoja na wakaguzi wakuu wa elimu.**”

(iv) Kifungu cha 6 ambacho kinazungumzia muundo wa Tume kimetaja kwamba, Mwenyekiti wa Tume atateuliwa na Rais na Wajumbe wa Tume watateuliwa na Waziri. Hata hivyo, kifungu hiki hakibainishi sifa za Mwenyekiti na Wajumbe watakaoteuliwa. Ni kwa mantiki hii Kamati inashauri viongezwe vifungu vipya vya 6(2) (a) na 6(2)(b) vitakavyoeleza sifa anazopaswa kuwa nazo Mwenyekiti na Wajumbe kwa mfuatano huo.

**Kifungu cha 6(2)(a) kisomeke;**

Mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume iwapo;

- (a) ni raia wa Tanzania
- (b) ana shahada ya uzamili au uzamivu ya elimu kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa na Serikali;



(c) ana uzoefu wa kazi ya Ualimu kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na mitano;

(d) ana uwezo wa kushughulikia masuala ya Walimu.

**Kifungu cha 6(2)(b) kisomeke;**

**Mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Tume iwapo;**

(a) ni raia wa Tanzania

(b) ana shahada kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa na Serikali;

(c) ana ujuzi na uzoefu wa kipindi kisichopungua miaka kumi katika nyanja zifuatazo:-

- (i) elimu
- (ii) utawala
- (iii) menejimenti, au
- (iv) sheria

(d) ameonesha uwezo wa kushughulikia masuala ya Walimu.

Kutokana na mapendekezo ya kuundwa kwa vifungu hivyo kilichokuwa kifungu cha 6(2) sasa inapendekezwa kiwe kifungu cha 6(3) na kilichokuwa kifungu cha 6(3) sasa kiwe kifungu cha 6(4) ili kuleta mtiririko sawia.

Pia Kamati inapendekeza kwamba, neno “**wasiopungua**” katika kifungu cha 6(1)(b) liondolewe na badala yake liwekwe neno “**wasiozidi.**” Aidha, Kamati inashauri idadi ya Wajumbe wengine iongezwe kutoka nane hadi kumi ili kuyapa makundi ya Walimu uwakilishi zaidi katika Tume. Kutokana na mapendekezo hayo kifungu hicho sasa kitasomeka “**Wajumbe wengine wasiozidi kumi watakaoteuliwa na Waziri kutoka;**

Mabadiliko haya yatawezesha maana ya kifungu hiki kwenye tafsiri ya Kiswahili kuoana na ile iliyoko kwenye tafsiri ya Kingereza ambapo maneno “**not more than...**” yametumika.

Aidha, kwa lengo la kuongeza uwakilishi wa Walimu katika chombo hiki ambacho kinaundwa kwa ajili yao, Kamati inapendekeza kuongezwa kwa vifungu vidogo viwili katika 6(1)(b) ambavyo vitakuwa (ix) na (x). Kifungu cha 6(1)(b) (ix) uwakilishi kutoka Vyuo vya Ualimu vinavyotambuliwa na Serikali na 6(1)(b)(x) Chombo kinachosimamia ubora wa Elimu (Ukaguzi).

Vilevile Kamati inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya 6(5) ambacho kitaeleza mambo ambayo yatamfanya mtu akose sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume. Kifungu hicho kisomeke ifuatavyo:-

**6.-(5) Mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume iwapo mtu huyo:**

- (a) ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;**
- (b) ni Diwani;**
- (c) kiongozi wa chama cha siasa; au**
- (d) amewahi kupatikana na hatia ya jinai au kutumia vibaya madaraka au ofisi ya Umma.**

(v) Kifungu cha 7(1) kinaelezwa kwamba Tume inaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji wa majukumu yake, kuteua Kamati mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza majukumu mahsusi kama itakavyoona inafaa. Kamati inaona kuwa, kifungu hiki hakioneshi ulazima wa Tume kuwa na Kamati, licha ya umuhimu wa Kamati hizo. Hivyo, basi Kamati inashauri neno “inaweza” liondoke na kifungu kitamke wazi kuwa Tume “**itaeua**” Kamati mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza majukumu mahususi...

(vi) Kifungu cha 8 kinazungumzia juu ya uwepo wa Katibu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais. Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa Katibu atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa Tume, aajiriwe na Tume kwa nafasi yake kutangazwa kwa kuzingatia vigezo vya elimu na uzoefu wa masuala ya elimu. Kamati inapendekeza kifungu cha 8.-(1) kiandikwe upya na kusomeka “**kutakuwa na Katibu wa Tume ambaye atajiriwa na Tume**”.

Aidha, Kamati inapendekeza kifungu cha 8(2) kiandikwe upya na kueleza sifa ambazo atatakiwa kuwa nazo Katibu wa Tume. Inapendekeza kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo:-

Mtu atakuwa na sifa za kuajiriwa kama Katibu wa Tume iwapo;

- (i) ana shahada ya uzamili ya ualimu kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa na Serikali;**
- (ii) ana uzoefu wa ualimu kwa kipindi kisichopungua miaka kumi; na**

(iii) sifa nyingine zitakazoainishwa na Tume,

(vii) Kifungu cha 11 cha Muswada kinaelezea kuhusu ofisi za tume katika ngazi ya Wilaya. Kifungu cha 11(1) kinaeleza kwamba, kutakuwa na ofisi za Tume katika Wilaya zenye idadi ya watumishi kama itakavyoamuliwa na Tume watakaotosheleza majukumu katika Wilaya husika. Kamati inaona kuwa kifungu hiki hakiipi Tume mamlaka ya kuanzisha ofisi zake katika Wilaya, hivyo inapendekeza kifungu hiki kiandikwe upya na kusomeka; **“Tume itaanzisha ofisi katika Wilaya, ambazo zitakuwa na idadi ya Watumishi watakaotosheleza utekelezaji wa majukumu katika Wilaya husika.”**

(viii) Kifungu cha 12 kinaeleza kazi za Tume katika ngazi ya Wilaya. Hata hivyo hakioneshi kuwa Tume katika ngazi ya Wilaya itahusika na ulipaji wa mishahara. Kamati inapendekeza kuwa, kwa kuwa imeshauri miongoni mwa kazi za Tume iwe ni ulipaji wa mishahara, basi inapendekeza kuwa miongoni mwa kazi za Tume katika ngazi ya Wilaya iwe ni kulipa mishahara. Hivyo, kuongezwe kifungu kipya ambacho kitasomeka kwamba; **“kulipa mishahara ya Walimu katika Wilaya husika.”**

Kamati inashauri kwamba, Kifungu 12(1)( c) kiandikwe upya ili kizungumzie mkataba wa ajira badala ya fomu ya makubaliano. Maneno **“fomu za makubaliano”** yaondolewe na badala yake yatumike maneno **“mkataba wa ajira”** na kifungu hicho kiandikwe upya na kusomeka ifuatavyo;

**“itahakikisha kwamba Walimu walioajiriwa chini ya sheria hii wanajaza na kusaini mkataba wa ajira kabla ya kuripoti katika maeneo yao ya kazi baada ya kuthibitishwa kuwa wanafaa.”**

Vilevile Kamati inapendekeza kwamba, mamlaka ya nidhamu kwa ofisi za Tume katika ngazi ya Wilaya yaongezwe iwe ni pamoja na kumfukuza kazi Mwalimu ambaye ametenda kosa linalostahili afukuzwe kazi. Kwa mantiki hiyo, Kamati inapendekeza maneno **“ikiwa ni pamoja na kupendekeza kuwafukuza kazi”** yaongezwe katika kifungu 12(g) na hivyo kukifanya kifungu hicho kisomeke **“kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Walimu katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kupendekeza kuwafukuza kazi.”**

Aidha, Kamati inapendekeza wigo wa mamlaka ya nidhamu katika shule kuhusu makosa madogo umeminywa sana hivyo inashauriwa uongezwe kwa kuhusisha Mwalimu Mkuu, Mwalimu Mkuu Msaidizi na Mwalimu mmoja ambaye atachaguliwa na Walimu wengine.

Kutokana na mapendekezo hayo kifungu cha 12(2) sasa kitasomeka **“kwa madhumuni ya aya ya (g) ya kifungu kidogo cha (1) mamlaka ya nidhamu katika shule kuhusu makosa madogo itakuwa ni mwalimu mkuu wa**

**shule husika, mwalimu mkuu msaidizi na mwalimu mmoja ambaye atachaguliwa na walimu wengine.**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la mapendekezo haya ni kuondoa uwezekano wa Mwalimu Mkuu kutotenda haki kwa Mwalimu anayetuhumiwa kukosa au kuonesha utovu wa nidhamu na pia kujengea mamlaka hii ya nidhamu mazingira ya kuaminika zaidi kwa Walimu.

(ix) Kifungu cha 13 kinazungumzia rufaa. Kamati inashauri mabadiliko katika kifungu cha 13(1) ili kiendane na mapendekezo ya marekebisho ya Kamati katika kifungu cha 12(1)(g) ambayo yameongeza wigo wa mamlaka ya nidhamu katika ngazi ya shule. Kutokana na mapendekezo hayo, kifungu hiki kiandikwe upya na kisomeke ifuatavyo;

**“Pale ambapo mwalimu hakuridhika na uamuzi wa mamlaka ya nidhamu katika ngazi ya shule, anaweza kukata rufaa kwa tume katika ngazi ya Wilaya.”**

Pia Kamati inapendekeza kwamba, kifungu cha 13(3) ambacho kinaelekeza kwamba, rufaa kutoka Tume zielekezwe kwa Rais, kibadilishwe na kumuondolea Rais jukumu hilo. Inapendekezwa kwamba, tume makao makuu ndiyo iwe chombo cha mwisho cha nidhamu.

Kwa mantiki hiyo, Kamati inapendekeza kifungu hicho sasa kisomeke **“uamuzi wa Tume Makao Makuu juu ya rufaa zitakazotokana na maamuzi yaliyopendekezwa na tume katika ngazi ya wilaya utakuwa wa mwisho.”**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la mapendekezo haya ni kupunguza mlolongo wa rufani, na hasa kwa kuzingatia kwamba, Rais ana majukumu mengi ya kutekeleza.

(x) Kifungu cha 14 kinazungumzia usimamizi wa masuala ya utawala wa Walimu. Kamati inaona kwamba, vifungu vidogo vya (1) na (2) vinaipokonya tume jukumu lake la msingi la kusimamia Walimu na kulielekeza kwenye mamlaka ya serikali za mitaa, jambo ambalo litaifanya tume kutokuwa na mamlaka juu ya utumishi wa Walimu. Pia kama vifungu hivi vitaachwa kama vilivyo vitakuwa vinakinzana na vifungu vya 5 na 12 vya sheria hii ambavyo vimeeleza kazi za tume. Kamati inashauri vifungu hivyo vifutwe na kifungu kidogo cha tatu sasa kiwe kifungu cha 14.

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo haya yanalenga kuifanya tume ya utumishi wa Walimu kuwa na mamlaka kamili ya shughuli zote zinazohusu utumishi wa Walimu na hivyo kukidhi kiu ya Walimu ambayo siku zote imekuwa ni kuondokana na utitiri wa mamlaka za ajira na kupata chombo kimoja kitakachosimamia masuala ya Walimu tu.

### 1.3 Sehemu ya tatu

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inaelezea kuhusu masharti ya fedha. Katika kuchambua na kupitia sehemu hii, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kifungu cha 19 kinazungumzia vyanzo vya mapato ya tume ambapo kifungu kidogo cha (1) kinaeleza kwamba, vyanzo hivyo vitajumuisha fedha zitakazotengwa na Bunge. Hata hivyo, Kamati inaona kwamba, kifungu hiki kimeminya wigo wa mapato ya tume kwa kutoanisha vyanzo vingine. Kamati inashauri sheria iruhusu tume kuwa na vyanzo vingine vya mapato kama vile **“kutekeleza shughuli za kuingiza mapato, zawadi, michango na misaada kutoka wadau wa elimu”**

**Kamati inashauri kifungu cha 19 (1) kiandikwe upya na kuwa na sehemu (a) (b) na (c) na kisomeke ifuatavyo:**

#### 19.(1) Vyanzo vya mapato ya Tume vitajumuisha;-

- (a) fedha zitakazotengwa na Bunge kwa ajili ya tume;
- (b) misaada, zawadi na michango kutoka kwa wadau wa elimu; na
- (c) fedha zitakazotokana na shughuli zitakazotekelezwa na tume.

### 1.4 Sehemu ya nne

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya Muswada inaeleza juu ya masharti mbalimbali. Kifungu cha 23 kinazungumzia juu ya kanuni na kifungu kidogo cha (1) kinaeleza kwamba, Waziri atandaa kanuni baada ya kushauriana na tume, kwa lengo la kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii. Kamati inashauri kwamba, mara baada ya sheria hii kupitishwa Waziri atekeleze jukumu hilo mapema ili ianze kutumika hasa kwa kuzingatia kwamba, kiu ya Walimu kuwa na chombo kinachosimamia masuala yao ni ya muda mrefu sana, lakini pia ni ukweli usioplingika kwamba, Walimu hawapati huduma kwa wakati kutokana na urasimu unaotokana na kusimamiwa na mamlaka mbalimbali serikalini.

Kifungu cha 24 katika tafsiri ya Kiswahili hakieleweki vizuri kama ilivyo katika tafsiri ya Kingereza. Kamati inashauri kifungu hiki kiandikwe upya kwa kuzingatia maana iliyopo katika tafsiri ya kingereza na inapendekeza kisomeke ifuatavyo:-

**Kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, Waziri ndani ya muda wowote kabla ya kumalizika kwa kipindi cha miezi sita tangu kuanza kutumika kwa sheria hii, ataandaa masharti ya mpito ambayo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya sheria hii.**

## **SEHEMU YA TANO**

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii ya Muswada inaeleza juu ya marekebisho yatoakanayo ambapo baadhi ya vifungu vya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 vitafanyiwa marekebisho ili kutokinzana na masharti ya utekelezaji wa sheria hii.

### **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaamini kuwa, Muswada huu muhimu umebeba maoni mengi ya wadau wa Sekta ya Elimu, na bila shaka utakapokuwa Sheria kamili inayoanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu, maoni ya Wadau yatakuwa yamezingatiwa kikamilifu. Aidha, Kamati inachukua fursa hii kuishauri Serikali kutosita pale itakapobaini kuna maeneo yatayohitaji marekebisho, kuleta mabadiliko mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuweza kuboresha zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia wasaa wa kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Pia ninawashukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati pale ulipohitajika.

Aidha tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, (Mb) Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Waziri Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, (Mb) na aliyekuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama, Mb, Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome pamoja na wataalamu wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha kwa Kamati.

Pia ninawashukuru Wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ambayo yameisaidia sana Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Kwa namna ya pekee niaomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa ushirikiano wao na pia michango na mapendekezo ambayo yanalenga kuboresha Muswada huu. Ninapenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Stephen Hilary Ngonyani, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Faki Haji Makame, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Agripina Zaituni Buyogera, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Christowaja Gerson Mtinda, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt Antony Gervas Mbassa, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Riziki Omari Juma, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Ezekia Dibogo Wenje, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ali Juma Haji, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Gregory George Teu, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Abia Muhama Nyabakari, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Salome Daudi Mwambu, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Zabein Muhaji Mhita, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Mohamed Gulam Dewji, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Hasnain Mohamed Murji, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Juma Sururu Juma, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndugu Charles Mloka na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Happiness Ndalul, Ndugu Gerald Magili na Ndugu Nesta Kawamala kwa ushauri na uratibu wa kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,**

Ninaunga mkono Muswada na ninaomba kuwasilisha.

Margaret Simwanza Sitta, Mb  
**KAIMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII**  
**27 Juni, 2015**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Margaret Mkanga wajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Muswada huu muhimu unaowahusu Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda niishukuru na kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuona umuhimu wa dhati kabisa wa kuingiza Muswada huu tena kwa haraka kwa maslahi yetu sisi Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda ku *declare interest* kwamba mimi ni Mwalimu wa Shule ya msingi. Muswada huu unalenga moja kwa moja Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kwa vile inaweza kuwa ni mara yangu ya mwisho leo kusimama kwenye Bunge hili kwa wakati huu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kunichagua niwe Mbunge wao. Nami nina imani nimewawakilisha vizuri sana na kama Mungu atapenda kwa ridhaa yenu nitaendelea kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Kamati ya Huduma za Jamii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kupitia Muswada huu. Pia nawashukuru wadau nikiwemo na mimi mwenyewe, tumekuwa tukishinda na kukesha kuujadili na kuuchambua Muswada huu kwa maslahi ya Walimu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha Walimu, kila siku tulikuwa tunauliza, hivi sisi Walimu mwajiri wetu ni nani? Hili swali ambalo lilikuwa likitupata kila siku Waalimu mwajiri wetu ni nani? Serikali kwa kuona hilo, wametuletea Muswada huu wa uwazishaji wa Tume ya Walimu. Tume hii ndiyo itakuwa mwajiri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Walimu kila anayeajiriwa anasema mimi nimeajiriwa na Mkurugenzi Manispaa ya Temeke, ama Mkurugenzi Manispaa ya Iringa! Kila mmoja anaandika vyake, kila mmoja ana historia yake.

Sasa hii itakwisha na wote wataajiriwa na Tume hii ya Utumishi ya Walimu. Ni jambo jema tunaishukuru sana na kuipongeza Serikali. Pia Tume hii itashughulikia maslahi ya Walimu katika upanganyaji na ugawanyaji wa Walimu; jinsi gani Mwalimu anaweza kupatiwa huduma mbalimbali ambazo zilikuwa kero kwa Walimu.



## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo dogo! Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Lakini wapo watu! Nataka niwaambie Walimu wenzangu, kuna watu watakuja huko, watajifanya wao wanaelewa kuliko wengine kwa kuona kwamba labda hii Tume imeanzishwa sijui kwanini, au kwa nini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu ni muhimu! Walimu kwenye Sherehe ya Wafanyakazi walimwuliza Mheshimiwa Rais; Unatuachaje? Sasa na Rais anawaacha na hili! Kawajengea chombo kimoja. Mheshimiwa Rais anatuacha vizuri Walimu. Ameweza kutatua kilio chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, jinsi gani amepambana katika kutatua matatizo mbalimbali katika sekta mbalimbali. Sisi Walimu tunamshukuru sana sana! Yapo mambo mengi ambayo atatufanyia kabla ya kuondoka, lakini pia kubwa alilolifanya ni kutuletea Muswada huu ambao kwetu sisi ni maslahi. *(Makofi)*

Vile vile wapo watu wanasema, kuna vipengele haviko sawa. Hii ni sheria! Inaweza ikarekebishika wakati wowote. Kwanza tuangalie je, tumepata? Kile tulichokitaka tumekipata? Kweli tulichokitaka tumekipata. Leo hapa kwa uwezo wa Mungu sheria hii itapita. Tumepata, changamoto zipo, lakini zinarekebishika. Aliyepata amepata tu, siyo sawa na aliyekosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali, lakini naishauri sasa Serikali yangu. Kuna kipengele au sehemu ambayo Tume hii pamoja na yote itafanya kazi na TAMISEMI kwa sababu tayari TAMISEMI ina majengo, madarasa na imewekeza. Sasa naiomba Serikali iangalie, Katibu wa Tume ile wa Wilaya aweze kuingia moja kwa moja kwenye Vikao vyote vya Halmashauri ili naye aweze kuchangia na kuelewa, kwa sababu wao ndio watakaolipa mishahara wale watu wa Halmashauri. Kwa hiyo, nitaiomba Serikali iangalie katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine juu ya uhamisho wa Walimu; uhamisho kwa Walimu ni kero kubwa. Mwalimu anaajiriwa leo Musoma, anataka kurudi Dar es Salaam. Anaambiwa apate mtu wa kubadilishana naye, aje Dar es Salaam wewe uende Musoma. Jamani, mimi nina imani, hii Tume sasa turejee tulikotoka. Sisi tuliajiriwa miaka ya 1979 na 1980, haya hayakuwepo! Sasa nimeona Serikali imeona umuhimu kweli wa kurudisha.

Hata yale ya zamani yaliyo bora yanapaswa kufanyiwa kazi. Sasa Mwalimu asisumbuliwe tena na TAMISEMI. Kama anataka kuhama kumfuata mumewe, basi utaratibu wote utafanyika na Tume.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiki kitu ni chema na niombe sana Serikali iweze kusaidia na Wabunge wenzangu, tuisaidie sheria hii ipite kwa maslahi ya Walimu wa Shule za Misingi na wale wa Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi tena kwa Walimu wenzangu Tanzania; yapo mambo mengi, changamoto zetu ni nyingi kama Walimu, lakini changamoto zote haziwezi kwisha kwa siku moja. Sisi tuliokuja humu miongoni menu mmepata Wawakilishi na hili Bunge hili lina Walimu wengi tu. Niwaambie sasa, hiki kitu kinachokuja, tena narudia, siyo kibaya kwetu! Kingekuwa kibaya na sisi hapa tukitoka Bungeni, tutarudi huko kwenye chaki. Kwanini tupitishie kitu ambacho hakina maslahi nasi.

Kwa hiyo, nawaomba sana mpokee hii Tume na tuipe ushirikiano, hii sheria ipite, upungufu wote tutaufanyia kazi, utakuja hapa tutafanya *amendment* kama tutaona kuna tatizo, lakini ni Tume nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kwa mara nyingine niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwenye Bunge hili kwa jinsi walivyoniipa ushirikiano katika utendaji wangu kazi, japokuwa nilikuja katika kipindi cha pili cha Bunge, lakini nina imani kwenye Bunge lijalo nitakuja kwenye kipindi cha kwanza kabisa cha Bunge kwa uwezo wa Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Subira na Mheshimiwa Margareth Mkanga na Mheshimiwa Abdul Marombwa wajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kusimama ndani ya Bunge hili, lakini nikisimama namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nasimama ndani ya Bunge hili nikiamini uwezo wangu ndani ya Bunge hili umetokana na Walimu kwa namna ambavyo wametupa elimu na ndiyo maana tuna uwezo wa kusimama na kuchangia masuala mbalimbali.

Pia natambua mchango mkubwa wa Walimu wote katika maisha yangu na hasa katika fani yangu ya Uhasibu. Kwa hiyo, ninaposimama pia katika Bunge hili kwa dakika za mwisho mwisho, nachukua fursa hii kuwapongeza Walimu wote nchini Tanzania wa Msingi na Sekondari lakini hususan Walimu wa Mkoa ninaouwakilisha wa Pwani, Walimu wa Bagamoyo, Kisarawe, Mafia, Kibaha, Rufiji na Mkurunga. Nawashukuru kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuinua kiwango cha elimu katika Mkoa wetu katika nyakati mbalimbali.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia nawapongeza sana Walimu wa Shule ya Sekondari ya Wama na Kayama kwa kufaulisha wanafunzi 58 kwenda Kidato cha Tano mwaka huu, shule maalum ya wasichana wanaotokana na mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa Muswada huu. Naipongeza sana Wizara ya Elimu na viongozi wake. Lakini kipekee naipongeza Kamati ya Huduma za Jamii chini ya uongozi wa mama mahiri Mheshimiwa Margaret Sitta. Tangu niingie Bunge hili awamu hii ya kwanza nimemsikia Mwenyekiti na Kamati hii ikililia Tume ya Utumishi ya Walimu.

Kwa hiyo, leo tunapojadili Muswada huu ama kwa hakika ni fanikio kubwa sana kwa Kamati hii ya Bunge ya Kuduma lakini hata kwa Bunge hili la Kumi kwa namna ambavyo imesikiliza kilio cha Walimu Tanzania kwa uhitaji wa Tume hii ya Watumishi ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa nchi yetu ni wavumilivu. Wameidai sana Tume hii. Lakini kama Waswahili wanavyosema subira yavuta heri na leo sasa wanaona ni jinsi gani Serikali hii sikivu imesikia kilio chao na Tume hii, Muswada huu umewasilishwa Bungeni na kwa sisi Wabunge wote wenye nia njema tunaujadili na tunaridhia, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa sababu kazi za Tume hii ya Watumishi wa Walimu zimeelezwa kinabaubaga katika sehemu ya pili Kifungu cha (5), lakini pia naona na maoni ya Kamati namna ambavyo wamechambua Kifungu hiki cha (5) kazi zake; naomba pia kwa mujibu wa taratibu mbalimbali na sheria mbalimbali za fedha zingetazamwa kwa umakini wake na pengine Kamati inayo sababu ya msingi kwamba Tume hii ya Utumishi kama imepewa mamlaka ya kuajiri Walimu, kuwapandisha vyeo kwa sababu tatizo lililokuwepo sasa hivi wakati tuna TSD; TSD ilikuwa inapandisha vyeo Walimu, lakini inachukua muda mrefu Walimu hawa yale mabadiliko yao kuingia kwenye taratibu za kubadilishwa rasmi na kubadilishwa mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Walimu wanachukua zaidi ya miaka minne, mitano enzi ya zamani. Lakini naipongeza Idara kuu ya Utumishi kwa namna ambavyo wamefanya maboresho kupitia *Lawson*, angalau sasa, lakini bado tatizo lipo. Bado Walimu wengi wanadai malimbikizo ya mishahara yao na Walimu wengi bado wanadai vyeo vyao. Kwa hiyo, naamini kama kweli tumeipa mamlaka ya kuajiri, kupandisha vyeo, basi tupe mamlaka. Naamini mishahara itaendelea kulipwa na Serikali Kuu kupitia Hazina. (*Makofi*)

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara zote, kwa mfano, Idara ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inajipangia mishahara, inaomba kibali Idara Kuu ya Utumishi lakini unaona utaratibu kwamba mishahara inakuja kwenye Idara yao wanalipana. Kwa hiyo, nadhani hili siamini kama ni kubwa zaidi.

Kwa hiyo, naamini linazungumzika, kwa sababu wamepewa mamlaka, wamepewa uwezo, basi mamlaka haya yasiwe nusunusu ili iwe mwarubaini wa kutatua matatizo ya Walimu ambayo kikubwa ilikuwa vyeo vyao na mishaharra yao. Kwa hiyo, naomba waendeleo kulitizama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana pia na namna ambavyo imeundwa Tume hii, Wajumbe wa Tume, pamoja na Mwenyekiti na mapendekezo ya Kamati yetu ya kudumu kuainisha kinagaubaga, sifa za Mwenyekiti na sifa za Wajumbe wa Tume ni muhimu kwa sababu tunataka kweli wale ambao wameboba katika Sekta hii ya Elimu, Sekta ya Utawala na Sekta ya Fedha, lakini angalau pia wameshiriki katika kuyajua matatizo ya Walimu kupitia fani yenyewe ya Ualimu. Kwa hiyo, naunga mkono sifa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Muswada huu umeainisha masuala ya uwezeshaji wa Tume hii. Tumeona Tume ya TSD ina changamoto kubwa ya uwezeshaji. TSD wapo, lakini Ofisi zao zimechoka sana, lakini kikubwa ni uwezeshaji.

Kwa hiyo, naiomba Serikali kama kweli imeainisha vizuri kifungu cha 19namna ya uwezeshaji wa Tume hii, fedha zitakazopatikana, uandaaji wa taarifa yao; basi hili kwakweli kama Bunge hili tukipitisha, lizingatiwe ili kweli tuzipe hadhi Ofisi za Wilaya za Tume ya Utumishi, Makao Makuu ya Tume, mambo yawe mazuri, wapewe hela zao kama inavyokusudiwa, wajengewe weledi watumishi na Wajumbe wa Tume ili basi yale matatizo ambayo yanawapata Walimu ambao kwa kiwango kikubwa ni nusu ya Watumishi wote wa Tanzania, yawe yamepata mwarobaini wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza, kwakuwa nimesimama mara ya mwisho ndani ya Bunge hili, naendelea kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Pwani kwa dhima waliyonipa. Naamini wengine pia walikuwa Walimu, tumeshirikiana vizuri.

Pia naamini pamoja na majukumu mengine ambayo Mheshimiwa Rais alinipa, namshukuru sana, sikuwaacha, nilikuwa nao pamoja, nimeshirikiana nao kwenye shughuli mbalimbali za wanawake, kwenye Mabaraza yetu ya UWT kuwasemea ndani ya Bunge.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awape wepesi katika shughuli zao na awabariki sana Walimu wote nchini Tanzania, hongereni na tunajivunia tunaposimama hapa kutokana na uwezo wenu mliotujengea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nawaomba wanawake wa Pwani, Mwenyezi Mungu akipenda awajalie wanipe fursa tena niwawakilishe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni zamu ya Mheshimiwa Mkanga na Mheshimiwa Abdul Marombwa na Mheshimiwa John Cheyo wajandae.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu mimi nikiwa Mwalimu, tena Mwalimu mzoefu kweli kweli; na matunda humu ndani machache tu mnayaona na mnayajua, mnayasikia pamoja na kwamba nasikitishwa, mengi yapo upande huu. Kule! Lakini basi ndiyo matokeo haya ya siasa, lakini wamo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii bila hata kubabaika kwa sababu chombo hiki ni muda mrefu tumekipigania, tumeshauri, tumeshawishi, hatimaye tunamshukuru Mungu kwamba chombo hiki kwakweli kinarejea. Ni kama cha zamani, lakini hiki naamini kinarejea kwa mabadiliko mazuri mazuri na hata tutakaporekebisha vipengele ni kule kuendelea kukiboresha chombo kama hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, enzi zangu za Ualimu tulikuwa na kitu kinaitwa *UTS*, hapa katikati kikaja hicho cha TB nini, lakini hii naona kama inakuja kama kama *UTS*. Tofauti yake kubwa ninayoiona, mambo ambavyo yapo ni yale yale kwamba chombo hiki kitaajiri, kitaadhibu, kitafanya, kitafanya, lakini naona bado kumbe pamoja na kazi ya kuajiri haijapewa nafasi ya kuwa mlipa mishahara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama wenzangu wanavyosema, mimi najjuliza, hivi mwajiri gani ambaye halipi mishahara? Sasa unapokuwa mwajiri halafu hulipi, ndio vipi? Inanichanganya kidogo, lakini naamini Serikali itaweza kunisaidia kwa sababu hata mimi hapa niliyemwajiri ndiye mimi ninayemlipa mishahara. Siwezi kumwajiri halafu nikasema, wewe huko nyumba hiyo, nilipie huyu! Hapana! Mnakubaliana ninyi unamlipa wewe! Kwa hiyo, hilo halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu walivyosema, nadhani tujipe nafasi ya kuliangalia kuwepo hili ili kwakweli tukamilishe chombo hiki kiwe *One Stop Centre exactly* kwa Walimu wote, hao wanaohusika wa Msingi na Sekondari. Hiyo itanisaidia sana. Kuliko huku halafu kule! Aah, mbona sasa bado ile ya kusema angalau ndiyo yeye, mbona tunaacha mapengo kidogo?

Hilo kama siyo leo, tuendeleo kulitafakari ili kweli chombo hiki kiweze kuwa na manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupewa nguvu ndiyo kabisa! Kiwezeshe kikamilifu kusudi Waheshimiwa Walimu sasa waweze kujiona wana nafasi nzuri kabisa kama wenzangu walivyosema. Jamani Walimu kazi zetu ni nzito! Nyuma huko tulishasema, ni wito! Kama Mwalimu hujajitoa sawasawa kwakweli unaweza ukalipeleka Taifa mrama!

Kwa hiyo, tutumie chombo hiki kwamba angalau terejeshe imani na nia na mipangilio yake ipo. Watapewa *inservice training*, sijui mambo gani! Yote haya yanamsaidia Mwalimu kumjenga na kuwa na hamu na kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki ndicho naambiwa kitashughulikia *welfare* ya Walimu hasa katika Halmashauri zetu. Nijikite hapo; na chombo hiki ndicho kitagawanya Walimu katika shule mbalimbali huko katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina ombi kwa Serikali; kwa Walimu wenye ulemavu wa *style* yoyote ile ambayo wanaweza kuajirika wakawa Walimu, naomba Walimu hawa wawekwe kwenye Shule zenye mazingira zinazowafaa kuwasaidia kufanya kazi vizuri, kinyume cha hapo ni tatizo! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wasioona wapewe vifaa vya kufundishia vikiwa na (kwao ni lazima) *braille machine* na *braille paper* zile, Mwalimu huyo siyo kwamba ajinunulie, hapana! Ni nyenzo ya kufundishia kwake hiyo. Serikali iwawezeshe kuwapa hizo mashine, karatasi zake, *tape recorders* zile na hata ile fimbo ya kutembelea afike darasani iwe *provided* na Serikali na *Commission* hii. Ndiyo maana nasema iwe ndiyo inalipa mishahara na marupurupu yote hapo. Watajua hawa watu wao wako wapi na wawezeshe namna gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wenye ulemavu naomba sana wawekwe kwenye shule zilizo karibu na Ofisi Kuu za huduma mbalimbali, siyo unamweka kijiji cha mbali huko ambako atahangaika kuja kuchukua mishahara, jamani ni tatizo! Kwa sababu katika hali ya kuwa na ulemavu anatumia pesa nyingi zaidi kujihudumia yeye kuliko hata mzima. Yeye itamlazimu aende kwa nauli nzuri na gari; labda pikipiki anaogopa ataangushwa. Sasa mambo kama haya yanawaongeza gharama; na hapa ndiyo nakwenda huko huko!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zile posho maalum sijui muhimu zile, jamani wafikirieni Walimu wenye ulemavu. Wana matumizi kama ambaye sio mlemavu. Lakini ili aweze kufanya kazi, anahitaji kutumia pesa nyingi na muda mwingi kuweza kufika mahali anakohitajika.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, Kamisheni hii pamoja na kazi nyingine, iangalie sana. Siyo kwamba wengine wasiangaliwe, lakini hawa Walimu wenye ulemavu wana mahitaji ya ziada muhimu. Kwa hiyo, nayo yawekwe katika fikra na yatendewe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi leo nimefarijika; kama siku ile Bunge letu Tukufu lilipopitisha sheria ya Watu wenye Ulemavu, ndiyo raha niliyonayo leo; kwamba kwa Walimu tayari tumekwishakamilika na nimekuwa mmojawapo wa kushiriki kupitisha sheria. Mimi ninaamini tutaipitisha tu! Ni nani hapa hamheshimu Mwalimu? Mbona wote tumetokana na kazi ya Mwalimu jamani kwa *level* mbalimbali? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria inapaswa tuiptishe kusudi Walimu wetu wajisikie raha, nami namshukuru Mungu kuwa mmojawapo ambaye nimeweza kuwemo *among us* katika kujadili na kupitisha sheria hii muhimu kwa Walimu nchini Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine tutayarekebisha, sheria siyo vitabu vya Mungu; tutakapona tumejigongagonga mambo hayaendi na wakati, Sheria itarekebisha ikae vizuri zaidi. Kwa hiyo, ni bora kupitisha halafu baadaye yale ambayo yatatokana na, ndiyo unaendelea kuyarekebisha. Lakini kusema tusipitisha, ooh, kwa sababu imekuja kwa dharura! Mheshimiwa Rais ameona hii sheria lazima tuipe kipaumbele kuipitisha katika Bunge hili, kusudi Agosti Mosi na kuendelea Walimu hawa wajisikie Waa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwa sababu ni mara yangu ya mwisho kwa kweli kusimama nikasemea kipaza sauti hiki kwa *term* hii, nawashukuru Walimu wenzangu wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuvumilia na sasa hivi wanaendelea. Kuna wakati walichoka kidogo, nadhani Serikali imeanza kuwaweka sawasawa; tunapasisha; na wote hawa ni kutokana na kazi zetu sisi Walimu tuliomo humu ndani na wote ambao wako nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wamama wa Morogoro kwa mara nyingine, nawashukuru wenye ulemavu na Vyama vyao; tumeshirikiana kusaidiana kupeana mawazo. Mliona hata kwenye Bunge Maalum la Katiba hapa, nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge mlionikubalia wakaingia 20 kwa kubadilisha kile kipengele. Mliona kazi zao, tuko pamoja; na Mungu *inshallah* tutaendelea kuwa pamoja. Nawashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote; mmenipenda, mmenilea, mmenishauri; kwa kweli najisikia kukubalika ndani humu, kabisa! Mlinipenda sana, kila mtu Magee! Magee! Mkanga! Mkanga!

Unapata faraja kwamba ulemavu siyo hoja, unao wenzako. Ahsanteni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja sana. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abdul Marombwa, ajiandae Mheshimiwa Cheyo, jiandae na Mheshimiwa Zainab Kawawa!

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kuniwezesha kukaa Bungeni hapa kwa muda wa kipindi cha miaka kumi kupitia wananchi wa Jimbo la Kibiti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kufanya kazi kwangu vizuri, hasa kupitia Serikali ya awamu ya nne, nimewaambia wenzangu wa Jimbo la Kibiti kwamba miaka kumi niliyofanya kazi inatosha. Kijiti hiki sasa tuwatafutie wengine waendeleo. Kwa hiyo, nawaaga Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba huenda tusikutane tena katika Bunge linalokuja, mwingine atakuja. (Makofi/Minong'ono)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia sheria hii iliyoletwa. Samahani sana, naona kuna minong'ono, kwa kweli sitagombea tena.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah! (Makofi/Kicheko)

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kama walivyosema wenzangu, Walimu tulikuwa tunatafuta, hivi sisi Walimu Mwajiri wetu ni nani? Ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, ni TSD, ni Wizara au ni nani? Lakini kutokana na sheria hii imetuweka vizuri sasa kwamba Mwajiri wetu atakuwa ni TSD.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende kifungu kwa kifungu. Ukiangalia Sehemu ile ya Pili, Kifungu cha (5), kinaelezea kazi za Tume hii ambayo itaundwa. Kwa kiasi kikubwa kazi zile mwanzoni zilikuwa zinafanywa na hiyo TSD lakini kulikuwa na kazi nyingine zilikuwa zinafanywa na Afisa Elimu wa Wilaya. Kwa mfano, ile sehemu (d) kazi ya Afisa Elimu wa Wilaya ilikuwa ni kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa Walimu ndani ya Serikali za Mitaa na shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili halikuwa suala la TSD lilikuwa ni suala la Afisa Elimu, naiomba Serikali make; wakati mnapoweka utaratibu mzuri wa utendaji kazi wa hii Tume, na hili nalo mlione: Je, tunapotoa kazi hii kule, huyu Afisa Elimu wa Wilaya naye mnampatia majukumu gani? Kwa sababu hapa mnamnyang'anya majukumu aliyokuwanayo, mnaipatia hii Tume. Hilo ni la kwanza.



Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, kwenye kazi za Tume katika ngazi ya Wilaya, kuna kazi nyingi pale ambazo zimeoneshwa kwenye ngazi ya Wilaya ambazo zitafanywa na Tume baada ya kuteuliwa na Tume Makao Makuu ndiyo watakaounda Tume za Wilaya hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kazi nyingi, lakini mimi ombi langu katika kazi zile ni kwamba, huyu atakayeteuliwa kuwa Katibu wa TSD wa Wilaya, yeye ana majukumu mengi sana kama yalivyodainishwa katika ile Ibara ya nyuma yake; lakini majukumu haya, huyu Katibu atakayeteuliwa, yeye ataingia na miongoni mwa kazi zake; “kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya kifungu hiki, Tume katika ngazi ya Wilaya itakuwa na vikao vya mara kwa mara vya mashauriano na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kwa lengo la kujadili masuala yanayohusu Walimu katika Wilaya husika na kutoa ushauri.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jukumu hili, naiomba Serikali, huyu Katibu Mtendaji wa Wilaya atakayeteuliwa kuongoza hiyo Tume katika ngazi ya Wilaya, basi yeye kwa vyovyote vile awe Mkuu wa Idara. Apewe mshahara kama wanavyopewa Wakuu wa Idara wengine, kwa sababu huyu sasa ana jukumu kubwa kama Afisa Utumishi katika ngazi hiyo ya Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Afisa Utumishi alikuwa na Watumishi 3,000, basi Watumishi 2,000 ambao ni Walimu wanatoka wanakuja kwenye ngazi hii ya kwake huyu, kwa hiyo, naye ni lazima awe Mkuu wa Idara. Kwa hiyo, mtakapokuwa mnaunda hii Tume na huyu ni lazima mumfikirie hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni hii TSD, Makatibu wake walikuwa wanapandishwa cheo bila mshahara. Anakuwa Katibu wa TSD wa Wilaya, anakuwa Katibu wa TSD wa Mkoa, anaondoka na mshahara wake ule ule wa Ualimu. Lakini kwa mwongozo huu uliokuwepo; na kwa kuwa anafanya kazi kubwa sana sasa hivi katika ngazi ya Wilaya, Katibu wa TSD kwa vyovyote vile ni lazima awe Mkuu wa Idara ili aweze kufanya kazi zake vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hawa Watendaji wengine ambao watateuliwa kuunda hii Tume katika ngazi ya Wilaya. Hii ni *promotion*! Huyu mtu unampandisha cheo sasa. Unapompandisha cheo, hawa Wasaidizi wake ambao naamini watakuwa ni Walimu, nao pia wafikiriwe katika suala hili la mishahara.

Asiende tu pale moja kwa moja kwa kupitia mshahara wake anaoupata wa Ualimu; lakini pia huyu aende akipandishwa cheo, basi upandishwaji wa cheo uende sambamba na upandishaji wa mshahara ili waweze kuwahudumia vizuri zaidi hawa Walimu. (Makofi)

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa nimalizie tu kwamba Walimu wetu kwa muda mrefu wamepata matatizo makubwa sana ya mishahara yao, wamepata matatizo makubwa sana ya uhamisho wao; na kama alivyosema Mwalimu mwenzangu pale kwamba uhamisho wa Walimu ni adhabu! Sasa hivi Mwalimu anaweza kufanya kazi katika kila Wilaya kwa sababu Mwajiri ni Mkurugenzi Mtendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya inapanga masharti yake, kwamba Mwalimu ukija katika Wilaya yangu, basi huwezi kuondoka mpaka ufanye kazi kwa muda wa miaka mitano.

Sasa masharti haya nawaambia Walimu wenzangu kwamba sasa yanaondoka. Mwenye mamlaka sasa hivi ni TSD. (Makofi)

Nawaombeni Walimu tuunge mkono kabisa Muswada huu kwamba ile adhabu tuliyokuwa tunaipata, Mwalimu unakaa miaka 10 au 15, ukiomba ni lazima upitie kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na wakati mwingine Mkurugenzi hataki kukuhamisha; basi kupitia Muswada huu, utakuwa umetoa kero kubwa sana kwa Walimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kipengele cha mwisho kuhusu ukataji wa rufaa. Kutokana na kile kipengele cha 13; Kifungu cha 13 kinaelezea utaratibu wa kukata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile Tume muundo wake upo kwenye ngazi ya Taifa na ngazi ya Wilaya. Ngazi ya Mkoa, hakuna. Mwalimu amefanya makosa kwenye ngazi ya Shule ya Msingi; Mwalimu Mkuu akamrekebisha yale makosa yake. Kama Mwalimu hakuridhika na marekebisho hayo, anakata rufaa kwenye ngazi ya Wilaya. Kuna hii Tume kwenye ngazi ya Wilaya ndiyo inayotoa hukumu sasa kwamba hukumu ni hii. Akishamaliza pale, yule Mwalimu kama hakuridhika na ile hukumu, anakata rufaa. Rufaa hii sasa inakatwa moja kwa moja Taifani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli Taifa limejiandaa kupokea rufaa za Walimu wanaokaribia 200,000 wa nchi yetu hii? Kwa sababu makosa ya binadamu yanafanana. Sisi sote kwamba rufaa yetu iende sehemu moja tu ambayo ni Taifani, kama unakata rufaa ile ya mwisho; nafikiri mapendekezo yaliyokuwa yametolewa na Kamati ni ya muhimu, lakini kubwa zaidi ni lazima tuweke chombo imara sana chenye haki cha kuhakikisha kwamba yale mambo ambayo Mwalimu ameyapeleka kwenye ile Tume kama kukata rufaa yake, yamalizike katika ngazi ya Wilaya vizuri; au yakipelekwa kule Taifani yasiwe na marekebisho makubwa. Lakini ngazi ya Wilaya ipewe majukumu makubwa sana ya kuhakikisha kwamba kusiwe na makosa tena ya kukatiwa rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi turekebishe katika ngazi ya Wilaya kwa sababu Mkoani hawana kazi. Mkoa unafanya kazi gani? Kuiondoa Mkoa ni sahihi tu, lakini ngazi ya Wilaya ni lazima tuweke muundo mzuri, watu wazuri ambao watahakikisha kwamba Mwalimu ataridhika na yale maamuzi yatakayotolewa na ile Kamati ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa John Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Aidha, natumia nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa sisi wote uzima tuweze kujadili jambo muhimu kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi nimekaa hapa na huku hakuna watu; na wananchi ambao wananisikiliza wanataka kujua kwanini mimi niko hapa na sikuweza kwenda na upepo ambao umepita katika Bunge hili? Kwa hiyo, nataka kutumia nafasi hii kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hakuna mtu ambaye anaruhusiwa katika nchi hii kuzia muhimili wowote kufanya kazi yake. Huwezi ukaenda Ikulu ukasimama pale katikati ukasema Mheshimiwa Rais leo haingii Ikulu au hafanyi kazi yake; hutabaki! Huwezi kuingia Mahakamani ukawaambia Mahakama leo imefungwa, unapiga kelele; hautabaki! Hivyo hivyo huwezi ukasimama katika Bunge hili ukasema Bunge hili lisiweze kufanya kazi yake; jambo hili haliwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nawaambia watu wa Itilima, nipo hapa kukisimamia Kiti chenu mlitchonipa; na mwaka unaokuja huu, narudi tena, nitawaomba kiti hiki niendeleo nacho. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada uliopo mbele yetu unazungumzia juu ya watu muhimu sana; Walimu. Mimi nasimama hapa kwa sababu nilifundishwa na Mwalimu. Kila mmoja wetu aliyepita shule amekutana na Mwalimu. Kwa hiyo, ni vizuri tumeweza angalau kuleta kitu ambacho kitawalea Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kusema, la kwanza, kama kuna watu ambao ni lazima tuwasifu na tuwape hongera sana ni Walimu wa Tanzania. Mimi mwaka huu kama kuna kazi nzuri Serikali imefanya ni kuweza kutuletea Walimu wengi katika Wilaya yetu ya Itilima. Walimu wa *Secondary School* tuliwapata ni zaidi ya 400; Walimu wa *Primary School*, ndiyo hivyo, ni lukuki. Lakini kila mafanikio yana matatizo yake.

Tatizo kubwa tulilonalo, kweli tumefundisha Walimu, kweli tumepata Walimu, lakini hatujatengeneza miundombinu ya kuweza kuwahifadhi Walimu wetu. Hiyo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe una Wilaya mpya kama Itilima, unapata Walimu 400 wa *Secondary School*, hakuna Mji, hakuna nyumba ya kupanga, hawa watu unawapeleka wapi? Unawapeleka Walimu hata mishahara; nazungumza juu ya mishahara ya Walimu wangu waliokuja Itilima, leo ni mwezi wa Pili hawajapata mishahara yao. Watu hawa wanafanya kazi kwa njia gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tume hii ndiyo jawabu, basi naunga mkono moja kwa moja pawepo na Tume hii ili iweze ikatusaidia katika kutatua matatizo mbalimbali ambayo yanawahusu Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, nimesoma Muswada, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri; na nimemsikiliza Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ambaye amefanya kazi nzuri sana; ukweli ni kwamba kutunga sheria hii ndiyo mwanzo tu wa kutatua matatizo. Bado kuna mambo mengi ambayo ni lazima yaelezwe vizuri. Nafasi ya Halmashauri iko wapi na itafanya kazi gani? Nafasi ya Waziri wa Elimu iko wapi na atafanya nini? Nafasi ya Waziri ambaye ametajwa ambaye ni Waziri Mkuu, yeye anahusiana namna gani? Kwa vyovyote vile, nafikiri ni vizuri yale yaliyosemwa na Kamati yakawekewa umuhimu. Mkae mzungumze ni namna gani mnatatua baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho nimemsikia Mwenyekiti akizungumza ni kwamba Tume ipate nafasi ya kulipa mishahara. Nawaomba tusiende mpaka tufike mahali pa kuwaaminisha Walimu kwamba wao sio Watumishi wa Serikali. Hawa Walimu ni Watumishi wa Serikali na Serikali ni lazima iwe na jukumu la kuwaangalia na kuhakikisha hawa Walimu wanapata mafao yao kama Mtumishi mwingine anavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ni nyenzo tu ya kuhakikisha wanapata mafao yao kwa urahisi zaidi kuliko ilivyotokea. Tusipoweka hili sawa tutapata matatizo ya nidhamu, tusipoweka jambo hili sawa tutapata matatizo ya kibajeti, tusipoweka jambo hili sawa tutashindwa kujua mlolongo wa uajiri uko namna gani. Kwa hiyo, nawashauri kwamba tumetunga Sheria na vizuri tumetunga Sheria, lakini uwe tu ndiyo mwanzo wa kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Jimbo langu, nawaambia na bado kwa kuwa labda hii ndiyo mara ya mwisho kuzungumza, baadhi yetu hapa kwa leo, lakini Mungu atusaidie tutarudi na nawatakia wote

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanaogombea turudi hapa pamoja na Marais wanaogombea waje hapa tuanze awamu nyingine ambayo inategemewa sana na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kusema katika vitu ambavyo bado Bunge hili halijafanya, bado hatujawaangalia wakulima wetu vizuri zaidi, bado hatujaangalia wafugaji wetu vizuri zaidi. Naomba tunakokwenda mbele ya safari, agenda ambazo ziwekewe umuhimu katika Bunge hili, huduma za jamii. Leo tumezungumza elimu, afya, maji, umeme vijijini na ndiyo maana nawalaumu ndugu zangu, kila wakati ambavyo tumezungumza jambo zuri katika Bunge hili, tumezungumza juu ya Katiba wao wamekimbia, tumezungumza kila bajeti tunataka kupeleka umeme vijijini, maji vijijini, elimu, wao wanakimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tumezungumza juu ya kuhakikisha pesa yetu ya gesi inaonekana mikataba yote inawekwa wazi kwa watu wote kuangalia, pesa ile inawekwa kwenye Mfuko maalum, hivi ni vitu ambavyo tulikuwa tunadai miaka yote, wao wanakimbia. Sasa ni kitu gani basi ambacho kimetuleta kwenye Bunge hili kama siyo kutunga sheria ambazo zitasaidia Watanzania kuondokana na lindi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wote wale ambao wanauwania Urais na mmeanza kufikiria kama vile nilivyoanza kufikiria mwanzoni nilipoingia kwenye siasa, tusiendeleo kujiita sisi maskini, maskini, ni sawasawa kama wewe una mtoto unamwambia wewe ni mjinga, ni mjinga, atakuwa kweli mjinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu sasa kwa awamu inayokuja tuwaeleze wananchi wetu kwamba nchi yetu ina rasilimali lukuki na tutatengeneza mazingira ya watu kutengeneza mapesa kibao. Hiyo ndiyo njia ya kuweza kutengeneza Taifa linalojitegemea, lakini Taifa la kuendelea kuimba wimbo mimi maskini, mimi maskini, la kuendelea kuwa omba omba, la kuendelea kudai usiwe mtu wa kujitegemea, hiyo siyo awamu ambayo inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini uchumi wa gesi ambao wote tunatumaini sasa, utatuwezesha kupaa Tanzania na tuna uwezo wa kupaa kama tu tutahakikisha, kama tunaendesha mambo ya siasa tujue. Maana ya demokrasia wachache kila wakati wasikilizwe na wapewe nafasi ya kusikilizwa, lakini wengi ni lazima ndiyo wataamua, ndiyo maana ya demokrasia. Basi tutumie Bunge linalokuja kwa uwingi wowote utakaokuja ili kuhakikisha wengi tunawasaidia kuhakikisha wanatengeneza pesa, wanatengeneza maisha yao na njia ya kutengeneza maisha yao tutumie rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu ili kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo wosia ambao nataka kuacha kwa Bunge hili. Nawataki kila la kheri, asanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa pengine leo ndiyo mara yangu ya mwisho kuzungumza hapa Bungeni, napenda kutumia nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa na kwa namna ya pekee kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa fursa ya kuwa Mbunge wa Viti Maalum niliyekuwa nikiwakilisha Vyama vya Wafanyakazi nchini. Fursa hii imenipa uzoefu wa kutosha, imenipa uzoefu mkubwa sana, nimejifunza mambo mengi na pale ambapo nilijikwaa, basi nawaomba Watanzania na Waheshimiwa wenzangu tusameheane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ku-reestablish hii Tume ya Walimu. Tunairejesha Tume ya Walimu kwa dhana ya kwamba katika Taifa letu ambalo Serikali ndiyo mwajiri mkubwa kazi ya Ualimu kwa sasa ndiyo kivutio kikubwa kwenye soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunairejesha Tume ya Walimu kwa dhana ya kwamba tunaleta njia bora zaidi itakayotatua mahitaji na kero za Walimu za kuifanya taaluma hii ya Ualimu iwe kivutio. Naunga mkono Muswada huu ingawa yako maeneo mawili ambayo ningependa Serikali iyatazame kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye Muswada huu kifungu cha 12, kinaeleza kazi za *Commission* katika ngazi ya Wilaya yaani majukumu ya Tume katika ngazi ya Wilaya inasomeka hivi: *“In performing functions conferred by this Act each District office shall*

*(a) keep and maintain an updated register of all teachers under its jurisdiction who are employed in the public service;*

*(b) keep and maintain an updated seniority list for all teachers under their jurisdiction;*

*(c) Ensure that teachers appointed in the service fill and sign agreement forms before reporting to their respective stations;*

*(d) Recommend to the Commission for approval of reappointment of teachers formally terminated from the services provided that such a teacher shall have been out of service for a period not less than twelve month and ...”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiangalia pia katika kifungu cha 14, kinaelezea *supervision na administration of welfare of teachers*. Wanasema

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

*Supervision and administration of the welfare of the primary and secondary school teachers shall be the responsibility of the Local Government Authority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunarudi tena kwenye hoja yetu ya mwanzo ambayo Kamati imeieleza kwamba, kero iliyopo kwa Walimu wanakosa *a one stop center*. Leo Mwalimu anakwenda kuhudumiwa chini ya *Local Authority*, kesho anakwenda kuhudumiwa chini ya *TSD*, sasa lipi ni lipi? Tunaleta mkanganyiko usiokuwa na ulazima. Nilidhani kwamba leo tunaleta suluhisho kwa kuifanya hii Tume iwe chini ya Wizara ya Elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanapata matatizo hata kwenye mafao, mnawachaganya mara leo alipwe na *PSPF*, mara leo alipwe na *GEPP*, yote haya ni kwa sababu ya *contradiction* iliyopo hapa. Sasa ni lini tutaiondoa hii *contradiction* na ni kwa vipi? Nasema hii hatua tuliyoipiga leo ni kubwa kwamba tumeirejesha Tume, lakini nilitegemea hii Tume ifanye kazi *per se* kwa Walimu na isiwe chini tena ya *Local Authority*. Naomba hivi vifungu viangaliwe vizuri ili tuweze kutatua kama kweli tuna dhamira ya dhati ya kutatua kero za Walimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ni kwamba, tumeona hapa kazi ya Tume ni kuajiri, kuwa-*discipline* Walimu, kwa maana hiyo *of course* itakuwa ina kazi ya kuweka *data* vizuri za Walimu jambo ambalo ni zuri tu kwamba sasa tunategemea kuona kunakuwa na kada mbalimbali zinazotambulika. *Professionally* kila Mwalimu anayo taaluma yake kuna Walimu ambao wana uwezo wa kufundisha viziwi, kuna Walimu ambao wana uwezo wa kufundisha historia na kadhalika. Kwa hiyo nina uhakika kwamba sasa tumepata suluhisho la kuwa na *database* ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *functions* zilizotajwa hapa mimi ni mwanataaluma wa *HumanResources Management*, ziko kwenye taaluma hiyo. Unapokuwa mwajiri unaajiri, unam-*train* mfanyakazi, unampa likizo mfanyakazi, unampa stahiki zake mfanyakazi ikiwemo mshahara, ikiwemo mafao yake ya kustaafu wewe ndiyo msimamizi wa hayo masuala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasikitika na nashangaa kuona kwamba hii Tume inafanya kazi chache inaacha ile kazi ya muhimu, ya stahiki za mfanyakazi, kwa nini tusiipe Tume *mandate*, mamlaka ya kuwa inamlipa Mwalimu, lakini pia ningepomba suala la kusimamia mafao ya Walimu na yenyewe pia yaingizwe kwenye *functions* za hii Tume ili iweze kuwa Tume inayoielewika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa ni hayo na naomba Serikali iyapatie majawabu. Ahsante. (Makofi)

**MHE. HAMIS A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini zaidi nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kwa mara nyingine tena kusimama hapa Bungeni siku hii ya leo. Mungu akijalia pengine nitakuja kusimama mahali pengine ndani ya Bunge hili miezi michache ijayo, la kama asipojalilia sijui nitakwenda wapi Mungu anajua. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwenye Muswada huu kwa sababu ya umuhimu wa Walimu kwenye Taifa lakini pia uzoefu wangu wa kufanya kazi kama Mbunge kwenye Jimbo, nimepokea malalamiko mengi sana kutoka kwa Walimu, kila siku nimekuwa nikiwasumbua Mawaziri na Manaibu Waziri kwenye eneo hili. Kaka yangu Mheshimiwa Majaliwa ni shahidi, nakuja na makabrasha ya kutosha kutoka Jimboni kulalamikia mambo haya haya ambayo leo hii tunajaribu kutunga Sheria ambayo itayapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika muktadha huo, napenda kusema jambo moja tu kwa sababu nina dakika tano na hili ni mamlaka ya kuajiri na kulipa mshahara, kwamba kama unamtuma mtu aende akakujengee nyumba, maana yake wewe ndiyo mwajiri wake na wewe ndiye utamlipa ujira wake na kama usiporidhika na kazi wewe ndiye utakayemnyima ujira wake, ama utamwambia arekebishe, ama utampa kila aina ya adhabu kadiri utakavyoona kwa sababu wewe ndiye mwajiri. Litakuwa ni jambo la ajabu wewe ukatoe ajira ya mtu kukujengea ukuta wako, halafu umwambie akalipwe na mtu mwingine wakati yeye anakujengea wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni lazima tuyachukue mamlaka yote yaku-*hire* na ku-*fire* na kuyaweka kwenye chombo kimoja. Hilo ni jambo la msingi ambalo lazima tukubaliane *this is an issue of principle* kwamba lazima anayeajiri na ndiyo huyo huyo afukuze, ndiyo huyo huyo aadabishe, ndiyo huyo huyo atoe motisha tukifanya hivyo tutaondoa *frustration* ambayo imekuwa ikiwakumba Walimu wetu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Sheria hii nikisoma kile kifungu cha tano, naona kuna mamlaka mengine hayapo na hapa pia nimewasilisha jedwali la marekebisho kutaka kuongeza baadhi ya vifungu kimojawapo ni hiki cha kuajiri, ningependelea kile kifungu cha 5(c) kiongezewe uzito zaidi kimaanishe kwamba chombo hiki ndicho kitakachoajiri na ndiyo hicho hicho kitakachofukuza watumishi ili Walimu wajue kwamba wao mwajiri wao ni nani na nani anayewajibika kuwalipa mishahara na mwisho wa siku wajue wanakwenda kudai wapi haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napendelea tuongeze kifungu kingine na hiki kinahusu motisha kwa Walimu. Ni lazima tuweke mazingira ya kuwapa motisha Walimu kwa sababu haitoshi tu kumlipa Mwalimu mshahara wake.



Frederick Herzberg anasema mshahara ni *hygiene factor*, haisababisha Mwalimu asiridhike, haisababishi mtumishi yeyote yule wa umma ama mtumishi yeyote yule asiridhike, kwa sababu anajua mshahara wake atapata tu mwisho wa mwezi, hivyo hata upandishe mshahara namna gani hata siku moja haiwezi kumpa motisha mtumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengine kama mazingira ya kazi, kuna mambo kama taaluma uwezo wa kujiendeleza akiwa kazini, kuna mambo kama posho za mazingira magumu, mambo kama posho ya kufundisha masomo maalum labda masomo ya sayansi, ama masomo ya hisabati, masomo ya historia, kadiri ambavyo kama tutaipa mamlaka Tume itaamua kadiri wakati utakavyoruhusu na kadiri tutakapokuwa na uwezo wa kuwapa motisha Walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napendelea tuongeze kifungu kingine hapa ambacho kinaweka wazi mamlaka ya kutoa motisha, kutengeneza mpango wa motisha, lakini pia kutengeneza mpango wa *retention* ya Walimu kwenye maeneo ambayo yako *remote*, yako mbali na *center*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mwalimu anayefundisha shule ya msingi Dodoma Mjini hapaswi kupata marupurupu sawa na Mwalimu anayefundisha shule iliyopo kule Kibakwe, kwa kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, kule ni ndani zaidi hata mitandao ya simu utakuta hakuna, hata mitandao ya umeme utakuta hakuna, lakini mwalimu yule anayekaa kule analipwa sawa na Mwalimu anayekaa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta Mwalimu wa kule hata nyumba ya kuishi hakuna, hata akisema anataka kupanga hakuna mahali pa kwenda kupanga, lakini analipwa sawa na Mwalimu anayefundisha hapa Dodoma Mjini ambaye ana *access* ya mitandao ya simu, mitandao ya *internet* na mwisho wa siku Mwalimu wa hapa hata akitaka kupanga nyumba nzuri ya namna gani ataweza kupanga. Hivyo ninachokizungumzia ni kwamba, ni lazima mamlaka ya kutoa motisha yawekwe wazi kwenye Sheria hii ili Walimu waone tunawajali na lakini pia tunawasemea, lakini pia tunawapenda Walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye Muswada huu muhimu sana, sheria hii muhimu sana kwa ajili ya Walimu nchini. Kwa kweli Sheria hii imechelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, naamini leo ni siku yangu ya mwisho kuongea hapa kwenye Bunge hili la Kumi. Niwashukuru sana wananchi wa Kigoma kwa heshima waliyonipa kwa miaka hii kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanza Jimbo letu lilikuwa Upinzani, tulifanya kazi ya kuondoa Upinzani na tumefanya mambo mengi sana, ukienda leo Kigoma siyo Kigoma ya mwaka 2005. Naamini tutaendeleza kwenda kuondoa Upinzani kote katika Mkoa wetu na kazi hii naiweza, nimeshaifanya na nitasimamia kufanya kazi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ni nzuri sana, lazima tuhangaike na mishahara ya Walimu, stahiki zao, mafao, mazingira bora ya kazi, lakini nataka twende mbali kidogo, kama Taifa ili tuendeleo tunawahitaji sana Walimu na elimu ndiyo itakayotutoa hapa tulipo leo. Hatuwezi kwenda kwenye kasi kubwa ya maendeleo ya uchumi bila elimu, hata kama Mungu ametujalia kila aina ya rasilimali, lakini kama tuna tatizo kwenye elimu hatuwezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Korea Kusini ili uwe Mwalimu lazima uwe umepata maksi za juu kuliko wengine wote. Ukienda Singapore ili uwe Mwalimu lazima uwe mtu ambaye umepata *first class* na nchi kama hizi na ndiyo maana wamepiga hatua kubwa kwenye maendeleo hasa ya elimu. Nadhani umefika sasa wakati haiwezekani Walimu wawe ni wale ambao hawakufanya vizuri sana, nadhani umefika wakati wale wa *division one* hawa ndiyo wawe watu wa kwanza kwa kwenda kufanya kazi ya ualimu. Tukifanya hivyo kama Taifa na huku tunaendeleza kuweka mishahara mikubwa na tuweke mishahara mikubwa ili kazi hii ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika alitupeleka Malaysia na Singapore, wakatuambia wakati wameanza Singapore kuna kada mbili zilikuwa zinalipwa mishahara mikubwa kuliko kada yoyote na walikopa mpaka *World Bank* kwa ajili ya kulipa mishahara. Kwanza ilikuwa ni Walimu na Polisi, ndiyo ilikuwa kada inalipwa mishahara mkubwa kuliko mtu yeyote ilikuwa ni ualimu, ya pili Polisi. Maana yake nini, kwamba Walimu ndiyo kitovu cha maendeleo yetu, Walimu ndiyo watabadilisha maisha yetu ya vijijini na mijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili Walimu hawa ndiyo maana wakasema, anayekwenda kufanya kazi ya ualimu, lazima awe ni yule kijana ambaye amefanya vizuri sana darasani na ndiyo maana na ukweli ikawa kazi ambayo kila mtu anaikimbilia kwa sababu ndiyo kazi inayolipa kuliko kazi yoyote. Naamini na sisi kama nchi imefika wakati Waziri wa Elimu tuanze kufikiri haiwezekani ualimu waende wale ambao hawakufanya vizuri. (Makofi)

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja wakati mnafikiria kuboresha maslahi yao, kuboresha mishahara yao na kwa kweli jamani Walimu wetu wanaishi mazingira magumu sana, chombo hii ni muhimu kitusaidie ili kibadilisha maisha ya Walimu wetu hasa walioko vijijini. Hata kwenda kupata mishahara inakuwa ni kadhia haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa nadhani umefika wakati tuanzishe chombo hiki kije kitatue matatizo, tusije tukaanzisha chombo hiki bado tunarudia mambo yale yale. Maana sisi ni wazuri kwenye kutunga sheria, tuna sheria nyingi nzuri sana, lakini utekelezaji wake una matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba, sasa umefika wakati tumeleta chombo hiki ambacho Walimu wamekililia miaka mingi, chombo hiki tukipe nguvu, chombo hiki tukipe mamlaka, chombo hiki tukipe *resources* kwa maana ya rasilimali fedha ili kiweze kufanya kazi ya kuboresha maslahi ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimalize kwa kukushukuru sana. Nimshukuru Waziri kwa kuleta sheria hii, hata kama imechelewa, naamini ni sheria nzuri, itasaidia kutatua matatizo Walimu hasa walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge saa sita na nusu tutawapa Mawaziri watatu kuchangia na jioni tukifika saa kumi tutaendelea na Waziri anayehusika. Sasa namwita Mheshimiwa Profesa Mwandosya mpaka saa sita na nusu.

**MHE. PROF. JAMES M. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kusema naunga mkono hoja hii muhimu sana, imekuja kwa wakati na kwa kweli ni mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma kwa Walimu na kwa maana hiyo kuendeleza ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wamehangaika sana, wamehamishwa hapa na pale, sasa tunarudi katika chombo kimoja ambacho kitaangalia maslahi yao, kitaangalia utendaji wao na vile vile kitarekebisha masuala mengi ambayo Walimu walikuwa wanauliza. Kwa hiyo, ni wakati mzuri na inaonesha pia kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi kinajali Walimu. Hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja hapa kuhusu mishahara. Niseme tu kwamba, mishahara ya Serikali inalipwa kwa kweli na Serikali, ni taratibu tu ambazo huwa tunaziweka ambazo tunataka kuboresha au kuleta ufanisi katika kutoa mishahara, lakini mishahara yote inatokana na Serikali na fedha zote zinaidhinishwa hapa Bungeni, kwa hiyo, hili suala lisiwape shida hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo baada ya kuanzisha hiki chombo itaonekana kwamba kuna umuhimu wa kuwa na mfumo bora zaidi wa kujenga, wa kufanisha hili suala la mishahara, basi kutumia kanuni ambazo Waziri mhusika amepewa katika sheria hii, basi hilo litafanyika. Jambo kubwa ni kwamba Tume sasa inaundwa hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, hii ni mara yangu ya mwisho kuzungumza katika Bunge lako hili Tukufu kwa sababu tayari nimeshaaga huko Rungwe Mashariki kwamba baada ya vipindi vitatu vya kuwa Mbunge na kupitishwa bila kupingwa labda umefika wakati mzuri tu wa kufanya mambo mengine muhimu mambo mengine kwa ajili ya Taifa hili. Kwa hiyo, hii ni mara yangu ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida unapozungumza ikiwa ni mara yako ambao wengi wanasema *valedictory*, basi kuna mambo muhimu ambayo nimejifunza katika kipindi hiki cha kuwa Mbunge katika miaka kumi na tano ambayo ningependa kugawana au kutoa kama sisemi kama wosia, lakini kama ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

La kwanza ni kwa sisi Mawaziri; kwa kweli nimejifunza sana kwa kuwa Mbunge hapa na kuwa Waziri na nimeona umuhimu mkubwa sana wa sisi Mawaziri kuwa wasikivu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wanapotaka maelezo, ufafanuzi na masuala yanayowagusa wananchi. Hili nimeona ni muhimu sana na linajenga uhusiano mzuri sana kati ya sisi Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba ili kutekeleza hili nililolisema, basi ni muhimu sana kwa sisi Mawaziri kuhudhuria vikao vya Bunge, unaweza ukakaa ofisini ukasema nikaangalie televisheni, lakini kumwona Mbunge akiwasilisha hapa na kumwangalia na jinsi anavyowasilisha, unajifunza zaidi kuliko kusoma katika magazeti na vinginevyo. Kwa hiyo, natoa ushauri tu kwa wale ambao watakuwa Waheshimiwa Mawaziri hapo baadaye, kwamba viko vya Bunge ni vikao muhimu sana, sana, naomba sana wahudhurie. *(Makofi)*

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna vikao vya caucus ambavyo ni vikao muhimu sana ambavyo lazima Waheshimiwa Mawaziri tuwe tunahudhuria. Halafu kuwepo kwa Upinzani hapa Bungeni kumekuza sana uwanda wa demokrasia. Hili ni muhimu sana, Bunge la kwanza, Bunge la Kumi, Bunge la Tisa, Bunge la Nane kwa kweli unaweza kusema kwamba Upinzani ulikuwa ni Upinzani hasa, sijui imekuja kama vile katika Bunge hili ni kama vile shetani amepita mambo yamebadilika au labda ni wakati umebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kweli demokrasia haina maana kupingana kila kitu, ina maana kwa kweli kujenga hoja ambazo zitamsaidia mwananchi, ziwe zinatoka Upinzani na au ziwe zinatoka upande huu wa Serikali. Maana yake ni kwamba kama Serikali inaona kuna jambo nzuri lile linalotolewa na Upinzani, hata usijali jinsi inavyotokea lakini ni kulichukua na kulifanyia kazi. Vile vile kwa upande wa Upinzani si kila kitu ambacho hoja inatolewa na Serikali lazima ipingwe, huo siyo Upinzani, huo siyo Upinzani bora hata kidogo wala haina maana hiyo kwamba ni demokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwa haraka haraka ni suala la mgongano wa fikira. Mgongano wa fikira ni bora, unaleta fikira iliyo bora zaidi, lakini unakuwa mgongano mzuri pale ambapo hoja zinatolewa kwa kistaarabu, zinatolewa bila jazba, zinatolewa kwa staha na vile vile kuheshimiana. Hili ni jambo muhimu sana katika kujenga ushirikiano na vile vile kujenga heshima ya Bunge letu Tukufu, kufuata kanuni, taratibu na sheria na kuziheshimu hizo kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mmoja ambao ningependa kushauri ujio wa Rais katika Bunge au Mkuu wa Nchi popote pale duniani ni siku muhimu sana katika ratiba ya Bunge na vile vile katika ratiba ya Taifa. Sasa matukio ya kuondoka au kutoka wakati Rais anahutubia Bunge au kutohudhuria kwa makusudi vikao vya mkutano wa namna hiyo, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashauri kwamba iwe lazima katika kanuni kwamba siku hiyo muhimu kwa Taifa, kila Mbunge ahudhurie isipokuwa pale alipo na udhuru maalum. Labda tuliweke hili katika kanuni kwa sababu hii siku ni muhimu sana na tumejionea hapa ambapo Rais wetu amedhalilishwa na sisi kwa kweli wananchi wamedhalilishwa kwa Rais wao, anakuja hapa na watu wanaondoka Bungeni. Duniani haifanyiki hata siku moja, hiyo ni siku moja ambapo Wabunge wote wanaiheshimu na wanakuwa kitu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niishie kwa shukrani tu; nisingeweza kuwa Mbunge kama Chama cha Mapinduzi kisingeniteua kugombea Ubunge.

Kwa hiyo, shukrani zangu kubwa sana ni kwa Chama cha Mapinduzi, kupita mara tatu bila kupingwa ni kutokana na Chama cha Mapinduzi kuiteua halafu wananchi wa Rungwe Mashariki kunichagua. Kwa hiyo, shukrani zangu ni kwa chama kwanza. Halafu pili vile vile kwa wananchi wa Rungwe Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini shukrani zangu vile vile ni kwa hayati Baba wa Taifa ambaye aliniteua kuwa Kamishna wa Kwanza wa Masuala ya Petroli nchini. Mzee Mwinyi kuiteua kuwa Katibu Mkuu Viwanda na Biashara, Maji, Nishati na Madini. Mzee Mkapa kuiteua kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Rais Kikwete kuiteua kuwa Waziri mhusika na masuala ya mazingira, baadaye maji na umwagiliaji na baadaye maji na sasa kama Waziri kama mshauri wake katika ofisi ya Rais, Kazi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Mheshimiwa Spika, Wenyeviti, Mawaziri, lakini sana sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli katika miaka yangu kumi na tano hamna kitu kikubwa sana ambacho sijajifunza kutoka kwa Wabunge, kila wakati imekuwa shule kwangu, nimeelimika zaidi kuliko ambavyo nilivyoingia humu Bungeni, naacha Ubunge au nahitimisha Ubunge wangu kwa sababu ya elimu niliyoipata kutokana na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli inawezekana nimewakosea Waheshimiwa Wabunge katika kipindi changu cha miaka 15 ya kuwa Mbunge mwenzenu au kuwa Waziri, mimi ni binadamu, kwa hiyo, mniwie radhi lakini sikufanya hivyo kwa makusudi lakini kama nilivyosema kwa sababu ni binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakiane heri, nawatakia heri wote mrudi tena wale ambao mtarudi hapa, wananchi wameona kazi kubwa mliyofanya nadhani mtarudi sina wasiwasi. Bila shaka name mtanitakia heri kwa yale ambayo natarajia kuyafanya baada ya hili Bunge, lakini yote haya tumwachie Mwenyezi Mungu lakini Mwenyezi Mungu hufanya maajabu yake kupitia waja wake na waja wake ndiyo nyie na nyie ndiyo mtakaoamua, hivyo nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Majaliwa dakika kumi, Mheshimiwa Celina utafuatia kwa dakika kumi na Mheshimiwa Anne Kilango dakika kumi!

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya mwisho ya kuchangia kwenye jambo hili muhimu sana ambalo pia hata mimi mwenyewe ni mdau mkubwa kwa sababu mimi ni Mwalimu, lakini pia nilipewa dhamana ya kushughulikia jambo hili.

## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana pia sitapata nafasi nyingine ya kuchangia, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Walimu wote nchini ambao walinipa ushirikiano katika kipindi hiki cha miaka mitano nikiwa nafanya kazi ya uratibu kuwasikiliza na kuweza kuandaa mambo mema yanayoweza kuboresha sekta ya elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakati wote mlipokuwa mnataka ufafanuzi mbalimbali, tumeendelea kushirikiana kwamba majibu ambayo tulikuwa tunayatoa ili kuweza kufanya kazi pamoja kule ambako mlipo kwa kuwasemea Walimu, lakini pia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii pia niwashukuru sana wana Ruangwa walioweza kuniwezesha kufika hapa, lakini nitumie nafasi hii kuwashukuru wana Ruangwa kwa uvumilivu wao mkubwa waliouonesha katika kipindi hiki cha miaka mitano, nikiwa naendelea kufanya kazi za Walimu wakiwemo Walimu walioko pale Wilayani Ruangwa kwa kusimamia mambo yao, lakini pia kufanya ufuatiliaji kwa kupokea hoja zao na kuzifikisha Serikalini na jambo ambalo leo tunalo la kupitisha Muswada huu ambao Waheshimiwa Wabunge wameridhia ni miongoni mwa yale ambayo Walimu wa Ruangwa nao walitaka sana jambo hili liwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niwahakikishie Serikali imeridhia na Wabunge hapa wameliunga mkono na baadaye hapa Wabunge hawa watapitisha ili Walimu sasa nchini kote wakiwemo Walimu wa Ruangwa tutaanza sasa kupata manufaa ya kuwa na chombo chetu, hii Tume ambayo itakuwa inaratibu mambo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pia Mwenyekiti wa Kamati wakati wote ukiwa kwenye jukwaa umekuwa ukinisaidia sana kuniweka vizuri na kunipa uhakika wa kutoa fafanuzi mbalimbali hapa Bungeni na tumeweza kufika hatua nzuri hapa tulipo. Sitamsahau Mwenyekiti wa Kamati na Kamati ya Huduma za Jamii ambayo pia imefanya kazi za elimu wakati wote ilipokuwa inataka ufafanuzi kutoka Wizara ya Elimu na TAMISEMI tumeendelea kushirikiana kikamilifu na hatimaye jambo hili muhimu ambalo leo hii linapewa ridhaa na Waheshimiwa Wabunge liweze kutoa matokeo mazuri kwa Walimu ni matokeo ya Mheshimiwa Mwenyekiti ambaye pia aliwahi kuwa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania na Kamati yake tukufu ambayo imeweza kutupa mchango mkubwa sana wa kufanikisha jambo hili.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya, nianze sasa kuchangia umuhimu wa kuwa na chombo hiki. Kama ambavyo nimeeleza faraja yangu, chombo hiki ni muhimu na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ya kuridhia chombo hiki kuanzishwa, sasa ndiyo tunamaliza matatizo kwa kiasi kikubwa yale ambavyo Walimu walikuwa wanahangaika kwenda huko na huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni shahidi wakati nafanya ziara kwa Walimu kote nchini, tumekuwa tukipokea maoni yao na kuyaratibu na leo hii miongoni mwa maoni yale tunapata muafaka mzuri wa namna ya kuunda chombo hiki. Pamoja na kuunda chombo hiki na kwamba ndicho ambacho kitasimamia, Mheshimiwa Kisangi, aliomba sana kwamba Tume hii kwenye ngazi ya Wilaya, yule Katibu wa Tume aingie kwenye Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili litakuja kuelezwa vizuri sana na Waziri wa Nchi atakapopata nafasi ya kuchangia, lakini nionyeshe umuhimu wa Katibu kuingia kwenye Baraza lile kwa sababu unapofanya *check and balance* Waheshimiwa Madiwani sasa watakuwa majibu ya namna ambavyo Walimu wanaajiriwa, matatizo yao na namna ambavyo wanashughulikiwa kwenye madaraja kwa ukaribu ili waweze kushirikiana kupata muafaka wa matatizo ya Walimu. Kwa hiyo, pendekezo hili ni nzuri na naamini pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi atakapokuja kuchangia atalieleza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Kisangi alizungumzia uhamisho wa Walimu kwamba wako Walimu wanahangaika nchini kwa kupewa masharti ya kumtafuta Mwalimu wa kubadilishana naye, jambo hili halipo, Mwalimu hana uwezo wa kumpata Mwalimu atakayekuja pale anapotoka. Mwalimu anayehama kazi yake ni kuandika barua kwa maelekezo ya sasa, kwenda kwenye halmashauri anayotaka kuhamia na kuomba nafasi na Wakurugenzi wote hili wanalijua kwamba mahitaji ya Walimu katika kila Halmashauri yapo. Kwa hiyo, mwalimu atakachofanya ni kuruhusiwa nafasi ipo aanze utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumewahusisha Walimu tumeondoa tatizo ambalo lilikuwa likijitokeza kwa watendaji la kuhamisha watumishi huko na baadaye tukawa tuna watumishi hewa nchini. Kwa hiyo, sasa uhamisho wa sasa tunamhusisha Mwalimu mwenyewe kwa kuandika barua na kuthibitishwa na Mkurugenzi mahali alipo ndiyo sasa tunadhibiti kuwepo kwa watumishi hewa kwenye sekta ya elimu.

Kwa hiyo, suala la Mwalimu mtafute Mwalimu mwingine hilo halipo nchini na Wakurugenzi wasiwasumbue Walimu kwa kuwaambia watafute Mwalimu mwingine kubadilishana naye, hilo halipo kwenye Sheria ya Utumishi wa Walimu.



Kwa hiyo, Mheshimiwa Kisangi jambo hili halipo na Wakurugenzi wamenisikia na sitarajii kama kuna Mwalimu tena ataambiwa atafute Mwalimu wa kubadilisha naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Marombwa ametoa mchango mkubwa wa kutosha na amezungumzia sana sehemu ya Tume hii kuwa sehemu ya maeneo ambayo tunahitaji kuboresha, uboreshaji kama ambavyo tumeridhia na naomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kama ambavyo tumeonesha *spirit* ya kupitisha Muswada huu ili Tume hii iweze kuwasaidia Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Mkanga alizungumzia sana walemavu, wale Walimu wapate nafasi ya kufanya kazi yao vizuri. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mkanga kwamba, kwa uratibu ambao tumeendelea nao Ofisi ya Waziri Mkuu, suala la Walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum limeratibiwa vizuri, tumetenga na bajeti, bajeti tunayo na wanaendelea kuhudumiwa na pia tumeendelea kuwahusisha hata wanafunzi pia kushiriki mambo yote ya Kitaifa pamoja ikiwemo na ushiriki wa kwenye michezo ambayo sasa inaendelea ya UMITASHUTA na UMISETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili ni kuonesha nia thabiti ya Serikali kwamba, tunawahusisha kikamilifu wale wote wenye mahitaji maalum ili waweze kutoa mchango wao kwenye Taifa hili na inawezekana na pia tumeshatenga fedha za kutosha tu kwa kutengeneza vifaa vile vifaa vyote vinavyotumika katika kufundishia na kujifunzia ikiwemo na vitabu na *machines* zile ambazo zinatumia kuandika makaratasi yao, kila kitu kinaratibiwa pale Uhuru Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale idarani TAMISEMI tuna yule afisa ambaye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Celina Kombani!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na niseme tu kwamba, nawashukuru Waheshimiwa wote ambao wamechangia Muswada huu, mimi ni mdau mmojawapo ambaye nimeshiriki sana katika kutengeneza Muswada huu. Nasema kwamba niwashukuru tu wapiga kura wote, narudi Ulanga Mashariki, naomba waendelee kuwa na imani na mimi, nilichokifanya wao wanakifahamu.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mwajiri, mwajiri ni nani, namshukuru sana Mheshimiwa Cheyo, amesema Walimu ni watumishi wa Serikali. Kwa hiyo, wanaajiriwa na Serikali, hakuna mwajiri mwingine zaidi ya Serikali, ila Serikali ina mamlaka ambazo zinaajiri. Kwa mfano, mamlaka za Serikali za Mitaa, mamlaka ya Tume ya Mahakama, Mamlaka ya Tume ya Bunge, hizo ni *Appointing Authorities*.

Kwa hiyo, *TSC* pia ni *Appointing Authority*, *employer* ni mmoja tu, ni Serikali. *Appointing Authorities* ziko nyingi; Vyuho mbalimbali vimekasmiwa madaraka hayo ya kuwa *Appointing Authorities*. Kwa hiyo, hilo naomba tuelewane na Waheshimiwa Wabunge, kwamba mwajiri ni mmoja tu, Serikali, lakini *Appointing Authorities* ziko taasisi mbalimbali ambazo zimepewa madaraka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la chombo hiki kazi zake. Kazi za chombo hiki, yaani kwa ujumla, ni ajira na usajili wa Walimu katika shule za umma.

Hili tumeliwekea *break down*, tusingeweza kuandika yote kwamba wataajiri, sijui wataingizwa watumishi katika mfumo wa *LAWSON*, watatunza kumbukumbu za Walimu, kuthibitishwa. Hatuwezi tukayaandika yote kwenye sheria, mengine yatakwenda kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pale tumeandika tu yale ambayo ni *main*, lakini tumeshajiandaa na kanuni ambazo zitatoka, ambazo tumeshaziandaa kwa ujumla. Kwa hiyo, mengine ambayo wanasema wajumbe wa Kamati, yatakuwa kwenye kanuni, yako kikanuni zaidi kuliko kisheria. Hilo naomba Waheshimiwa Wabunge watukubalie, ili tuweze kuyaweka kwenye kanuni, maana yake huwezi ukaweka kila kitu kwenye sheria mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu *Vote* au Fungu la *TSC*, tunapoanzisha mamlaka yoyote, tunapoanzisha Tume yoyote, lazima wawe na Fungu lao. Kwa hiyo, katika lile Fungu, litakuwa 20 au vyovyote vile, katika hilo Fungu, kutakuwa na fedha za *PE(Personal Emolument)*, *Development* na *OC*. Kwa hiyo, hata hayo wanayosema ya mishahara yatakuwa *described* kwenye Fungu ambalo litawekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tumeleta *amendment* kama Serikali inayohusu mambo ya mishahara, tumeiweka kisheria zaidi na siyo kuiweka kwamba lazima watafanya hivi, hapana, imewekwa kisheria, naona kwamba inatosheleza.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundo kwamba, muundo huu katika level ya Wilaya, je, Katibu huyo wa Tume atakuwaje! Miundo yote ya Utumishi inashughulikiwa na Ofisi ya Rais, Utumishi, kwa hiyo, hilo litashughulikiwa na Ofisi ya Rais, Utumishi. Kwa hiyo, tunaomba hulo mtuachie litakuwa kama ilivyo kwa miundo mingine ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uhamisho, naomba hapo niweke angalizo, kwamba, tukiruhusu, lazima tuweke angalizo, tukiruhusu kwamba Mwalimu ahame tu, anakotaka kwenda, nawaambia Wabunge, *within no time* vijijini hatutapaa Walimu, lazima tuweke angalizo. Kule kwako Cheyo Itilima hutakuta Mwalimu hata mmoja, wote watahamia Dar es Salaam, wote watahamia Arusha. Kwa hiyo, vijijini tutakuwa na tatizo. Kwa hiyo, jamani, lazima tuweke *mechanism* ambayo tutahakikisha kwamba Walimu wapo vijijini na mijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaingia madarakani, yaani Awamu ya Nne ya Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Wlimu walikuwa na matatizo matatu makubwa, chombo cha Walimu, muundo wa kada ya Walimu, pamoja na madeni ya Walimu. La kwanza, madeni ya Walimu, jamani Awamu ya Nne, tumelipa madeni mengi ya walimu. Tumeshughulikia kero nyingi za walimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, muundo wa utumishi wa Walimu, tayari unaanza rasmi tarehe 1 Julai, 2015, Walimu wanajua hilo! La tatu, ni hicho chombo, tumemaliza, hatukumaliza matatizo yote, lakini tumeyapunguza kwa kiasi kikubwa. Hizo ndiyo kero tatu ambazo zilikuwa kubwa kwa walimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwamba tukubali hicho chombo kianzishwe, kama alivyosema Mheshimiwa Mariam Kisangi, sheria yoyote unapotunga, inaweza ikawa na changamoto zake, huko mbele ya safari kwa kuwa huo siyo msahafu, tutayaangalia hayo matatizo, lakini kikubwa, *the bottom line*, ni kuhakikisha kwamba tunakianzisha hicho chombo na sisi tuko tayari, tutakianzisha hicho chombo. Jamani muundo wake kwa taarifa yenu, tayari, kabrasha hili tumeshaweka vizuri. Kwa hiyo, tuko *serious* na hicho chombo, kinaanza mara moja baada ya sheria hii kupitishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zake za kuanzia ziko kwenye Vote 94, Waheshimiwa Wabunge, tayari mmeshapitisha, zile fedha za TSD zinahamia TSC. Kwa hiyo, fedha za kuanzisha hicho chombo ziko tayari na watumishi wa kuanzia wapo, wale wa TSD tutawahamishia TSC, tutaimarisha zaidi, wale wenye *qualifications*, tutahakikisha tunawaingiza kwenye muundo huu wa TSC.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya vyeo na nini, ni kweli watahughulikia wao, lakini niseme kwamba vyeo na kila kitu, miundo ya utumishi na nini na nini inashughulikiwa na utumishi. Kwa hiyo, sisi tuko tayari tutaitengeneza hiyo bila matatizo yoyote, tunaingia kwenye kanuni, kanuni zinazomhusu Waziri wa Utumishi, tutahakikisha tunaziingiza, Waziri anayesimamia hicho chombo, tutahakikisha tunashirikiana naye, tuzitengeneze hizo kanuni mapema iwezekanavyo ili chombo hiki kiweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anne Kilango, Naibu Waziri wa Elimu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, halafu nianze kwa kusema kwamba, naomba kwa unyenyekevu mkubwa niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Same Mashariki, kwa kipindi hiki cha miaka mitano nimeshirikiana nao kusukuma maendeleo ya Jimbo lile, lakini niwaambie rasmi kwamba narudi sasa, Jimbo la Same Mashariki kwa wana CCM wenzangu, nikiwa na uhakika watanipitisha, niende kusimama kupeperusha bendera, kwa sababu nina uhakika na wao wanajua kwa hakika kwamba nina uwezo wa kupambana na UKAWA na Chama cha Mapinduzi kikashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kuzungumzia kwamba, Wizara yangu inakiri na kuheshimu kilio cha Walimu cha kupatiwa chombo kimoja ambacho kitasimamia utumishi wa Walimu wa Tanzania Bara ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo katika kusimamia utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda nichukue nafasi hii adimu kuwahabarisha Walimu wote wa msingi na sekondari Tanzania Bara kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Nne, imelichukulia suala hili kwa uzito wa kipekee kabisa na leo hii lengo la Muswada huo ni kutunga sheria ambayo itasimamia masuala ya utumishi wa Walimu pamoja na kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana wachangiaji wote, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Margaret Mkanga. Michango yao imetupongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu sana ambao utaweka Walimu wote wa msingi na sekondari Tanzania Bara chini ya Tume ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wote hawa watatu wamekubaliana na Serikali kwamba itakuwa siyo sahihi, wala siyo rahisi, Tume hii kufanya kazi bila kushirikiana na TAMISEMI.

TAMISEMI ndiye mwenye shule, mwenye wanafunzi, mwenye miundombinu ikiwepo pamoja na maabara na kadhalika, TAMISEMI ndiye mwenye vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kwa hiyo, Serikali itaweka taratibu za kueleweka kabisa, za kuifanya Tume hii ifanye kazi yake ya kusimamia utumishi wa Walimu na kushirikiana kwa ukaribu mkubwa na TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kabisa kwamba Walimu ni kundi kubwa la watumishi wa Serikali, inazidi asilimia 50. Malalamiko ya Walimu, ni ya ukweli na yana uzito ambao Serikali imeukubali. Niwasihi Walimu wote wa msingi na sekondari Tanzania Bara kwamba Muswada huu utakaopelekea kupata Sheria ya kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu, ndiyo utakaoweza kutatua matatizo yote ambayo yamekuwa yakiwakumba Walimu na tunakiri kwamba ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundwaji wa Tume hii ndiyo mwanzo wa kuelekea kutatua changamoto hizi. Nawasihi sana Walimu wote wa Tanzania waelewe kwamba, sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inasimama imara kupambana na changamoto zao zote kupitia Tume hii inayoundwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie, kwa unyenyekevu mkubwa, niseme kwamba Walimu wa Tanzania na mimi nikiwa ni Mwalimu wa sekondari, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hilo tunalikubali, lakini wamekuwa wanaitikia kwenye sehemu tatu kuu ambazo wao wenyewe wanazifahamu na mimi nazifahamu. Kwa hiyo, sasa tumefikia mahali tunawaweka kwenye Tume ya Utumishi wa Walimu, ambayo itakuwa inaangalia mambo yote, lakini mwisho wa yote ni kwamba tutakapokwenda kwenye kanuni, tutasimama imara kuziweka kanuni vizuri na Walimu wote watakuwa wanafanya kazi vizuri kama ambavyo wafanyakazi wengine wa Tanzania wanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wambunge, nina tangazo, Mheshimiwa Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pale asubuhi, niliomba Mwongozo wako, lakini naona mpaka sasa sijapata majibu ya Mwongozo ule. Sasa naomba tena Mwongozo kwenye suala lile lile, kwamba ni kwa nini kanuni ya 58 ambayo iko ukurasa wa 37 wa kanuni hizi mpya, inayohusu mabadiliko ya hoja na kuondoa hoja, kwamba ile fasili ndogo ya pili na ya tatu na ya nne zote zikisomwa kwa pamoja zitumike, ambazo zinasema kwamba:

“Mbunge yeyote anaweza akasimama Bungeni na kuomba kuondoa hoja inayoendelea ama hoja ambayo ipo kwenye ratiba ya Bunge.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kukuomba Mwongozo wako kwamba, kwa nini nisipewe fursa ya kutoa hoja ya kuondoa hoja ya shughuli zilizopangwa kufanyika kesho, ili mambo ambayo tuna-*plan* kuyazungumzia yapatiwe ufumbuzi, ndipo Kamati ya Uongozi ikae na kupanga ratiba mpya ambapo sasa tutashughulika na ratiba zilizokuwa zimesalia kwenye Mkutano huu wa Bunge, naomba nipate fursa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla, taratibu...

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Nimeshasimama Mheshimiwa Kigwangalla, mnawahisha mambo halafu mnachelewa wenyewe.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa!

**MWENYEKITI:** Tulieni wala msipate tabu na Majimboni wameshawaona na mtarudi vile vile. Isipokuwa Mheshimiwa Kigwangalla, Mwongozo wako wa asubuhi ambao jibu lake, mamlaka inayohusika itautolea majibu aidha leo au kesho asubuhi.

*(Hapa Wabunge walionekana kutokubaliana  
na jibu la Mheshimiwa Mwenyekiti)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo. Jamani kanuni za Bunge za kuhoji Kiti zipo, haimanishi kuwa bado hatuna muda wa kuwatoa watu na kuwapeleka Kamati ya Maadili. Kwa hiyo, hoja yako hii ya pili, nitakutolea majibu yake jioni leo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia Wabunge Wakatoliki kwamba leo tarehe 8 Julai, 2015 kutakuwa na ibada mara tu baada ya kuahirisha Bunge mchana.

Waheshimiwa Wabunge, nami nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru, inawezekana kwa leo, kwa Bunge hili ikawa ni siku yangu ya mwisho ya kukaa kwenye Kiti au kutoa mchango wowote. Kwa sababu kesho kama ratiba inavyosema kuwa ni siku ya kufunga Bunge, kutakuwa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hatimaye baadaye Mheshimiwa Rais kuja kufunga Bunge.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Pia nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna alivyoniwezesha, amenisaidia, amenipa afya njema, na kukamilisha ngwe hii ya kwanza ya kipindi hiki cha Bunge. Nachukua nafasi hii vile vile kumshukuru Mheshimiwa Spika, kwa mwongozo na ushauri wake, amenisaidia sana kuweza kufanya kazi ya kumsaidia katika Kiti hiki.

Nachukua nafasi kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwongozo alionisaidia kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge. Vile vile nawashukuru Wabunge, bila ninyi shughuli hizi haziendi. Nawashukuru kwa msaada wenu, ushirikiano wenu, hiki kiti kina kazi ngumu sana, siyo kazi rahisi, inahitaji *tolerance*, inahitaji hekima, inahitaji busara kubwa sana.

Namshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Kasilillah, namshukuru Mkurigenzi wa Shughuli za Bunge, Mheshimiwa JJ, kwa msaada ambao amenipa mimi, kuniongoza na kunisaidia kuliongoza Bunge hili. Nawashukuru Watendaji wote wa Bunge, Makatibu ambao wanasaidia Kiti wakiwa kwenye meza. Kwa upendeleo maalum, nawashukuru wahudumu wa Bunge, ambao wanatusaidia kupitisha taarifa mbalimbali humu ndani kwa kazi nzuri waliyofanya. Wakipigiwa hesabu ya kilomita walizotembea humu ndani, kila mmoja inaweza kufika kilomita siyo chini ya 3000 kwa kipindi hiki chote waliokuwa katika uhai wa Bunge hili. *(Makofi)*

Namshukuru mama yangu Mheshimiwa Jenister, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu na Bunge), kwa mwongozo wake. Namshukuru sana *Attorney General*, kunisaidia, namshukuru Waziri Mkuu, kwa namna alivyoniiongoza na namna ya kuendesha Bunge, lakini namshukuru vile vile Mheshimiwa Lowasa, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo. *(Makofi)*

Nawashukuru Wanajimbo wangu wa Ilala, kwa kweli mmelivisha nguo Jimbo la Ilala, mmelipa heshima kubwa sana kwa kushinda Serikali za Mitaa kwa asilimia mia moja na ni Majimbo machache sana nchini Tanzania, labda mawili tu, yaliyoweza kushinda asilimia mia moja. Hii imetokana na ushirikiano na kazi ngumu ambayo mmeshirikiana na Mbunge wenu kuweza kuhakikisha Chama cha Mapinduzi sasa kimeshinda na kinaweza, kitaendelea kushinda, nawapongeza sana Wanajimbo. Nawashukuru sana kwa haya yote ambayo tulifanya nao pamoja.

Jimbo, Waheshimiwa wananchi na Waheshimiwa Wajumbe wa Ilala, si mali ya Mbunge, ni mali ya wananchi wenyewe na kuanzia tarehe 9 Jimbo linakuwa liko wazi, yeyote mwenye kutaka kuja Jimbo la Ilala anakaribishwa.

Aje na nidhamu, aje na heshima ya kuomba ridhaa ya wananchi, anapokuja na mikwara, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa wananchi wa Jimbo la Ilala, yeyote anayekudanganya ujue anakudharau. Kwa hiyo, muwaulize, huko wanakotoka wametoka wapi, wamefanya nini, wanajua nini! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa wananchi wa Jimbo la Ilala, lakini kikubwa nilichojifunza, elimu yangu ya juu ni kuwajali na kuwatekelezea na kuwaheshimu wananchi wangu wa Ilala na wananchi wa Tanzania. Hakuna elimu bora iliyokuwepo, zaidi ya kuwajali wanyonge, kuwajali wananchi wasiokuwa na uwezo ambao wanahitaji mtu madhubuti wa kuwasimamia na kuwatetea hoja zao, ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Haya tumeyafanya wote na mimi nimefanya kwenye Jimbo langu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa wananchi, Jimbo langu halina hoja ya stakabadhi ghalani. Waheshimiwa Wabunge Skatabadhi ghalani nimeisikia Dodoma tu hapa, maishani mwangu sijalisikia hili neno.

Sisi hoja yetu ni nyumba za *National Housing*, nimewapigania wananchi kwa *National Housing* na Bunge hili limesema, wananchi wote, wazee, wastafu, wajane, wagonjwa, watapewa kipaumbele maalum cha kufikiriwa kupunguziwa kodi yao. Hii ndiyo kazi ambayo nimeifanya Jimboni, najivunia sana.

Nimesaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na wafanyabiashara wakubwa wa maduka mbalimbali, Kariakoo na maeneo mengine. Huduma za afya tumezisimamia, wananchi wa Jimbo la Ilala hawahitaji zahanati, zahanati ni kazi ya Madiwani wa Ilala, wakitaka wataomba wananchi wao wawatafutie. Mimi nahudumia mahitaji makubwa ya huduma za afya, hivi karibuni tutaingia mkataba na *National Housing*, tuanzishe hospitali mpya, pale pale Amana, ya kuhudumia wanawake, watoto na wazee, dogo hilo?

**WABUNGE FULANI:** Si dogo, kubwa.

**MWENYEKITI:** Na kuhakikisha uzazi salama kwa akinamama na kuhakikisha *zero death* kwa wazazi ambao wana nini! Pia kuna *X-ray* mpya ambayo tunaweka, sijipigii debe jamani, nasema mambo haya watu waelewe, tunapunguza gharama za *x-ray*, kuwe na *digital* ya kutoka 25,000 mpaka chini ya 7,000. Pia barabara na miundombinu. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo, mimi ni binadamu, lazima nina upungufu wangu, nawaomba radhi wote, ndani ya Bunge, nje ya Bunge, kama nimewakwaza kwa jambo lolote.



**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Naomba radhi, lakini nawatakia vile vile Idd njema Waislamu wote ambao karibu watamaliza mfuno huu wa Ramadhani na niwahakikishie Wanajimbo wa Ilala, kabla ya idd tutakuwa pamoja, tutafanya mambo yetu yale ya kawaida.

La mwisho, niwashukuru tena wote, lakini nasema sasa nawaambia Wanajimbo la Ilala na wote wanaogombea Jimbo la Ilala, ngariba sasa anarudi Jimboni na anaanza kazi yake.

Baada ya maneno haya, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni. Ahsanteni sana.

*(Saa 6.56 mchana, Bunge liliahirishwa hadi Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10:00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) alikalialia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae! Katibu!

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa, mwongozo!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nakushukuru kwa nafasi hii jioni hii. Nilikuwa naomba nipate mwongozo wako, kwa sababu saa hizi ni saa kumi na ushee. Mheshimiwa Kigwangalla alitoa hoja asubuhi kuhusu mwongozo, tukaambiwa kwamba utakuja kujibiwa jioni hii; na jioni ndiyo hii. Baada ya muda tutaanza kujadili hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungependa tupate mwongozo wako ili kuondoa hali ambayo sasa hivi ndani ya Bunge lako kuna sintofahamu, na Wabunge wako hawa hatuelewi kinachoendelea.

Ili tuelewe kinachoendelea, hebu tuweke vizuri tujue nini kinaendelea, tuwe na amani ndani ya Bunge lako, na tujadili suala lililoko mbele yetu kwa amani na utulivu kwa kutumia akili zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa unavyotuona, sintofahamu ndani na nje ni kubwa ni kubwa ni kubwa zaidi. Tungependa kupata maelezo ya Kiti lile lililoulizwa na Mheshimiwa Kigwangala asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa wabunge, nawaomba sana tuwe na subira kidogo. Hivi sasa ninavyoongea Tume yetu ya Huduma za Bunge inakutana na Mheshimiwa Spika. Kuna *briefing* muhimu ambayo wanaifanya na kutokana na *briefing* hiyo ndiyo tunaweza tukajibu suala ambalo Mheshimiwa Dokta Kigwangala na vilevile Mheshimiwa Ndassa wameliweka mbele yetu. Kwa vile kikao kinaendelea hivi sasa, mimi naomba tuendelee na shughuli zetu. Tutakapopata tu maelezo ya nini kinaendelea, tutawafahamisha.

Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tulianza vizuri, tumeendesha vizuri, tumalizie vizuri kwa uvumilivu. Kwa hiyo, nawaomba sana tuendelee na shughuli zetu, mara tu nitakapopata majibu yoyote yale nitawaambia.

Mheshimiwa, bado?

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado kidogo.

Sisi Wabunge wako kama kujitolea, tumejitolea vya kutosha. Jambo hili tulipokuwa kwenye Ukumbi wa Msekwa tuliambiwa kesho mambo yatakuwa mazuri. Leo ni Jumatano, Bunge linavunjwa kesho, siku haziko na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuliona jambo hili ni dogo, lakini ni jambo kubwa kweli kweli. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama kujitolea tumejitolea vya kutosha kwa ajili ya Serikali yetu na chama chetu, ndani na nje. Mimi niwaombe Wabunge wenzangu, kwa nia nzuri kabisa...

**MBUNGE FULANI:** Tukuunge mkono!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Kama inawezekana, tuahirishe kikao hiki, tusubibiri Makamishina waje au Spika aje atueleze. Jibu kama ni ndiyo tuendelee. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja, toa hoja!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja ya kuahirisha kikao chako.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa heshima na taadhima niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ajenda iliyoko mbele yetu ya kujadili chombo kinachowahusu walimu ni ajenda muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sio siku ya mwisho ya Bunge letu Tukufu, bado tunayo kesho, tunao usiku mzima leo. Niwaombe Waheshimiwa, tutumie busara sana sana sana. Kama ni mtihani nadhani tumeufaulu, mimi naona kama tunataka kufeli dakika ya mwisho. Tuungane na Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu ya Uongozi iko kwenye kikao. Ingekuwa ni busara sana tukasikiliza maamuzi ya Kamati ya Uongozi ndipo sisi tukatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi yetu, kwa maslahi ya chama chetu, naomba sana san asana tuendelee na kazi iliyoko mbele yetu, wakati Mheshimiwa Naibu Spika unawasiliana na Kamati ya Uongozi. Mimi nina uhakika kabisa kabla ya kufika saa kumi na mbili, Kamati ya Uongozi itakuwa imetuletea yale waliyoafikiana katika kikao chao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, langu ni kuwahoji tu, tuendelee au tuahirishe?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisema tuendelee  
na wengine walisema tuahirishe)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee, tuendelee!

**MBUNGE FULAN:** Tuahirishe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lekule, nimekuona umesimama, unataka kutushauri ee?

**MHE. MICHAEL L. LEKULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Seriklai imeona hali ya Wabunge ilivyo na sisi tunaiheshimu Serikali, tunakuheshimu wewe. Tunaomba hili tunalolisema Serikali iwekee maanani na itimize. *(Makofi)*

Nawaomba tu Wabunge wenzangu, tuendelee tumalize kiporo hiki, kwa sababu tumeishaanza, tumemaliza na bado siku ya kesho; na jambo hili linazungumzwa kwenye mkutano.

Wale Wabunge tuliowachagua walioko kwenye kikao, ambao ni Tume, wako kwenye shughuli na wanatetea maslahi yetu. Naomba niwaombe Wabunge wenzangu tukubali kuendelea. Tukimaliza, kwa sababu ni kupitisha tu, bado tunaweza tukaendelea na *Party Caucus*. Naomba tumalize hili, lakini twende kwenye *Party Caucus*. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kwa busara ambayo nimeiona hapa, tuendeleo. Nawaomba sana tuendeleo tuifanye hii kazi iliyoko mbele yetu. Lakini *front bench* ni vizuri mkaelewa kwa nini nilikuwa nasimama na nasita, sisiti kwa sababu ya hili la leo jioni, hili tutalifanya, nilikuwa nasita kwa sababu ya la kesho ambalo ni kubwa la muhimu zaidi, litatuletea shida. *Caucus* haisaidii, ni wenzetu kulibeba hili na uzito wake kujua kwamba jambo hili lilipofikia ni mahali ambapo lazima kufanyiwa kazi vinginevyo kwa kesho itakuwa mbaya sana. Ndiyo maana mlikuwa mnaona nasimama kidogo, napata tabu kwa sababu inaweza ikawa ni aibu ya mwaka kidogo. Ahsanteni sana. Mheshimiwa Mama Hawa ghasia, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, tafadhali mchango wako. Tunaanza suala letu moja kwa moja sasa.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo, mwenye hoja, mimi nachangia!

**NAIBU SPIKA:** Ahaa, mwenye hoja, sawa, hapo hapo. Dakika ngapi?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ishirini.

**NAIBU SPIKA:** Dakika ishirini. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi anazozifanya katika kuangalia na kuyasimamia maslahi ya watumishi wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais tangu aingie madarakani amekuwa kila mwaka akihakikisha kwamba maslahi ya watumishi yanaboreshwa; na katika kipindi chote cha miaka kumi hakuna mwaka hata mmoja ambao umepita bila mishahara ya watumishi kuongezwa; na mara zote amekuwa akitoa maelekezo hata pale watendaji wamekuwa wakisita na kutoa

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

visingizio vya kila aina, lakini kama muhimili Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa maelekezo kwamba lazima mshahara uongezeke japo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia amekuwa mbele kusikiliza makundi yote ya watumishi na kuhakikisha kwamba anatatua kero ambazo zinawahusu watumishi wa kada zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa walimu kwa kweli Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi sana kuhakikisha kwamba kero za walimu zinatatuliwa kwa wakati. Hata suala la kuondoa walimu kutoka Wizara ya Elimu na kuwapeleka TAMISEMI ilikuwa ni katika harakati za Mheshimiwa Rais kuhangaika na kutafuta njia gani ambazo ataondokana na kero za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya walimu kupeleka TAMISEMI, walimu wa sekondari suala la kupanda vyeo kwa kweli ilikuwa ni changamoto kubwa. Kazi kubwa ambayo TAMISEMI ilifanya ikiwa ni pamoja na halmashauri kwa walimu wa sekondari mara tu baada ya kuhamishiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni kuhakikisha kwamba wanapandishwa vyeo kwa wakati; na wale ambao kwa muda mrefu walikuwa hawajapandishwa cheo tulihakikisha kwamba wanapandishwa kwa mseleleko na kuwaweka kwa mujibu wa walivyoajiriwa kwa sababu kipindi kile kulikuwa na neno la mlundikano wa watumishi katika cheo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Wizara ya Elimu na naungana na Kamati kuhakikisha kwamba chombo cha pamoja cha walimu kinaundwa kama jitihada za kuhakikisha kwamba kero zao zinaondoka na kama mojawapo ya hatua ambazo Mheshimiwa Rais ameona kwamba zitasaidia kwa kiwango kikubwa kuhakikisha kwamba walimu wanaondolewa kero zao. Katika kuhakikisha kwamba walimu wanaajiriwa, wanapandishwa kwa wakati na wanarekebishiwa mishahara yao kwa wakati, Mheshimiwa Rais aliridhia pesa zitolewe ili kuhakikisha kwamba mfumo wa *low zone* toleo la tisa unafika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zoezi hilo lifanywe kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge watakuwa mashahidi, walimu wenyewe watakuwa mashahidi na Chama cha Walimu kitakuwa ni shahidi. Kabla ya hapo ilikuwa ni suala la kawaida mwalimu anaajiriwa na tunakaa zaidi ya miezi sita walimu hawajapata mshahara. Sasa hivi suala hilo imebaki ni historia. Sasa hivi tunavyozungumza, mwezi Mei Serikali ilipeleka awamu ya kwanza walimu 28,007, na kati ya hao 26,046 walikuwa wameripoti. Mwezi Mei huo huo walimu 23,180 walikuwa wameingia kwenye *payroll* na kupata mishahara.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili napenda niishukuru sana Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliamua kwa makusudi kuchelewesha kufunga ule mfumo kwa sababu kuna tarehe maalum ambayo ikifika ni lazima iwe ni mwisho wa kuingiza watumishi kwenye *payroll* ili waweze ku-*print* na kuhakikisha kwamba mishahara inafika kwa wakati. Lakini Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma mwezi Mei walichelewesha makusudi mishahara ya watumishi wengine ili kuhakikisha tu walimu walioripoti waweze kuingizwa kwenye mfumo na waweze kupata mishahara mwezi ule ule kama ambavyo wamepangwa. Kwa hiyo, wale wote ambao walikwenda mwezi Mei kwa wakati bila matatizo ya vyeti na matatizo mengine, waliingia kwenye *payroll* na walipata mishahara. Kati ya wale walimu 26,000 ni walimu 2,866 tu ndio ambao walikuwa hawakupata mishahara, na sababu ni kwamba baadhi yao walikwenda bila vyeti, na baadhi yao walikosea katika ujazaji wa fomu za kutuma kwenye mtandao.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei huo huo mwishoni tulipeleka walimu wengine na kufanya jumla ya walimu waliotumwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, walioajiriwa kufikia 33,777. Mwezi Juni huu, kati ya hao walimu 33,777 walimu 32,000 wameingia kwenye *payroll* na wamepata mishahara. Ni walimu 1,577 tu ambao hawajapata mishahara mpaka leo, kitu ambacho kwa miaka ya nyuma tulikuwa tunaajiri walimu 2,000 tu au walimu 3,000, lakini, hao hao ilikuwa inatuchukua miezi sita kuhakikisha kwamba wanaingia kwenye *payroll* na wapata mishahara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maboresho ambayo yamefanywa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya utumishi wa Umma kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara zote kuingiza wenyewe watumishi wanaoajiriwa na kuwaondoa pale wanaostaafu wanapostaafu au wanapoacha kazi, sasa hivi suala la kuchelewa watumishi kupata mishahara yao kwa kweli limetatuliwa kwa kiasi kikubwa, na napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Celine Kombani kwa kulisimamia hilo pamoja na timu yake ya Utumishi. Pia niwashukuru sana kwa kutuvumilia kwa sababu walimu wengine walichelewa kufika katika vituo, tuliwaomba kwamba watusubirie, pamoja na kwamba wamewachelewesha watumishi wengine kupata mishahara wa mwezi Mei, lakini walitusaidia watumishi wetu hasa walimu kupata mishahara kwa wakati na kwa muda unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi tena kuungana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Kamati katika mapendekezo waliyoyatoa, lakini naungana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuweka angalizo katika suala zima la uhamisho wa watumishi.

## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwalimu angependa apangiwe mjini na kila mwalimu angependa apangiwe Dar es Salaam. Sasa hivi tunavyozungumza kuna halmashauri ambazo hazihitajiki kupelekewa mwalimu hata mmoja kwa sababu walimu waliopo wanatosheleza na wana ziada kubwa. Tuna halmashauri ambazo bado zinahitaji kupelekewa walimu zaidi. Sasa ili mwalimu aweze kuhamia na kuhamia katika halmashauri nyingine, ni lazima halmashauri anayohamia kuwe na nafasi ya kumpokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule ambazo zina vyumba vya madarasa 30, zina Walimu 100, kwa hiyo, katika kila muda walimu 30 wako madarasani wanafundisha na walimu 70 wamekaa. Kwa hiyo, katika hali ya kawaida hawezi mwalimu tena aombe kwenda katika shule hiyo aweze kuruhusiwa. Kwa hiyo, hata kama tukiunda chombo, nina imani kabisa watakaokuwa kwenye chombo hicho ni watu wenye busara, wataangalia uwiano wa walimu katika shule na wilaya; na hatutegemei kwamba watapeleka watumishi katika halmashauri ambazo tayari zimejitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naungana na mambo mengine yaliyopendekezwa, lakini suala la kusema chombo kilipe mishahara, suala la mishahara sio suala tu la kukaa pale dirishani na kulipa bali ni mchakato mrefu na ni mchakato unaohitaji watumishi wengi wa kutosha. Kama tutataka kila wilaya ilipe yenyewe mishahara ndiyo kusema kwamba tutaandaa vitengo vya fedha au idara za fedha na utawala mbili katika kila halmashauri. Kuwe na idara ya uhasibu kwa ajili ya halmashauri nzima na kuwe na idara ya uhasibu kwa ajili tu ya chombo hiki katika ngazi ya wilaya, kitu ambacho sifikirii kama ni matumizi sahihi ya rasilimaliwatu na rasilimali fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuwe wakweli, wote tunakaa katika halmashauri zetu, siku ambayo analipwa mwalimu ndiyo siku hiyo analipwa daktari, analipwa afisa kilimo na kila mtumishi aliyepo katika halmashauri. Katika halmashauri zetu hatuna siku ya kulipa walimu na hatuna siku ya kulipa watumishi wengine. Kama watumishi wote wanalipwa kwa siku moja ambapo mishahara unafika na hatujawahi kuwa na matatizo, kwa nini tufike mahali mpaka katika halmashauri kule Waheshimiwa Madiwani na watendaji waliopo pale wajione wanyonge kwamba hawaaminiwi kwa kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba kwenye halmashauri zetu hao hao Madiwani na hao hao watendaji waliopo pale ndiyo wanaotufanyia kazi zote hizi ambazo tunasimama na kujisifu kwamba tumetekeleza ilani ya chama vizuri. Hebu tuwaamini, kama wanaweza kuwalipa watumishi wengine, basi tuwaamini kwamba wanaweza kuwalipa na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya ajira, *promotion* na nidhamu mimi sina mgogoro wowote, naona ni sawa yafanywe na chombo, lakini hili la mshahara kwa kweli mimi naomba Waheshimiwa Wabunge tuliangalie mara mbilimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake ambazo kwa kweli amezifanya katika kuwahudumia na kuangalia maslahi ya watumishi wa umma. Amehakikisha kwamba kodi ya makato ya mishahara inapungua kutoka 18% mpaka 11%, punguzo la zaidi ya 7%. Lazima tufike mahali tumpungeze. Pia amekubali kuhakikisha kwamba kero za watumishi zinaondoshwa na kwa kiasi kikubwa kwa kweli kero nyingi za watumishi kwa kipindi chake zimeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtwara na mimi ni miongoni mwa ambao wanawahudumia walimu na kuwatunza walimu nadhani kushinda Wabunge wengine wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Juma la Elimu nimetoa zawadi kwa walimu wote waliofanya vizuri pamoja na wanafunzi katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini. Mwalimu aliyeongoza kwa kufanya vizuri kwenye somo la Kemia, nimempa tiketi ya kwenda Dubai, nimemlipia tiketi ya ndege kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na nimempa tiketi ya kwenda Dubai, nimemlipia hoteli na tayari amekwenda tarehe moja na tarehe sita amerudi. Mwalimu wa pili nilimwambia achague Mkoa wowote anaotaka kwenda Tanzania, alichagua kwenda Zanzibar na nilimlipia tiketi ya ndege kutoka Mtwara mpaka Zanzibar yeye na mke wake, walikaa wiki nzima na wamerudi. Mwalimu wa tatu naye aliomba yeye ana matatizo ya kifamilia nimpe pesa tamslimu, nimempa. Shule zilizofanya vizuri niliahidi kuweka solar na nimeweka kwenye nyumba za walimu, nimebaki kutimiza ahadi moja ya pikipiki na yenyewe nitatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na motisha zinazotolewa na Serikali, mimi kwa kuwajali walimu kwenye wilaya yangu nilihakikisha sherehe inafanyika na tuzo binafsi ninatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naungana na yale yaliyopendekezwa na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa nakuomba mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Dokta Shukuru Kawambwa, karibu sana.

Dakika ngapi, Katibu?



**KATIBU:** Dakika 40!

**NAIBU SPIKA:** Una dakika 40, lakini kama unavyoiona hali ya hewa ukifanya kifupi zaidi itakuwa bora.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natangulia kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupa uhai na afya na kuniwezesha mimi kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kufanya majumuisho ya hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana wewe mwenyewe lakini pia Mheshimiwa Spika na Wenyeviti kwa kuliendesha vyema Bunge letu kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano. Wewe na Mheshimiwa Spika mmesimama imara hata nyakati ngumu zenye majaribu tele katika uendeshaji wa Bunge na wala hamkutetereka. Namwomba Mwenyezi Mungu awaajalie afya nyingi, uwezo, hekima na busara ili mtuwezeshe kuhitimisha Bunge letu pia kwa amani na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Katibu wa Bunge na Watumishi wote wa Bunge kwa kulihudumia vyema Bunge na kutuwezesha sisi Wabunge kufanya kazi zetu vizuri.

Namshukuru na kumpongeza Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa George Masaju na *Chief Whip*, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama kwa utendaji wao mzuri ambao umechangia sana uendeshaji mzuri wa Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za pekee kwa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kutusimamia vyema katika Kamati, wamekuwa makini, waangalifu na wamefuatilia mambo yote ambayo Serikali ilikuwa inawasilisha katika Bunge hili Tukufu kupitia Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, najua kuna vipindi vilikuwa vizito na vingine vyepesi, lakini umakini wao umetusaiaia kufanya kazi vizuri zaidi na kuhakikisha kwamba elimu inaboreka katika nchi yetu.

Mwisho, nawashukuru Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano ambao mmenipa kwa kipindi hiki cha miaka mtano. Bila ushirikiano mkubwa wa Wabunge, kazi hii ambayo tumeifanya mimi kama Waziri pamoja na Wizara yangu kwa kipindi cha miaka mitano sidhani kama ingeweza kufikia hapa ambapo tumefikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hii itakuwa mara yangu ya mwisho kusimama katika Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu wa 20 na wa mwisho wa Bunge lako Tukufu, basi nichukue fursa hii kuwashukuru awali kabisa wananchi wangu wa Jimbo la Bagamoyo kwa kunipa fursa hii ya kuwawakilisha

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bungeni kwa vipindi viwili, wamenipa ushirikiano mkubwa na mimi nimewatumikia kwa kadri ya wezo wangu na kwa unyenyekevu na umakini mkubwa. Bagamoyo ya mwaka 2015 sio Bagamoyo ya mwaka 2010.

Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru mno na kuwapongeza kwa ushirikiano mkubwa mlionipa na niseme tu kwamba, naomba nitangaze kwamba narudi tena na nina imani kuwa mtanipokea vyema ili tuweze kuendeleza kazi ambayo tumeanza kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi, sasa naomba kwa niaba ya Waziri Mkuu niongelee Muswada wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu nchini mwetu wamekumbwa na changamoto kadhaa zikiwemo madeni ya walimu, kupanda madaraja, muundo wa utumishi, utitiri wa mamlaka zinazimhudumia mwalimu na kadhalika. Lakini, mambo haya manne ni mambo makuu ambayo kila mara walimu wameyapigia kelele kwa Serikali yao na kutaka Serikali ichukue hatua madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii sikivu ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi mahiri wa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila wakati imeshughulikia matatizo haya. Madeni kama suala la kwanza Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba madeni haya yanafutwa. Kila mahali tunapokwenda sasa kadhaa hii imekuwa nyepesi zaidi sio kama ilivyokuwa; na niseme tu hivi sasa tunatarajia ndani ya mwaka huu 2015 kufikia mahali pale ambapo mimi kama Waziri mwenye dhamana ya elimu naweza kuwatangazia umma wa walimu wote katika nchi yetu kwamba madeni yote tumeyafuta. Hizi ndiyo hatua ambayo Serikali yenu imezichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali imepambana na upandishaji wa madaraja na kuboresha hali ya upandaji wa madaraja kwa walimu wetu kwa ngazi mbalimbali mwaka hadi mwaka. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) tayari ametoa maelezo kuhusu jambo hili na sitaongezea hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa utumishi wa walimu umetoka ambao walimu wameupenda sana na wamefurahi na kwa hilo tu nadhani mambo mengine mengi sana yamefutika kwamba, sasa tuna muundo wa utumishi ambao walimu wameuridhia, wameupenda na unawafungua walimu kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa na kwa mafanikio makubwa ambayo tumeanza kuyaona kwa miaka hii ya karibuni.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, utitiri wa mamlaka zinazomhudumia mwalimu ndilo jambo ambalo lilikuwa la mwisho kubwa ambalo Serikali imelisikiliza kwa walimu na sasa leo imewasilisha katika Bunge hili Tukufu ili Waheshimiwa Wabunge walijadili kwa kina na kwa umakini ili sasa baada ya leo kama Bunge lako Tukufu litapitisha Muswada huu, maana yake kadhia hii nayo itakuwa imewekwa pembeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kwamba Wabunge tutashirikiana vizuri sana katika kuhakikisha kwamba Muswada huu umejadiliwa vyema na kwa umakini kama sisi tulivyojipanga upande wa Serikali kuhakikisha mambo ambayo ni upungufu katika Muswada tunayarekebisha vilivyo ili tupate Muswada ambao utaweka chombo cha kumhudumia mwalimu chenye ufanisi ule ambao walimu nchi nzima wanautegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa majadiliano ya Muswada huu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 13 wamechangia kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge wawili wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ambayo yamewasilishwa na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, naomba haya niyatolee ufafanuzi wa mwanzo kabisa na nitachukua masuala makubwa ambayo yanahitaji ufafanuzi wa bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limeongelewa tayari na Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia hususani suala la kuhusu mwajiri wa mwalimu kwamba, nani ni mwajiri wa mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limetolewa ufafanuzi katika mapana yake kwa kusema kwamba mwalimu ni mtumishi wa umma na watumishi wa umma wote nchini mwajiri wao mkuu ni Serikali. Sasa kwa kujua kwamba hili limezungumzwa sana na Kamati yangu na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ameliwasilisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba kuna tume nyingine ambazo zimeundwa ndani ya nchi yetu kama vile Tume ya Mahakama, Tume ya Majeshi ambayo inajumuisha Polisi na Zimamoto na kadhalika; na kuna mamlaka nyingine pia ambazo kwa namna moja ama nyingine hizi zimepewa uwezo wa kuwa mawakala wa ajira au wao ndiyo mamlaka ya ajira kwa maana kwamba ingawa sasa Serikali ndiyo mwajiri wa kila mmoja, lakini mamlaka ya ajira ya watumishi hao inakuwa kwenye tume fulani au mamlaka fulani. Kuna utaratibu maalum ambao umefanywa kwenye tume hizo na umefanywa katika mamlaka nyingine ambazo zimeundwa chini ya sheria mbalimbali.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wakala kwa mfano TANROADS na wakala nyingine ambazo pia nazo zina mamlaka ya ajira. Taratibu hizo zitatumika pia katika tume hii kwamba tume itakuwa ni mamlaka ya ajira kwa maana hiyo itaweza kuwaajiri watumishi wake, itawasambaza watumishi hao kwa maana ya walimu katika halmashauri mbalimbali na itawasimamia katika upandishaji wao wa madaraja na pia itawasimamia katika suala zima la nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namna nyingine ya kufanya nje ya utaratibu ambao upo kikatiba na nje ya utaratibu ambao Serikali imeweka katika tume, sio tume hii, lakini na tume nyingine zote ambazo zimeundwa mpaka hivi sasa, namna ile itakuwa ngumu sana kwa Serikali kuifanya na pengine isilete ufanisi ule ambao tunautarajia kwa ajira ya mwalimu, kwa sababu hapa kilicholengwa kikubwa sana ni ufanisi katika kumuweka mwalimu ajue mwajiri wake ni nini kwamba, sasa hahitaji tena kuzunguka kwa mamlaka hizi chungu nzima, Ofisi ya Rais Utumishi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na kadhalika, hapana, wao moja kwa moja wanaangalia Tume ya Utumishi wa Walimu na ndiyo mamlaka ya ajira ya mwalimu na mambo yote yanamazikia pale pamoja na kusaini mkataba wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili naomba niombe Kamati ya Huduma ya Jamii kwamba hili halina utata sana, hili ni jambo ambalo tunalifanya katika taratibu mahsusi za kiserikali ambazo zimeleta mafanikio katika nyanja mbalimbali kama nilivyotolea mfano Mahakama na tume nyingine ambazo tunazo na hatujasikia malalamiko huko na wao wanafanya shughuli zao vizuri bila ya matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kulipa mishahara, naomba kufafanua kuhusu hoja hii ambayo inataka kwamba, tume ilipe mishahara. Lakini, kama nilivyofafanua katika hoja iliopita ya mwajiri, naomba kusema kwamba, kwa sababu walimu ni watumishi wa umma, kwa hiyo, Serikali Kuu kupitia kasma mbalimbali ndiyo mlipaji mishahara ya walimu. Kwa vile walimu ni watumishi wa umma basi watalipwa mishahara yao na tume katika kasma ya tume ambayo tayari sasa hivi kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi ametaja awali kwamba tayari tuna kasma 94 ambayo ni ya Tume ya Utumishi wa Walimu na kasma itakayotengenezwa ndiyo ambayo itatumika kwa ajili ya kuwalipa walimu. Lakini, pesa inatoka wapi, nani atatafuta pesa na nani atatoa pesa, hii ni Serikali Kuu na pale tunaposema mlipaji mkuu ni Serikali, basi ni kwa maana kwamba Serikali ndiyo ambayo yenye watumishi wote wa umma na yenyewe ndiyo italipa mishahara, lakini inalipa mishahara kupitia taratibu mbalimbali, mojawapo ni kupitia katika vote hizi zinazohusiana na tume ama wakala mbalimbali. Kwa hiyo, mishahara utalipwa ndiyo na tume itahusika katika kulipa mishahara kapitia kasma zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili niombe kwa heshima na taadhima kwa Kamati yangu kwamba halina utata, halina utata kwenye tume zingine, halina utata katika taasisi zetu, wakala zetu nchi nzima, kwa hiyo, nategemea halitakuwa na utata kwa Tume ya Walimu na kwa walimu kwa ujumla kwamba tume yenyewe itasimamia jambo hili kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la sifa za Mwenyekiti na Katibu wa Tume. Suala hili, Kamati imependekeza kwamba sifa zao zianishiwe. Naomba kusema kwamba, Serikali inakubaliana na pendekezo la Kamati na kifungu husika kimefanyiwa marekebisho kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ili kuweza kuingiza mapendekezo ya Kamati ya Huduma za Jamii.

Aidha, napenda kutoa maelezo kuwa; kwa kuwa wajumbe wa tume watatokana na nafasi zao katika utumishi wa umma, kwa hiyo bila shaka watakuwa wanakidhi sifa hizi. Kwa mfano, kuna wajumbe wa tume ambao wameelekezwa kwamba wajumbe hawa wanatoka Chama cha Walimu. Hatutegemei kwamba Chama cha Walimu kitaleta katika tume wajumbe ambao hawana sifa za ujumbe. Lakini pia, kuna ambao wanakuja kutoka Serikalini, kutoka Wizara ya Elimu na kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kuingia kama wajumbe katika tume hii. Nina imani kwamba vigezo hivi vyote ambavyo vimeanishwa watakuwa wameweza kuvikidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na hapa nimtaje Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir ambaye alitaka na walemavu nao watengewe nafasi maalum katika tume ile. Sasa najua kwamba, katika sheria ya sasa na hata sifa ambazo zimeanishwa na zimeletwa pia na Kamati hazikuweka angalizo hilo, lakini nina imani katika uteuzi wa wajumbe katika tume hii bila shaka kwa nia njema kabisa na kwa kujua changamoto maalum ya ndugu zetu walemavu, basi suala hili litazingatiwa ili sauti ya walemavu nayo iweze kusikika miongoni mwa wajumbe wa Tume ya Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu uteuzi wa Katibu wa Tume na Kamati imelihoji hili na ilipendekeza kwamba huyu Katibu wa Tume asiteuliwe na Mheshimiwa Rais, asiwe mteuliwa bali awe mwajiriwa na tume kwa njia ya kutangazwa kwa nafasi na kugombaniwa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi tungependa kusesitiza kwamba ni vyema Katibu wa Tume ateuliwe na Rais kwa mujibu wa Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyo kwa watendaji wakuu wa taasisi nyingine za Serikali. Hii ni nafasi maalum na nafasi nyeti katika utumishi wa Serikali na kama vile kwenye taasisi zingine muhimu sana Mheshimiwa Rais amechukua wadhifa huu kupitia Katiba ambayo inampa uwezo wa kuweza kumteua Katibu.

## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kamati na Wabunge waridhie hilo ili tumpate Katibu Mtendaji ambaye ataweza kuiongoza tume hii vizuri na kwa ufanisi kwa walimu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imependekeza kuongeza wawakilishi wa idara ya ukaguzi na wawakilishi wa vyuo vya ualimu kwenye tume hii. Napenda kufafanua kuwa Serikali imelipokea jambo hili kwa mikono miwili, katika kuteua mwakilishi wa Wizara ya Elimu suala hili litazingatiwa. Kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina mwakilishi kule na kwa bahati hivi sasa Idara ya Ukaguzi bado iko katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika sheria tukisema tumuweke mwakilishi kutoka Wakala wa Ukaguzi, wakala hii bado haijaundwa mpaka hivi sasa na haiwezekani katika sheria itakayotungwa itaje wakala ambayo haipo, labda kwa kutegemea kwamba itakuwepo, tuna mategemeo makubwa kwamba itakuwepo. Lakini wakati huu tunaunda sheria hii, wakala ule haupo. Kwa hiyo, ndiyo maana nilisema kwamba basi Wizara itazingatia wakati inateua mjumbe wake, basi mjumbe huyo awe anatokana na idara ile ya ukaguzi.

Kwa hiyo marekebisho yatafanywa katika jedwali la marekebisho ili hili liweze kuzingatiwa, lakini pia uwakilishi wa bodi ya kitaalam ya walimu kwa kuwa bodi hiyo bado haijaundwa nayo pia wawakilishi ambao wameombwa na Kamati, pia inafanyiwa marekebisho katika jedwali la marekebisho ili tuweze kuona namna ya kumpata mtu wakati huu ambao hatuna bodi ya kitaalam ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine ambalo Kamati ya Huduma za Jamii imependekeza ni kwamba walimu wasaini mikataba ya ajira kabla ya kuripoti kwenye maeneo yao ya kazi na sio barua za makubaliano kama ilivyoonyeshwa katika Muswada huu wa sheria. Serikali inaridhia mapendekezo hayo, inakubaliana na mapendekezo ya Kamati; na kwa maana hiyo Serikali inarekebisha Kifungu cha 12(1)(c) na kukiandika upya kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho kuendana na mahitaji yale ambayo Kamati imezungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia hoja ya tume kuongeza wigo wa mapato ambayo imeongelewa na Kamati na pia imeongelewa na baadhi ya Wabunge. Serikali imelitafakari pendekezo hili la tume kuweza kuongeza wigo wa mapato, kwamba isiwe tu mapato yale ambayo yameanishwa huku katika Muswada yale yanayotokana na Serikali tu, lakini waweze kupata wigo wa mapato katika maeneo mengine.

Serikali imetafakari pendekezo hili na kuona tume itaweza kupokea zawadi, itaweza kupokea misaada na mikopo kwa mujibu wa sheria zinazosimamia masuala ya fedha za umma. Hilo tunaliafiki na litafanyiwa marekebisho ili tuweke katika Muswada ili jambo hili nalo liwezekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba kuna masuala mengine mengi ambayo yamehojiwa, yameletwa kama majedwali ya marekebisho, moja la Serikali, lakini na ya Wabunge mbalimbali, tutapata fursa ya kuweza kutolea ufafanuzi moja baada ya lingine katika vifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutolea ufafanuzi masuala haya makubwa, naomba sasa niseme na nichukue fursa hii kuwasihi tena Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu, waweze kuujadili Muswada huu kwa umakini, lakini pia kwa unyeti wake wa kuhakikisha kwamba kilio hiki kikubwa cha walimu sasa kinafikia mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba hakuna ukamilifu katika jambo ambalo binadamu analifanya, yote yale ambayo sisi binadamu tunayafanya yana upangufu wake. Bila shaka katika Muswada huu na sheria tutakayoitunga pengine kutakuwa na upungufu wa hapa ama pale, lakini mwanzo tuwe tumeuweka kwamba, chombo hiki walimu wawe wamekipata, wapate chombo chao na Bunge letu sio Bunge la mwisho kabisa katika dunia hii aliyounda Mwenyezi Mungu, kuna Mabunge yatafuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge ndilo lenye dhamana ya kutunga sheria, upungufu wowote ambao sisi tutakuwa hatukuona au kuurekebisha, basi utakuja kurekebisha hatua kwa hatua katika Mabunge yanayofuata ili baadaye walimu wawe na chombo kinachowahudumia wao kwa namna ambayo wanaipenda na kwa namna ambayo inawaletea ufanisi na kwa namna ambayo watakumbuka kila siku kwamba ni Bunge hili ndilo ambalo limepitisha chombo hiki ambacho wamekilia muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu!

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**NAIBU SPIKA:** Kuna nini tena Mheshimiwa Said Nkumba? Naomba make kidogo Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

Waheshimiwa Wabunge walioko ndani ya Bunge wamekuwa kwa kauli moja wakitetea kwa dhati kabisa suala la walimu ambalo ndilo kundi kubwa sana la wafanyakazi Tanzania, kuhakikisha walimu wa Tanzania ambao wanafanya kazi kubwa sana; na Waheshimiwa Wabunge kwa muda mrefu sana wamekuwa wakitetea kwamba hawawezi hawa walimu wakaendelea kubaki kwenye tume ya pamoja inayojumuisha watumishi hiyo; na kwa maana hiyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiomba sana kwamba lazima warudi kwenye utaratibu wa mfumo wa zamani. TSC iliwasaidia sana walimu kuwafahamu, kutambua na kutatua matatizo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwamba, jambo hili ni jambo kubwa, ni jambo nyeti, hatuwezi kupitisha jambo hili kama ambavyo tulivyokuwa tunatarajia sisi. Mafanikio makubwa sana ya kuwaondoa walimu ni kuwapa tume yao ambayo watajitegemea wao wenyewe.

Kwa hiyo, naomba sana, jambo hili ni tete, ni nyeti, kabla hatujaenda kwenye vifungu na kwa sababu wengi waliobaki hapa ni Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, naomba sana twende tukajadiliane kwa maslahi ya walimu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, unapendekeza muende kwenye caucus?

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Naomba nipendekeze tuahirishe, twende kwenye caucus tukakae, tuzungumzie maslahi ya walimu, halafu baadae turudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote baada ya hapa muende ukumbi wa Msekwa.

*(Saa 10.51 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Tarehe  
9 Julai, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*